# Nipashe

Alhamisi Januari 23, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580135

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## NIMR yatangaza kuanza kutibu tezi dume kutumia miti shamba

UKURASA 3



ama

ALHAMISI JANUARI 23, 2020

AFYA NA MAZINGIRA

Ukurasa 20

Ukisikia 'kichanga' chako kinalia, sababu hizi hapa, unamkabili hivi

Ukurasa 16

Una shida ya ukoromaji? Tatizo hilo liko hivi

Ukurasa 14

Ruksa mbegu kiume toka kwa marehemu

DK. MWAISELAGE:

Ocean Road haina mshindani mashine kansa Kusini Sahara

Ukurasa 14

UKURASA 13

# Hofu Watanzania kuzuiwa Marekani

• **Yadaiwa** raia wake kunyimwa viza, serikali yasema ni habari za mtandaoni, ubalozi wasema 'ibaki ilivyo'... *Endelea ukurasa 2*



Mwonekana wa ujenzi wa barabara za mpishano (Ubungo Interchange) jijini Dar es Salaam katika makutano ya barabara za Morogoro, Mandela na Sam Nujoma, unaoendelea kujengwa kwa kasi kubwa, jana. Mradi huo unatarajiwa kuondoa adha ya msongamano mkubwa wa magari utakapokamilika. **PICHA: JACKSON MSANGULA**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play

Download on the App Store


## Serikali yaeleza ilivyojiandaa kukabiliana nzige wekundu waharibifu

UKURASA 2

## Mchungaji mbaroni tuhuma kumchoma mwanawe

UKURASA 3

**MICHEZO** NGASSA AFUNGIWA, MBELGIJI YANGA AONYWA UK.31

**MAONI, KATUNI** UK.6

## Babu amwangukia Rais kupata shamba

**Na Dege Masoli,** KOROGWE

MZEE Khatib Omar, mkazi wa wilaya ya Korogwe amemwandikia barua Rais John Magufuli kuomba msaada kwa kile alichokieleza kukoseshwa haki yake ya kukata rufani baada ya kutoridhishwa na uamuzi ya baraza la Ardhi la Wilaya.

Mzee Omar (92) katika barua yake hiyo, amemweleza Rais kuwa mwenyekiti wa baraza hilo alimnyima nakala ya hukumu aliyoitoa katika shauri lake baada ya kutoridhishwa na uamuzi wa kumkabidhi shamba mfanyabiashara aliyekuwa akimlalamikia kulipora.

"Mhe. Rais malalamiko yangu dhidi ya baraza hilo ni kwamba limeninyima nakala ya hukumu bila sababu za msingi baada ya kutoridhishwa na uamuzi lilioutoa kwa kumpa haki mfanyabiashara aliyevamia shamba langu ambalo nimeishi hapo tangu mwaka 1950 nikiwa nimelirithi kutoka kwa baba yangu mzee Omar Mhando," ilieleza sehemu ya barua hiyo.

Omar ambaye hivi sasa analazimika kusaidiwa kila jambo kutokana na umri wake, alisema kitendo alichofanyiwa na baraza hilo ni cha kinyama na anamuomba Rais aliwajibishe kwa kwenda kinyume cha mamlaka liliyopewa ya kusimamia haki bila upendeleo.

"Kwa kifupi Mheshimiwa Rais nikiwa kwenye eneo langu hilo kwa miaka yote hiyo, mwaka 2014 alijitokeza mvamizi wa shamba langu,

Belwizi Kwambaza na kudai shamba hilo na mali yake jambo lililosababisha kufikishana Baraza la Kata ambalo hatimaye nilipewa eneo langu baada ya mlalamikaji kushindwa kudhibitisha uhalali wa kumiliki. "Cha kusikitisha mwezi mmoja na nusu baada ya uamuzi wa Baraza la Kata kunipa haki yangu, mfanyabiashara huyo aliendа kufungua kesi Baraza la Ardhi la Wilaya ya Korogwe kwa madai yale yale ya kutaka baraza hilo limpe shamba langu" alisema Omar.

Alisema kilichotokea ni Baraza la Ardhi la Wilaya kuendesha shauri hilo kienyeji kwa maana ya kumpa shamba mfanyabiashara huyo bila kuzingatia uamuzi wa Baraza la Kata.

"Kibaya zaidi, hapakuwa na mjadala kwenye shauri hilo ikiwamo kuitwa mashahidi wa pande zote mbili na kwamba sikusikilizwa kabisa na baraza hilo," alisema.

Mbali na uamuzi huo, alisema kinachomfanya kuomba msaada kwa Rais kuingilia kati ni kile alichokieleza namna baraza hilo lilivyoendelea kumkandamiza ikiwamo kutumika vibaya kumnyima haki yake bila kujali umri na hali ngumu ya kimaisha aliyo nayo na mbaya zaidi ni kuzuia nakala ya hukumu ambayo aliiomba ndani ya siku kumi (10) baada ya uamuzi huo.

Mzee Omar katika malalamiko yake anasema baraza hilo lilitoa hukumu Novemba 25, 2014 na kumpa mfanyabiashara huyo shamba laki na yeye kuandika barua ya kuomba nakala hiyo Desemba 10, mwaka huu lakini katika hali isiyokuwa ya kawaida, alizungushwa kupata hadi ilipofika Machi 2, 2015 huku wakijua kuwa ni kinyume cha taratibu za ukataji rufani.

Alilalamika kuwa kigezo cha kuchelewa kukata rufani kimekuwa kikitumika kwa miaka yote hiyo licha ya kuwa si kosa lake na kumnyima haki ndiyo maana anaamini kuwa baraza hilo limetumika kumwonea kwa uzee na umaskini wake, hivyo kuchukua uamuzi wa kuomba msaada wa Rais aingilie kati ili haki itendeke.

# Hofu Watanzania kuzuiwa Marekani

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Marekani ikiwa katika maandalizi ya kuyapiga marufuku mataifa saba, ikiwamo Tanzania, raia wake kuingia nchini humo, serikali imesema haijapata waraka rasmi wa kidiplomasia kuhusu zuio hilo.

Taarifa iliyotolewa jana na vyombo vya habari vya Marekani vikimnukuu Msemaji wa Ikulu ya nchi hiyo, Hogan Gidley, iliyataja mataifa hayo kuwa ni Belarus, Eritrea, Kyrgyzstan, Myanmar, Nigeria, Sudan na Tanzania.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, baadhi ya nchi hizo zitazuiwa kupata visa na kwamba orodha ya nchi hizo bado haijatolewa rasmi.

Akizungumza na gazeti la The Guardian, kuhusu taarifa hiyo, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Emmanuel Buhohela, alisema wizara haiwezi kutolea tamko taarifa hizo kwa sababu hawajapata waraka rasmi wa kidiplomasia.

"Hatuwezi kutolea tamko taarifa hizo kwa sababu hatujapata waraka rasmi wa kidiplomasia kuhusiana na suala hilo. Hizo ni taarifa za mitandaoni," alisema Buhohela.

Nipashe iliwasiliana na Msemaji wa Ubalozi wa Marekani Tanzania, Ben Ellis, ambaye alisema: "Kwa sasa hatuna cha kusema wala kuongeza, ibaki ilivyo."

Rais wa Marekani, Donald Trump, akihojiwa na jarida la Wall Street juzi, alisema baadhi ya nchi ambazo raia wake watazuiwa kupata vibali vya kuingia nchini humo.

Mmoja wa maofisa wa juu katika Ikulu ya Marekani, alisema nchi ambazo zimeshindwa kudhibiti hali ya usalama ikiwamo kuzuia vitendo vya kigaidi, nazo zitaingizwa katika orodha hiyo.

Hata hivyo, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Marekani, na ile ya Usalama wa Taifa, hazikueleza chochote juu ya suala hilo.

Hadi sasa Marekani imeshawazuia raia wa Iran, Libya, Korea Kaskazini, Somalia, Syria, Yemen, na baadhi ya maofisa na ndugu zao kutoka kuingia nchini humo.

Chad nayo raia wake walizuiwa kuingia Marekani lakini iliondolewa kikwazo hicho Aprili, 2018.




Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Brigedia Jenerali John Mbungo, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu taasisi hiyo, kufanyia kazi ripoti ya ukaguzi wa vyama vya ushirika. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Serikali yaeleza ilivyojiandaa kukabiliana nzige waharibifu

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema imejiandaa kukabiliana na tishio la nzige wekundu, ambao wamekuwa wakishambulia mazao katika nchi jirani ya Kenya.

Hayo yamebainishwa na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, akisema kuwa serikali ina viuatilifu vya kutosha kwa ajili ya kudhibiti nzige hao.

Tamko hilo limekuja siku chache tangu nzige hao waharibifu kuvamia kaunti ya Turkana nchini Kenya na kufanya uharibifu wa hekari za mazao ya chakula, hivyo kusababisha hatari ya kutokea kwa njaa katika ukanda huo ambao unakabiliwa na ukame.

Waziri Hasunga alisema timu ya wataalamu kutoka wizarani kwake wako tayari kuhakikisha ndege hao wanakabiliwa ipasavyo ili kuwalinda wananchi na janga la ukosefu wa chakula na malisho ya mifugo.

Alisema ingawa kipaumbele kitakuwa kwa mikoa ya mipakani ambayo itakuwa katika hatari kubwa ya kuvamiwa na nzige hao, lakini uangalizi utakuwa ukifanyika katika mikoa yote.

"Ingawa Tanzania ni mwanachama wa jumuiya ya kimataifa ya kudhibiti nzige wekundu ambayo husaidia nchi inayokumbwa na ndege hawa, kama nchi tumejindaa vya kutosha kama hali hiyo itatokea," alisema.

"Nzige wekundu ni hatari sana kwa maendeleo ya nchi yetu kwa sababu wanaweza kusababisha njaa, kwa hiyo sisi tumeshachukua hatua kali kwa ajili ya kulinda wananchi," alisema.

Aliwataka wakulima na wafugaji nchini kote kutoa taarifa wakiona makundi ya nzige hao wakihama kutoka upande mmoja kwenda upande mwingine.

Alisema hifadhi ya dawa za kudhibiti ndege hao itasaidia kuwadhibiti wakati serikali ikisubiri mkakati mwingine wa kuwaangamiza ndege hao kwa kutumia ndege ndogo.

Kwa mujibu wa Waziri Hasunga, nchi mwanachama akivamiwa na ndege hao, jumuiya hiyo inaingilia kati na kupambana nao kwa kutumia ndege zake.

Jumanne, Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) lilionya kuwa idadi ya ndege hao inaweza kuongezeka mara 500 katika miezi mitano ijayo, kama jitihada za pamoja za kupambana na ndege hao hazitafanyika.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro, akizungumza na baadhi ya wananchi wa mkoa wa Shinyanga, baada ya kuwasili mkoani humo, jana, kwa ajili ya ziara ya kikao kazi chenye lengo la kukutana na Makamanda wa Polisi mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Geita, Kagera na Simiyu ili kuweka mikakati ya pamoja katika kushughulikia makosa ya mauaji yanayojitokeza nchini. **PICHA: JESHI LA POLISI**

# Mitishamba kutibu tezi dume, seli mundu

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imeagiza mtambo wa kisasa wa kutengeneza dawa za miti shamba za kutibu magonjwa mbalimbali yakiwamo seli mundu na kupunguza uvimbe wa saratani ya tezi dume.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) na Hospitali ya Taifa Muhimbili, Prof. Sayoki Mfinanga, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema hayo alipokuwa akielezea mafanikio ya miaka minne ya serikali katika kuboresha sekta ya afya katika mwendelezo wa kampeni ya 'Tumeboresha Sekta ya Afya' katika taasisi hiyo.

Kampeni hiyo yenye lengo la kuangazia mafanikio ya sekta ya afya nchini, imeandaliwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na taasisi zote zilizo chini yake.

Alisema katika mpango huo, serikali imetoa Sh. milioni 800 kwa ajili ya kununua mtambo huo kutoka China uliogharimu Sh. milioni 600.

Prof. Mfinanga alisema mtambo umeagizwa na Bohari Kuu ya Dawa (MSD) na Sh. milioni 200 kati ya Sh. milioni 800 zitatumiwa kusimika mtambo na kuhakikisha unaanza kutoa huduma.

Pia alisema Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (Costech), ilitoa Sh. milioni 400 kwa ajili ya kujenga maabara ya kuweka mtambo huo pindi utakapowasili.

Alisema dawa hizo zilizotengenezwa na kufanyiwa utafiti nchini na taasisi hiyo, zilionyesha kuwa zinasaidia kutibu na kuhusu ugonjwa wa saratani ya tezi dume zilionyesha kupunguza uvimbe lakini siyo kuponyesha moja kwa moja.

Kwa mujibu wa Prof. Mfinanga, asilimia kubwa ya dawa zinazotumika nchini zina asili ya miti shamba isipokuwa zinatengenezwa katika maabara ili kuondoa uasili kwa sababu hakuna miti ya kutosha kutengeneza dawa nyingi kwa asili.

Alisema dawa wanayotengeneza ni za asili kutoka kwenye miti iliyofanyiwa utafiti kwa ajili ya kutibu magonjwa yatakayolengwa.

Alisema tofauti ya dawa hizo na zile za waganga wa jadi ni kuwa zitakuwa zinaelezea kiwango cha dawa iliyomo kwenye ujazo na maelezo ya kimaabara na njia za matumizi kitaalam.

"Kikubwa naishukuru serikali kwa fedha ilizotoa kwa ajili ya kununulia mtambo huu wa kisasa wa kutengeneza dawa hizi," alisema Prof. Mfinanga.

Mkurugenzi Mkuu wa NIMR, Prof. Yunus Mgaya, alisema wataanza na dawa za kupunguza uvimbe wa saratani ya tenzi dume na kutibu seli mundu kwa sababu malighafi zake zinapatikana kwa urahisi na haraka.

Alisema pia watatengeneza dawa za magonjwa mengine sita ambazo upatikanaji wa malighafi ni wa muda kulinganisha na dawa watakazoanza nazo.

Pia alisema taasisi hiyo imeanza kufanya utafiti tatizo la upungufu wa nguvu za kiume ambao umehusisha mikoa ya Mbeya, Mwanza, Dar es Salaam na Dodoma.

Prof. Mgaya alisema wanaangalia nini sababu ya tatizo hilo na namna ya kudhibiti na kwamba pindi utakapokamilika watatoa taarifa kwa Wizara ya Afya ili kuandaa muongozo wa hatua za kuchukua kudhibiti tatizo hilo.

Kuhusu matumizi ya dawa za kuongeza makalio alisema bado hawajaanza kufanya tafiti huo na kama wataona kuna umuhimu wa kufanya hivyo watalazimika.

## Shahidi atetea wimbo 'kichanjio'

**Na Hellen Mwango**

MEYA wa Ubungo, Boniface Jacob, ambaye ni shahidi wa 10 katika kesi ya uchochezi inayowakabili vigogo wanane wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) ametetea neno 'kichinjio' kama linavyotumika kwenye mikutano ya chama chake.

Amedai mahakamani kuwa wimbo unaotumiwa katika mikutano ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na wakati kampeni, unawahamasisha wananchi kuwanyima kura wapinzani.

Kuhusu neno hilo, linamaanisha kadi za kupigia kura kwa kuhamasisha wananchi kuipa kura Chadema.

Kadhalika alidai kuwa wimbo huo uliotungwa na kuimbwa na Kapteni John Komba wa bendi ya TOT (sasa marehemu), pia unatumika katika mikutano ya CCM chini ya Rais John Magufuli.

Jacob alitoa madai hayo mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba, anayesikiliza kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Akiongozwa na Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala, Jacob alidai kuwa 'Kichinjio' kama ilivyoainishwa kwenye mashtaka ni kitambulisho cha kupigia kura ambacho hutumika kwenye uchaguzi mbalimbali.

Alinukuu kwamba: "Harambee mara tatu, wapinzani tuwalete, tuwachane chane tuwatupe, CCM tuwalete tuwakumbatie tuwabusu."

Alidai wimbo huo umetungwa na

INAENDELEA UK.8

# Mchungaji mbaroni tuhuma kumchoma moto mwanawe

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi mkoani Pwani linamshikilia Mchungaji wa Kanisa la Pentekoste lililopo Kongowe Wilaya ya Kibaha, Japhes Manwa (40), kwa tuhuma za kumchoma moto mwanawe.

Mchungaji huyo anadaiwa kumfanyia unyama mtoto huyo wa kiume mwenye umri wa miaka saba sehemu za mikononi na mgongoni.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema, tukio hilo liliripotiwa katika Kituo cha Polisi Kibaha juzi majira ya mchana.

Inadaiwa kuwa mtoto huyo mwenye ulemavu (mtindio wa ubongo) mkazi wa Vikuge Kata ya Soga, ni mwanafunzi wa darasa la kwanza katika Shule ya Msingi Kalabaka.

Kamanda Wankyo alisema, mtoto huyo, ambaye ni kati ya watoto wanne wa mtuhumiwa alikutwa na mkasa huo kwa madai kuwa baba yake hampendi.

Kufuatia tukio hilo, Jeshi la Polisi limetoa wito kwa wazazi na walezi wanaotoa adhabu kali kwa watoto kwa lengo la kuwakanya ambazo zinawasababishia majeraha na ulemavu.

Alisema, wazazi na walezi wanatakiwa kutoa adhabu kulingana na makosa na umri wa watoto.

## TAARIFA KWA UMMA



**KASSIM S. MALINGA**

Mtajwa hapo juu anatafutwa na mwajiri wake kwa tuhuma za kumuibia mali yenye thamani kubwa. Hupenda kutembelea mikoa ya **KAGERA, MWANZA, TABORA, DAR ES SALAAM** pamoja na nchini **UGANDA.**

Yeyote mwenye taarifa zitakazowezeshwa kukamatwa kwake tafadhali apige simu namba **0747 977 888** au atoe taarifa kwenye kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **KYE/IR/1001/2019**

# Tanesco yataja mafanikio miaka 4 ya JPM

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Umeme nchini (Tanesco), limetaja mafanikio mbalimbali yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano ikiwamo kuokoa Sh. bilioni 23.5 ambazo zilikuwa zikitumika kila mwaka kwa ajili ya kuendesha mitambo ya kufua umeme kwa kutumia mafuta.

Pia, Shirika hilo kwa kipindi hicho limeongeza ukusanyaji wa mapato kutoka Sh. trilioni 1.2 mwaka 2012/13 hadi kufikia Sh. trilioni 1.53 kwa 2018/19.

Hayo yalielezwa jana jijini hapa na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanesco, Dk. Tito Mwinuka, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi hicho chini ya Rais John Magufuli.

Alisema mitambo hiyo ilizimwa mwaka juzi katika vituo vya Tunduru,

INAENDELEA UK.8




Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Dk. Tito Mwinuka (kushoto), akizungumza na wanahabari (hawapo pichani), jijini Dodoma juu ya mpango mkakati wa maendeleo katika kuhakikisha huduma wanayoitoa inawanufaisha wananchi na Taifa. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Takukuru yaokoa bil. 4/- rushwa kwenye ushirika

**Na Enock Charles**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (Takukuru), imesema imefanikiwa kurejesha Sh. bilioni 4 kutoka kwa watuhumiwa wa rushwa na kuzirejesha kwa wakulima na vyama vya ushirika katika mikoa 28 nchini baada ya kufanya uchunguzi maalum kuhusiana na ubadhirifu wa fedha katika Vyama vya Ushirika na Saccos. Akizungumza na vyombo vya habari, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Brigedia Jenerali John Mbungo, alisema uchunguzi huo umefanywa kufuatia agizo lililotolewa na serikali kupitia kwa Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, kwa mamlaka hiyo baada ya uchunguzi mwingine kufanywa na Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) na kubaini mapungufu katika vyama hivyo.

"Mtakumbuka kwamba, takriban mwezi mmoja na nusu uliopita, Waziri wa Kilimo alinikabidhi muhtasari wa uchambuzi uliofanywa na Shirika la Usimamizi na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika, Takukuru mpaka sasa tumefanikiwa kuchunguza Sh. bilioni 51, na wakati uchunguzi wa Sh. bilioni 72 unaendelea," alisema Jenerali Mbungo.

Alisema kuwa vyama vilivyofanyiwa ukaguzi ni 4,413 ikiwamo Vyama Vikuu 38, Amcos 2,710, Saccos 1,448 na vyama vingine 217 na kugundua fedha ambayo ilikuwa na viashiria vya ubadhirifu na rushwa kiasi cha Sh. bilioni 124, na kwamba mpaka sasa taasisi hiyo imefanikiwa kukagua miradi 51 na kufanikiwa kuokoa kiasi cha Sh. bilioni 4 zilizokuwa na viashiria vya rushwa.

Katika ukaguzi uliofanywa na Coasco, hadi kufikia Juni 30, mwaka jana kabla ya ripoti hiyo kukabidhiwa kwa Takukuru, ulibaini kuwapo kwa vyama vya ushirika 11,410 vilivyosajiliwa na kati ya hivyo vyama hai ni 6,463 wakati vyama sinzia ni 2,844, huku vyama 2,103 vikiwa havijulikani vilipo.

Mikoa iliyokaguliwa na kiasi cha fedha kilichookolewa ni Ruvuma Sh. 9,968,000, Kilimanjaro Sh. 38,075,967, Manyara Sh. 9,856,800, Katavi Sh. 49,000,000, Pwani Sh. 291,400,000, Mbeya Sh. 50,701,900 , Iringa Sh. 133,801,317, Simiyu Sh. 57,178,000, Arusha Sh. 1,256,000, Lindi Sh. 1,042,362,754 na Njombe Sh. 1,021,472,480.

Mikoa mingine ni Mtwara Sh. 681,276,646, Songwe Sh. 354,374,673, Tabora Sh. 69,492,274, Tanga Sh. 10,842,480, Temeke Sh. 2,120,000 na Mara Sh. 242,982,800.

# RC awachongea watumishi Ardhi kwa Naibu Waziri

**Na Neema Hussein,** KATAVI

MKUU wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera, amewachongea watumishi wa Idara ya Ardhi mkoa huo kuwa wamekuwa na utovu wa nidhamu kwa viongozi mkoani humo kwa madai wao wapo chini ya wizara.

Mkuu huyo wa mkoa alitoa malalamiko hayo juzi mbele ya Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi mbalimbali.

"Watumishi wa idara hii wamekuwa wakishindwa kutekeleza majukumu yao na kuonyesha utovu wa nidhamu kwa baadhi ya viongozi wa mkoa wakidai wao ni watumishi wa wizara, hawako chini ya uongozi wa mkoa," Homera alilalamika.

INAENDELEA UK.8


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **SUMA JKT AUCTION MART, ANDAN GROUP COMPANY LTD** na **WUNGWANA AUCTION MART** kwa niaba ya AccessBank Tanzania Limited watauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba, Magari na Viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kuwa utakapopita muda wa siku kumi na nne tangu kutoka kwa gazeti hili, dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada. Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| S/N | TAWI HUSIKA | KAMPUNI INAYO HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | KIJITONYAMA | SUMA JKT AUCTION MART | ONE PLANET SCHOOLS LIMITED | MAHIGA/JULIUS,ELIZABETH | NYUMBA | IRINGA MANISPAA | 05/02/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 2 | KIJITONYAMA | SUMA JKT AUCTION MART | ONE PLANET SCHOOLS LIMITED | MAHIGA/JULIUS,ELIZABETH | SHAMBA | BAGAMOYO | 05/02/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 3 | KAHAMA | ANDAN GROUP COMPANY LIMITED | MSUYA/B,SAIDI | MSUYA/B,SAIDI | NYUMBA | KAHAMA | 05/02/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 4 | KAHAMA | ANDAN GROUP COMPANY LIMITED | BAYA/M,SULEIMAN | BAYA/M,SULEIMAN | NYUMBA NA SHAMBA | ITONGATALE | 06/02/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 5 | KAHAMA | ANDAN GROUP COMPANY LIMITED | REVILIAN/A,KAMSATILE | REVILIAN/A,KAMSATILE | NYUMBA | KAHAMA | 05/02/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 6 | KAHAMA | ANDAN GROUP COMPANY LIMITED | FARU/C,LEOCADIA | FARU/C,LEOCADIA | NYUMBA | KAHAMA | 05/02/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 7 | KAHAMA | ANDAN GROUP COMPANY LIMITED | MABULA/M,CHARLES | MABULA/M,CHARLES | NYUMBA | KAHAMA | 06/02/2020 SAA 4:00 ASUBUHI |
| 8 | TEMEKE | WAUNGWANA AUCTION MART | NYAKI/GASPAR,JERROME | NYAKI/GASPAR,JERROME | KIWANJA | BAGAMOYO | 08/02/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 9 | TEMEKE | WAUNGWANA AUCTION MART | RWELAMILA/SIMONI,AUDAX | RWELAMILA/SIMONI,AUDAX | NYUMBA | BUZA | 10/02/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 10 | TEMEKE | WAUNGWANA AUCTION MART | JONGO/OMARY,IBRAHIM | JONGO/OMARY,IBRAHIM | NYUMBA | MBONDOLE | 10/02/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 11 | KIJITONYAMA | WAUNGWANA AUCTION MART | MMBANDO/ELIMOKOZI,GLADSON | MMBANDO/ELIMOKOZI,GLADSON | NYUMBA | GOBA | 08/02/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |

MASHARTI YA MNADA

1. UKAGUZI UNARUHUSIWA MARA USOMAPO TANGAZO HILI.
2. MNUNUZI ATALAZIMIKA KULIPA MALIPO YA 25% YA FEDHA TASLIMU PAPO HAPO NA 75% BAADA YA SIKU 14 TOKA SIKU YA MNADA KUFANYIKA NA UKISHINDWA KULIPA MALIPO YALIYOBAKI MNADA UTARUDIWA NA FEDHA ULIZO LIPA HAZITARUDISHWA
3. GHARAMA ZA KUBADILISHA UMILIKI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE, KUMBUKA VIGEZO NA MASHARTI KUZINGATIWA.

**KWA MAWASILIANO**

**WAUNGWANA AUCTION MART 0713077474**
**SUMA JKT 0766609373**
**ANDAN 0684078494**

215595102

# Mpina achunguza kampuni ya samaki

**Na Mwandishi Wetu,** MAFIA



WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina (pichani), ameunda timu ya wataalamu kufanya uhakiki wa takwimu, mauzo, uzalishaji na uendeshaji wa Kampuni ya Alphakrust inayojishughulisha na uzalishaji wa samaki aina ya kambamiti pamoja na uhalali wa mapato ya serikali kufuati kuwapo udanganyifu kwenye biashara hiyo.

Kulingana na takwimu za mauzo ya kambamiti nje ya nchi, kampuni hiyo ilipaswa kulipa Sh. milioni 300 kama ushuru wa huduma kwa halmashauri hiyo, lakini imekuwa ikilipa shilingi milioni 100 kwa mwaka, hivyo kuipunja serikali kiasi cha shilingi milioni 200 kila mwaka.

Waziri Mpina amebaini njama hiyo inadaiwa kufanywa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia mkoani Pwani kwa kushirikiana na Mwekezaji wa Kampuni ya Alphakrust inayofuga samaki aina ya kambamiti kisiwani humo kwa lengo la kuiibia serikali mapato yake yanayotakiwa kutozwa kama ushuru wa huduma.

Alisema Halmashauri ya Mafia imetengeneza makadirio ya kutoza ushuru wa huduma ya Sh. milioni 9 kwa mwezi kutoka Kampuni ya Apha Krust na kuacha kanuni maalumu iliyowekwa kwa mujibu wa sheria ya ukokotoaji wa mapato yanayopatikana ya kutakiwa kulipa asilimia 3 ya mapato yote yanayopatikana kwenye biashara husika.

Madai ya udanganyifu huo yaliibuka wakati wa ziara ya Mpina ya kukagua kituo cha kutotoleshea vifaranga na shamba la ufugaji kambamiti lililomilikiwa kisiwani Mafia.

Waziri Mpina katika ziara hiyo aliambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Mafia ikiongozwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Shaib Nnunduma, wakurugenzi na wataalamu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mpina alihoji iweje halmashauri itoze ushuru kinyume cha sheria wakati kanuni za ukokotoaji wa mapato zinajulikana, hivyo kuamini kuwa huo ni mkakati wa siri uliosukwa baina ya Halmashauri ya Mafia na Kampuni ya Apha Krust kwa lengo la kukwepa kulipa mapato stahiki ya serikali.

"Haiwezekani Halmashauri ya Mafia ikaacha kufuata fomula ya uchukuaji wa 'service levy' uliowekwa na serikali na kutengeneza utaratibu wake yenyewe... mwisho wa siku watu wa nje tunachoweza kukielewa ni njama inayowekwa kati ya halmashauri na mwekezaji kuiibia serikali," alisema Mpina.

Waziri Mpina alisema kama halmashauri inatoza fedha nyingi zaidi za ushuru wa huduma tofauti na iliyowekwa kwenye sheria ni makosa kwani serikali haiwezi kukatoza fedha ambazo haziko kwenye utaratibu wa sheria.

Pia Mpina alielezea kusikitishwa kwake na kitendo cha mwekezaji huyo kushindwa kuwashirikisha wananchi wanaozunguka eneo hilo kujifunza teknolojia hiyo ili kukuza sekta ya ukuzaji viumbe maji hasa ufugaji wa kambamiti.

Alisema serikali haijapokea maombi yoyote ya upungufu wa wataalamu wenye utaalamu na uzoefu maalum kuendesha mradi kwani wataalamu hao wanazalishwa katika vyuo vya nchini kikiwamo Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na Vyuo vya Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA).

Meneja wa Alphakrust, Ganeshan Vedagiri, alilalamikia kukosa wataalamu wenye weledi na pindi watanzania wanapoajiriwa wanakaa muda mfupi na kuondoka, huku akilalamikia kudaiwa ushuru kwenye halmashauri zaidi ya moja

Alisema mradi huo una mabwawa 31 ya kambamiti ambapo kwa mwaka huzalisha wastani wa tani 400, huku asilimia 90 ya samaki hao wakiuzwa Ufaransa, kuwa asilimia 10 zinauzwa nchini.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mafia, Chuchu Silvery, licha ya kuwapo kwenye ziara hiyo hakuweza kuzungumzia chochote kuhusiana na dosari hizo.

# Wakurugenzi sasa wakabidhiwa mashine 7,200 kukusanya mapato

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amekabidhi mashine za kielektroniki za kukusanyia mapato 7,227, kwa wakurugenzi wa halmashauri nchini, huku akisema mashine za awali hazikuwa na ubora, hivyo kusababisha upotevu wa mapato mengi.

Jafo, alitoa kauli hiyo jana jijini hapa wakati alipokuwa akikabidhi mashine hizo kwa wakurugenzi hao kutoka halmashauri za majiji, manispaa na wilaya nchini.

Alisema mashine hizo ni za kisasa na mfumo wake si rahisi kuingiliwa na kusababisha mapato kupotea.

Waziri huyo alisema uchunguzi ambao umefanywa, ulibaini kuna baadhi ya mashine za awali zilikuwa zinazimwa zaidi ya mwezi mmoja, hali ambayo ilisababisha mapato kukusanywa nje ya mfumo.

Jafo alisema kutokana na hali hiyo, halmashauri nyingi zilipoteza mapato ambayo kwa kiasi kikubwa yalikusanywa nje ya mfumo wa kielektroniki na kuwanufaisha watu binafsi.

"Mashine za awali zilikuwa na tatizo la kimfumo, hali ambayo ilisababisha watu kuingilia na kuchezea na kuipotezea mapato ya serikali, mashine hizi tunazozigawa leo hii zimetengenezwa katika mfumo na ubora wa hali ya juu haziwezi kuingiliwa," alisema.

Jafo alisema upatikanaji wa mashine hizo za kisasa za PoS, hivi sasa halmashauri zitapata makusanyo mara mbili na hivyo kuondokana na utegemezi.

Alifafanua halmashauri nyingi

INAENDELEA UK. 8


**CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA VIWANDA, BIASHARA, TAASISI ZA FEDHA, HUDUMA NA USHAURI (TUICO)**

**TANGAZO LA RATIBA YA UCHAGUZI WA TUICO KWA MWAKA 2020**

A: Kwa mujibu wa Katiba ya Chama ya mwaka 1995, Rekebisho la Tano 2015 Sura ya Sita na Kumi na Nne ikisomwa pamoja na Kanuni za Katiba ya Chama, Kanuni ya 17, Taarifa inatolewa kwa Wanachama wote wa TUICO kuwa Ratiba ya Uchaguzi wa Chama (TUICO) kwa mwaka 2020 katika ngazi ya Matawi hadi Taifa iliyopitishwa na Baraza Kuu ni kama ifuatavyo:

**1. NGAZI YA MATAWI:**
Uchaguzi wa Viongozi wa Matawi na Kamati za Wanawake Matawini utafanyika Januari hadi Juni, 2020.

**2. NGAZI YA MKOA:**
Uchaguzi wa Viongozi ngazi ya Mikoa, Kamati za Wanawake na Wawakilishi wa Vijana Mikoa utafanyika kuanzia Julai hadi Agosti, 2020.

**3. NGAZI YA KANDA:**
Uchaguzi wa Viongozi ngazi ya Kanda utafanyika Septemba, 2020.

**4. NGAZI YA TAIFA:**
Uchaguzi wa Viongozi wa Kitaifa, Kamati ya Wanawake na Kamati ya Vijana Taifa utafanyika Desemba, 2020.

**B: FOMU ZA KUGOMBEA UONGOZI:**
Fomu za kugombea nafasi za uongozi Ngazi ya Tawi zitapatikana katika Ofisi za Matawi ya TUICO na Ofisi za TUICO Mikoa yote. Wakati wa kuchukua fomu ni lazima uoneshe nyaraka zifuatazo:-
(i) Kadi ya Uanachama
(ii) Nakala/kivuli cha "Salary Slip" au uthibitisho mwingine wa malipo ya ada ya Chama.

**C: NAFASI ZA UONGOZI ZINAZOGOMBEWA:**
Nafasi za Uongozi zinazogombewa ni kama zilivyoainishwa wazi katika Katiba ya Chama ya mwaka 1995, Rekebisho la Tano 2015, Kanuni za Katiba ya Chama na miongozo mbalimbali ilizotolewa na Chama.

**D: SIFA ZA WAGOMBEA:**
(a) Awe Mwanachama hai kwa mujibu wa Katiba ya Chama na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na.6 ya Mwaka 2004 ambaye analipa michango yake ya kila mwezi kwa wakati unaotakiwa.
(b) Awe anajua kusoma na kuandika kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza.
(c) Awe anazingatia Katiba na Kanuni za Chama na kuheshimu maamuzi yatokanayo na vikao.
(d) Awe na uelewa wa masuala ya Vyama vya Wafanyakazi na aweze kutetea Sera za Chama chake wakati wote.
(e) Awe anaunga mkono na kusaidia kwa vitendo maendeleo ya Chama.
(f) Awe mfano mzuri wa utendaji kazi na mwenye bidii ya kazi.
(g) Kwa Mgombea wa Uongozi wa nafasi ya Vijana, awe na umri kuanzia miaka 15 hadi 30.
(h) Awe jasiri na mvumilivu katika kusimamia na kutekeleza maamuzi ya Chama na kutetea haki na maslahi ya Wanachama.
(i) Awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai na kuhukumiwa.
(j) Awe hajawahi kufukuzwa uanachama au kuondolewa katika uongozi wa Chama.
(k) Awe makini katika kutoa maamuzi ya Chama.

**E: WITO KWA WANACHAMA:**
Wanachama wote hasa Wanawake mnahamasishwa kujitokeza kuchukua fomu za kugombea uongozi katika ngazi mbalimbali za Chama ili kukuza na kuimarisha demokrasia ndani ya Chama.

**F: MWISHO:**
Chama kinawatakia heri ya maandalizi na mafanikio mema katika Uchaguzi huu wa mwaka 2020.

**Mshikamano Daima,**

**B.Y. Nkakatisi**
**KATIBU MKUU TUICO**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tufanye juhudi zote kukomesha udumavu

**TATIZO** la watoto wachanga kukosa lishebora na kupata utapiamlo linachangia kurudisha nyuma njozi za jamii kuwa na familia bora, huku likiliongezea taifa mzigo wa watoto mbumbumbu, wagonjwa na nguvu kazi iliyodumaa akili, isiyofikiri kikamilifu na kutekelekeza majukumu yake ipasavyo.

Ili taifa lisonge mbele kimaendeleo halina budi kuimarisha lishe bora kwa wajawazito na watoto wachanga wanaozaliwa hasa kabla hawajafikia miaka mitano.

Kufanya hivyo ni kuepusha matatizo ya kuwa na watoto wenye udumavu na ulemavu wa akili ambao ni changamoto kubwa kwa Tanzania ya leo.

Takwimu za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii za mwaka 2014 zilionyesha kuwa wastani wa watoto wachanga 40,000 kwa wakati huo walikuwa wakipoteza maisha kila mwaka kabla ya kutimiza mwezi mmoja baada ya kuzaliwa.

Kama vile haitoshi kwa wakati huo ilikadiriwa kwamba watoto 100,000 walikuwa wanakufa kila mwaka kabla ya kufikisha umri wa miaka mitano. Kadhalika wengine 50,000 huzaliwa wakiwa wafu kutokana na sababu mbalimbali ambazo iwapo jitihada za makusudi zingechukuliwa mapema, zaidi ya asilimia 45 ya vifo hivyo visingezuiliwa.

Kuwalinda watoto ili wasife ni jukumu lisilokwepeka kwa taifa na wadau wengine wanaosaidia juhudi za kuleta maendeleo. Aidha, kuwalisha chakula bora kilichoongezwa virutubisho ni jitihada zinazotakiwa kufanywa na kuwa endelevu ili kuwasaidia wamudu maisha yao, kuchangia maendeleo ya taifa na dunia.

Mpango wa Chakula Dunia (WFP), Tanzania ni miongoni mwa wadau wanaohamasisha matumizi ya vyakula vyenye virutubisho kwa watoto na jamii yote na katika kufanikisha hilo ubunifu wa aina mbalimbali hutumiwa.

WFP ikishirikiana na wadau mbalimbali hufanyakazi na kaya maskini na za mikoa yenye ukame kama Dodoma na Singida kuwasaidia wananchi hasa wanawake na kuandaa chakula chenye lishebora zenye virutubisho kwa gharama nafuu na kuwalisha watoto wao ambao wanaathirika na ukosefu wa chakula bora.

Katika kitengo cha ubunifu cha WFP, shirika hilo linalofanyakazi zake chini ya Umoja wa Mataifa, ubunifu wa kuandaa vyakula vyenye virutubisho na vyenye viwango kwa ajili ya watoto wa chini ya miaka mitano na kuwapatia wananchi kwa gharama nafuu kunaelezwa kuwa ndiyo njia rahisi ya kuwasaidia watoto hao kukua na kufikia utimilifu.

NI wazi kwa serikali na kwa wadau wengine wa maendeleo kuwa na lishe bora na kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anapata lishe timilifu ni njia mojawapo ya kutekeleza malengo endelevu (SDG) lengo la 2 la kutokomeza njaa ifikapo mwaka 2030.


Tunaamini kuwa chakula bora na chenye virutubisho ni muhimu kwa kuwa idadi kubwa ya watoto kama hawatalishwa lishe bora na kuachwa kuwa wahanga wa utapiamlo taifa litakabiliwa na janga kubwa.

Tunaona kuwa ni lazima kuandaa na kutafuta ufumbuzi wa kumaliza tatizo hili la ukosefu wa lishebora na kutambua umuhimu wa chakula kwa watoto wadogo kwa kutumia ubunifu wa hali ya juu na kuwaeleza wananchi kuwa hiki ni kipaumbele.

Japo tangu mwanzo suala hili halijapewa kipaumbele cha kutosha kutokana na kutokuwapo mfumo bora wa kutoa huduma za chakula chenye virutubisho kikamilifu, lakini sasa ni lazima kuwa na msisitizo.

Ni vyema sasa wabunge, mawaziri wadau wa serikali za mitaa na washirika wengine kushirikiana na kuweka mkazo kwa wanaoandaa unga aina yoyote wapishi nyumbani, shuleni, vyuoni na kwenye biashara kila mmoja kuzingatia ubunifu na kuandaa vyakula bora vilivyoongezea virutubisho kwa ajili ya watoto na jamii yetu ili kuepuka udumavu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wadau wa elimu msiwe nyuma katika hili

**MOJA** ya matatizo yanayowakabili wanafunzi waliochaguliwa kuanza kidato cha kwanza mwaka huu, ni uhaba wa madarasa kwenye shule za sekondari nchini, hali inayosababisha baadhi yao kubanana chumba kimoja.

Kabla ya kuanza mwaka wa masomo, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, aliwaagiza wakuu wa mikoa nchini kuhakikisha wanasimamia ipasavyo ujenzi wa vyumba vya madarasa vikamilike kwa wakati.

Lengo, ni kuhakikisha wanafunzi wote waliochagulia kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu wa 2020 waanze masomo kwa pamoja, ili wasipishane na kujenga hali inayoweza kusababisha wasifanye vizuri kimasomo.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, watahiniwa 933,369 ambao ni sawa na asilimia 98.55 ya waliosajiliwa, walifanya mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi mwaka jana na kati yao watahiniwa 759,737 wamefaulu, ambao ni asilimia 81.50 ya wote.

Aliwaagiza, kuhakikisha ujenzi wa madarasa unakamilika, ili wanafunzi waliofaulu waanze masomo pamoja kwa vile kitendo cha kupishana kuanza masomo kinasababisha waliochelewa kutofanya vizuri katika mitihani yao.

Ingawa kuna maagizo hayo kwa wakuu wa mikoa, bado ipo haja kwa wadau wengine wa elimu kujiongeza na kushiriki kikamilifu kwenye mkakati huu wa kuongeza vyumba vya madarasa na siyo kuachia serikali tu.

Wasisubiri kuambiwa, bali waone kwamba wana wajibu wa kushiriki katika ujenzi huo iwe kwa kutoa rasilimali fedha au wenyewe wawe nguvukazi, ili kuharakisha ujenzi huo wa vyumba vya madarasa.

Kwa wale ambao wamejiongeza, tayari wanashirikiana na serikali katika jambo hilo muhimu la ujenzi wa vyumba vya madarasa, kwa ajili ya wanafunzi ambao wanategemewa kuwa viongozi wa baadaye.

Miongoni mwao ni wakazi wa vijiji vya Masinono, Bugwema, Kinyang'erere na Muhoji, katika Kata ya Bugwema mkoani Mara, ambao wameamua kugawana majukumu ya kujengwa vyumba vinne vya madarasa.

Wamechukua hatua hiyo kuunga mkono maagizo ya serikali ya kuwataka wakuu wa mikoa kusimamia ujenzi huo, na wao tayari wamekubaliana kujenga vyumba vinne ambavyo vinahitajika katika Sekondari ya Bugwema.

Katika kikao chao kilichofanyika wiki iliyopita, kwa ajili ya kujadili masuala ya elimu, Mkuu wa Shule, Ndaro Emmanuel, aliwaambia jumla ya wanafunzi 249 wamefaulu kwenda sekondari.

Lakini, kati yao 14 tu ndio walioripoti shule tangu ifunguliwe Januari mwaka huu na kwamba hao wote wanarundikana katika nyumba kimoja cha darasa, hali inayosababisha ufundishaji kuwa mgumu.

Kwa hesabu hiyo ya mkuu wa shule, bado kuna wanafunzi 135 ambao hawajaripoti shuleni, hivyo kuna haja na kuharakisha kukamilika ujenzi wa vyumba hivyo.

Kwa jinsi walivyo na uchungu na elimu ya watoto wao, jamii imekubaliana kukamilisha ujenzi huo Machi mwaka huu, ikiwa ni kuunga mkono uamuzi wa serikali kuharakisha ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Ushiriki wa wadau wa elimu wakiwamo wazazi kwenye maendeleo ya shule ni muhimu, hivyo wengine waige mfano huo kuhakikisha shule zote za umma zinakuwa na madarasa ya kutosha.

Wakazi wa Bugwema wameibuka na mkakati huo, wakati wenzao wa Kata ya Nyamrandirira mkoani humo, wamekubaliana kukamilisha vyumba vya madarasa vya sekondari inayojengwa, katika kijiji cha Seka.

Sekondari hiyo ina vyumba vinne vya madarasa, ambavyo wamepanga kuvikamilisha mwishoni mwa mwezi Machi mwaka huu, ili taratibu zifanyike na kupunguza mlundikano wa wanafunzi walipo Kasoma Sekondari.

Jumla ya wanafunzi 202 wamefaulu kwenda sekondari, katika Kata ya Nyamrandirira, na wote kwa sasa wanasoma Shule ya Sekondari Kasoma wakitumia vyumba vya maabara.

Hii ni kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney, na amejitolea kusaidia upatikanaji wa mawe na mchanga, huku mbunge, Profesa Sospeter Muhongo akitoa mifuko 100 ya saruji.

Mfano huo ukiigwa na wadau wote wa elimu nchini, tatizo la uhaba wa vyumba vya madaraka kwa shule za umma linaweza kubaki historia na hasa likiwa endelevu badala ya kusubiri matokeo ya darasa la saba.

Kwa hiyo wadau wa elimu wasiwe nyuma katika suala hili la ujenzi wa vyumba madarasa kutokana na ukweli kwamba kufanya hivyo ni sawa na kuchangia kudumaza elimu nchini.

## BARUA & MJADALA

# Turejee sura ya mgambo

**Mhariri,**

*KADRI maendeleo ya nchi yanavyofikiwa, yanaendana na changamoto zake. Tumeshuhudia katika maeneo mengi ambako kuna maendeleo ya makazi kukua kwa kasi kubwa, uhalifu nao unakua kwa kasi ya namna hiyo.*

*Sababu kubwa ni kwamba, ni suala linaloendana na maana kwamba, wasiokuwa na nidhamu katika jamii zao, wanatumia fursa hiyo kukodolea macho mali za wenzao kufanya wizi na uhalifu mwingine wa kudhulumu wenza mahali waliko.*

*Hiyo inageuka kero kwa wakazi wanaojitutumua kukabili uhalifu katika sura hiyo. Mojawapo, ni kuunda vikundi vya ulinzi wa kijamii miongoni mwao ambayo kwa sasa ni maarufu kama Sungusungu.*

*Huko nyuma, kuna askari wa akiba walioundwa kupitia mafunzo rasmi chini ya mamlaka za kijeshi nchini. Hao ni askari wa mgambo ambao kimafunzo hawajatoweka, ingawaje ni wachache sana kulinganisha na zama hizo.*


*Kila wilaya alikuwapo askari Mratibu Mgambo, ambaye ni askari wa Jeshi la Wananchi Tanzania, akiwanoa hao. Lakini wanasema, kila zama na azma yake.*

*Nadhani katika hali ilivyo, tunapaswa kukimbilia tulikotoka kutumia ujuzi wa mgambo na mazingira ya leo katika Sungusungu wetu kuangalia namna tunaweza kujipanga kupitia ulinzi huu wa jamii, kuhakikisha kwamba ulinzi unaimarika katika mazigira yetu, kwani ulinzi wetu unaotoka kwetu wenyewe na si vinginevyo.*

*Ni aina fulani ya maisha tunaweza kulirejesha Jeshi la Mgambo katika sura ya pili, wa kisungusungu iwe imeenea kila mahali na kutuletea tija kiutendaji.*

**Halfani Mejo,**
**Mwenapole, Kibaha,**

# Chakujifunza usajili wa laini kwa alama za vidole




**Na Sabato Kasika**

**JUMATATU** Januari 20 ilikuwa ni mwisho wa kusajili laini za simu kwa alama za vidole ulioanza mwanzoni mwa mwaka uliopita na kinachofuata ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kuzima laini ambazo hazijasajiliwa.

Awali, mwisho wa matumizi ya laini hizo ulikuwa ni Desemba 31 mwaka jana, lakini baadaye Rais John Magufuli, akaongeza siku 20, ambazo zilianzia Januari mosi na Jumatatu wiki hii.

Baada ya serikali kuongeza siku hizo, watu wengi walindelea kujitokeza maeneo mbalimbali kusajili laini zao, hadi siku ya mwisho walikuwa bado ni umati, hali inayoonyesha kuwa hata siku zilizoongezwa bado hazikutosha.

Lakini swali ni kwamba muda wote, ambao ulitangazwa na TCRA wa kusajili laini kwa mfumo huo na hata muda ulipooongezwa na walikuwa wapi, laini zao zikizimwa watamlaumu nani?

Siku ziliongezwa kwa kutambua kuwa inawezekana wapo baadhi ya watu walikuwa hawajazisajili laini zao, kutokana sababu mbalimbali ikiwamo kuugua na kukamilisha upatikanaji wa namba au vitambulisho vya taifa.

Kwa wale wenye matatizo hayo, walipaswa kutumia muda huo kuhakikisha wanapata vitu vyote vinavyohitajika kusajili laini, lakini inashangaza kuendelea kuwapo kwa wingi wa watu, ambao hawajasajili wakati muda unakwisha.

Lakini, pia kuna kitu cha kujifunza usajili huu wa laini za simu kutokana na mambo kadhaa yaliyojitokeza hadi kufikia baadhi ya watu kushindwa kusajili laini zao kwa muda wote ambao uliwekwa.

Kwanza kabisa Watanzania wamehimizwa sana kuhusu kusajili laini zao, Nida nao kwa upande wao walihimizwa kuharakisha utoaji wa vitambulisho au namba za vitambulisho ili watu waweze kusajili laini zao.

Cha kushangaza wapo baadhi ya watu wasio na vitambulisho, ambao hawakwenda Nida kwa wakati, vilevile hata mamlaka nayo ilikuwa ikitoa muda wa wiki tatu ndipo mtu apate kitambulisho.

Kwa mlolongo uliokuwapo wa kupata kitambulisho au namba, wale waliozoea kufanya mambo dakika za majeruhi, lazima watakwama tu na kuanza kulaumu serikali na kumbe wao ndiyo wamechangia hali hiyo.

Aidha, wapo watu wenye vitambulisho ambao walisubiri hadi siku ya mwisho ndipo wakasajili zao na mbaya zaidi ni kwamba siku za mwisho mitandao nayo iligoma na hivyo kusababisha usajili kukwama.

Ninaamini kwamba kwa mambo hayo yote kuna cha kujifunza, na asiwapo wa kulaumu mwingine, kila upande utafakari ni wapi ulikwama na kusababisha baadhi ya watu kutosajili laini zao kwa wakati.

Kimsingi kuna matatizo yaliyojitokeza ambayo yako juu ya uwezo wa Watanzania na mengine yako chini ya uwezo wao, ndiyo maana nikasema kila mmoja atafakari ni wapi alikwama.

Hivyo kama kuna mtu atakuwa hajasajili laini kwa uzembe kwa kusubiri hadi siku ya mwisho ndipo aende kusajili, au kwa sababu zilizo juu ya uwezo wake, basi wote watakuwa kapu moja.

Lakini, vilevile siyo vibaya kuwahurumia watu hao kwa vile tayari vitambulisho vyao viko kwenye mchakato, Nida iwatumie namba za vitambulisho vyao ili wasajili laini wawe na uhakika wa kutumia simu.

Pamoja na hayo, usajili wa laini za simu ulianza mwanzoni mwa mwaka jana na kisha muda ukaongezwa, hivyo wale, ambao watazimiwa, wajiulize walikwamishwa na nani?

Kabla ya siku ya mwisho iliyowekwa ili kufungia laini, baadhi ya wanasiasa walikaririwa na vyombo vya habari wakilaumu na kutaka serikali iongeze muda ili watu wengi wasajili.

Walichoomba ni sawa, lakini kwa nini waombe muda uongezwe bila kuhimiza wananchi wakasajili laini zao? Hapa walitaka kumaanisha kwamba hakuna uzembe wowote uliofanywa na wananchi.

Upo uzembe walioufanya na umekuwa kama wa kawaida kwa mambo mbalimbali kwani baadhi ya watu wamezoea kusubiri hadi siku ya mwisho ndipo wanaitikia maelekezo yaliyotolewa.

Kwa mfano hata kujiandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura, baadhi ya watu husubiri siku ya mwisho, na wapo wanaobahatika kujiandikisha na wengine kukwama kutokana na sababu mbalimbali.

Mtu anaweza kwenda kwenye kituo siku ya mwisho kwa ajili ya kujiandikisha na kukuta mashine ni mbovu na hivyo kukwama kama ilivyotokea kwenye usajili wa laini, ambapo baadhi ya mitandao ilikuwa haifanyi kazi.

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

**KABWELA** — Na Fadhili Mohammed



# Wakurugenzi wakabidhiwa mashine 7,200 kukusanya mapato

INATOKA UK. 5

hazijafanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato ya ndani hivyo mashine hizo zitapanua wigo zaidi.

"Sitaki kusikia tena halmashauri ina hizi mashine, lakini bado mkurugenzi wake analalamika kuwa hakuna tundu la choo cha shule hakikisheni kuwa mnakusanya mapato kwa wingi ili kujiondoa na utegemezi wa halmashauri zetu kwa serikali," alisema.

Awali Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tamisemi, Mhandisi Joseph Nyamhanga, alisema mashine hizo ni toleo la kwanza kutengenezwa na zina ubora kuliko za awali. Nyamhanga alisema kuwa mashine hizo 7,227 zimegharimu zaidi ya Sh. bilioni 2.32 na zimetengenezwa Ufaransa, na kuwa kwa mashine moja gharama yake halisi ni Sh. 900,000, lakini kutokana na serikali kununua nyingi ziliuzwa kwa Sh. 320,000.

"Kwanza niipongeze Norway kwa kusaidia kufadhili ununuzi wa mashine hizi, ambazo kwa kiasi kikubwa zitachangia katika ongezeko la mapato ya serikali ili kuendelea kuboresha huduma kwa wananchi," alisema Nyamhanga.

Aliongeza kuwa mashine hizo pia zitasaidia kupunguza udokozi wa fedha za umma ambazo zilikuwa zikidokolewa na watu wasiokuwa waadilifu.

"Mashine zile za awali mfumo wake unaweza kuchezewa hasa katika kubadili tarehe, lakini pia ulikuwa unaruhusu vitu vingi vifanyike lakini hizi za sasa ni kazi moja tuu ya kukusanya mapato hivyo zitakuwa salama zaidi katika kutunza mapato ya serikali," alisema Nyamhanga.



Mbunge wa Morogoro Mjini (CCM), AbdulAziz Abood (katikati), akizungumza na wananchi wa Kata ya Mafisa, baada ya kutembelea dampo kuu la takataka katika eneo la Viwandani, Manispaa ya Morogoro jana. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Shahidi atetea wimbo 'kichanjio'

INATOKA UK. 3

Kapteni Komba na kuimbwa na bendi ya TOT na kwamba chama hicho kinapofanya mikutano yake chini ya Mwenyekiti wake, Rais Magufuli na kwenye kampeni zao, huimbwa vizuri.

Wakili wa Serikali Mkuu, Faraja Nchimbi, alipinga swali kuhusu wimbo huo alilouliza Kibatala akihoji maana ya wimbo huo, lakini baadaye Hakimu aliruhusu kuulizwa, ndipo shahidi huyo akadai wimbo huo unamaanisha kuwanyima kura wapinzani.

Katika ushahidi wake, Jacob alidai Februari 16, 2018 majira ya saa 4:00 au 5:00 asubuhi, Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, Aron Kagurumjuli, alikula kiapo kuwa Wakala Mkuu wa Uchaguzi kwa Chadema na kwamba ndiye alikuwa mshereheshaji kwenye mkutano wa kufunga kampeni wa chama hicho uliofanyika viwanja vya Buibui Mwananyamala, Dar es Salaam.

Alidai wazungumzaji wakuu katika mkutano huo alikuwa Mwenyekiti wa Chadema Taifa, Freeman Mbowe, aliyezungumza kwa dakika 30 kuhamasisha watu kujitokeza kupiga kura pamoja na mgombea wa ubunge kwenye uchaguzi mdogo, Salum Mwalimu, ambaye alizungumza kwa dakika 20 akiomba kura na kueleza kwa nini ana nia ya kuongoza jimbo hilo.

Boniface alidai kuwa wabunge wengine waliopata nafasi ya kusalimia umma kwenye mkutano huo ni Halima Mdee (Kawe), Peter Msigwa (Iringa Mjini) ambaye alidai alihamasisha wananchi kufanya mabadiliko, John Heche (Tarime Vijijini) ambaye alihamasisha vijana kuwa na mwamko wa kupiga kura siku ya uchaguzi.

Alidai baada ya mkutano huo kwisha, viongozi hao waliondoka na magari yao wakisindikizwa na maofisa wa polisi ambao walikuwa wanalinda mkutano huo ili ufanyike kwa amani.

Pia alidai baada ya mkutano huo wananchi waliipongeza kamati ya maadili kwa hotuba zilizotolewa na viongozi hao na kwamba hakukuwa na malalamiko yoyote.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika, Heche, Msigwa, Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko, Mbunge wa Kawe, Halima Mdee, Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya na aliyekuwa Katibu Mkuu Dk. Vincent Mashinji.

Washtakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka 13, ikiwamo kula njama, kufanya mkusanyiko wenye ghasia, kuhamasisha hisia za chuki, kushawishi hali ya kutoridhika, uchochezi na kush-

# Tanesco yataja mafanikio miaka 4 ya JPM

INATOKA UK. 4

Mtwara, Namtumbo, Songea, Madaba, Ruvuma,na Liwale ambavyo vilikuwa vikitumia mafuta.

"Tunashukuru sasa hivi tumefanikiwa kuokoa kiasi hicho cha fedha tangu mwaka 2018 na tunaamini tutazidi kupiga hatua kwa hii miradi tunayoifanya," alisema Mwinuka.

Mkurugenzi huyo alisema mafanikio hayo yamepatikana kupitia ufuaji wa umeme, ununuzi, usafirisha pamoja na eneo la uwekezaji.

"Mafanikio kuacha kufua umeme kwa kutumia mafuta,yametokana na uwekezaji ambao tumeufanya na kuboresha sekta hii," alisema.

Dk. Mwinuka alisema pia wamefanikiwa kutatua tatizo la umeme jijini Dar es Salaam kwa kuboresha kituo cha Ubungo cha kupooza umeme kutokana na kuzidiwa na wateja.

Kadhalika, alisema watumiaji wa umeme wameongezeka ambapo kwa mwaka 2015 kulikuwa na mita zilizofungwa ni 1,648,386 na hadi kufikia mwaka 2019 mita zilizofungwa ni 2,700,682.

"Kuna ongezeko la mita milioni 1.05 ni sawa na asilimia 63.4," alisema.

Kuhusu uzalishaji wa umeme, alisema shirika limezalisha kilovati 132 na kwamba ni hatua kubwa ya kuboresha huduma za umeme hapa nchini.

Alitaja mafanikio mengine ni kushuka kwa gharama za umeme mwaka 2016 ambapo serikali ilishusha gharama za umeme.

Alisema kwa upande wa vijijini kufikia mwaka jana vijiji 8,236 nchini vimefungiwa umeme kati ya vijiji 12,268 vyote nchini sawa na asilimia 67.

# RC awachongea watumishi Ardhi kwa Naibu Waziri

INATOKA UK. 4

Alisema watumishi hao wamekuwa wakaidi wa kufuata utaratibu wa kazi unavyoelekeza ikiwamo kuondoka kazini bila kutoa taarifa kwa kiongozi yeyote.

"Kwa kweli nina changamoto kubwa, lazima nikueleze ukweli Naibu Waziri, mimi ndiye kiongozi wa Mkoa huu... wale viongozi wa eneo la Nsimbo kwa mfano licha ya kumuita anaweza akaondoka hapa bila kutoa taarifa kwa Mkurugenzi, akidai yeye ni mtumishi wa wizara," aliongeza Homera.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Naibu Waziri Mabula alisema kama mkurugenzi ameshindwa kuwasimamia, Mkuu wa Mkoa ana wajibu wa kuwachukulia hatua.

Alisema hakuna sehemu iliyoandikwa kuwa mtumishi anatoka kazini bila kuomba ruhusa kwa madai ni mtumishi wa wizara.

"Kwa utovu huu wa nidhamu, Wizara tunahitaji kupata barua ili tuwashughulikie," alisema Mabula.

Mabula alisema katika Wizara hiyo ipo changamoto ya watumishi ikilinganishwa na mahitaji.

Alisema watumishi wanaohitajika ni 2,500, lakini waliopo hivi sasa ni 1,500.

HABARI KITAIFA

# Ecobank yawanoa wahitimu vyuo vikuu

**Na Beatrice Philemon**

BENKI ya Ecobank Tanzania, imezindua mafunzo kwa wahitimu wa vyuo vya elimu ya juu inayojulikana kama 'Graduate Trainee Program' ili kupata mameneja wa benki wajao na kuwa mahili katika usimamizi wa fedha katika taasisi za kifedha hapa nchini.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Mkurugenzi Mkuu wa benki hiyo, Mwanahiba Mzee, alisema programu hiyo itawawezesha wahitimu kutapata mafunzo maalumu ya kazi ambayo yatawasaidia kufanya kazi zao za kibenki kwa ufanisi zaidi.

Alisema benki hiyo imeamua kuanzisha programu hiyo kama sehemu ya uwajibikaji kwa jamii (CSR) na pia kusaidia sekta ya elimu hapa nchini.

"Kwa kuanza tumeanza na wanafunzi 10 kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu Mzumbe, Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) na Chuo Kikuu cha Wenzhou ambao watajifunza mafunzo ya kazi mbalimbali katika benki yetu, ili kuwa na wakuu wa vitengo na mameneja wajao katika benki yetu ikiwamo taasisi zingine za fedha," alisema Mzee.

Naye Mkurugenzi wa Shahada za Awali, Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) , Dk. Shaban Ngole, aliipongeza benki hiyo kwa kuanzisha programu ambayo ni muhimu sana kwa wahitimu wa vyuo vya elimu ya juu.

Alisema kila mwaka benki hiyo imekuwa ikichukua wanafunzi wasiozidi 15 kutoka Chuo cha IFM kuja kufanya mafunzo katika idara mbalimbali za benki na kwamba mpaka sasa kupitia programu hizo zaidi ya wanafunzi 100 wameshanufaika.

"Tunaomba benki zingine ikiwamo taasisi nyingine za kifedha ziendelee kupokea wanafunzi zaidi hasa kwenye eneo la mafunzo kwa vitendo ili wanafunzi wapate ujuzi zaidi na kuwa mahili katika kozi ambazo wamesoma darasani," alisema Ngole.

Naye Mratibu, Shahada za Juu UDSM, Dk. Diana Mwiru, alisema kuwa wamefurahia kuanzishwa kwa programu hiyo kwa sababu wanafunzi watapata uzoefu wa kutosha kulingana na masomo waliosoma chuoni na pia kuingia kwenye soko la ajira.

"Ukiwa na mhitimu ambaye anasoma masomo kwa nadharia tu hana vitendo, hawezi kufanya vizuri kwenye kazi zake za ajira," alisema Mwiru.

Alisema kwa muda mrefu benki hiyo imekuwa ikichukua wanafunzi kutoka UDSM kuja kufanya mafunzo na mpaka sasa zaidi ya wahitimu 1,500 kutoka chuo hicho wameshanufaika na programu hizo, huku wengine wakipata ajira.

# Wapewa siku saba kukarabati kiwanda

**Na Stevie chindiye,**
NAMTUMBO

OFISA Afya Wilaya ya Namtumbo, Elias Patrick, ametoa siku saba kwa wamiliki wa kiwanda cha kuchakata mahindi na kutengeneza unga cha Baraka Sembe wilayani humo kuhakikisha wanakifanyia marekebisho.

Alitoa agizo hiyo baada ya kubaini kuwapo kwa baadhi ya upungufu katika kiwanda hicho ambao unahatarisha afya za wafanyakazi na wananchi wanaoishi jirani na kiwanda hicho.

Patrick alizitaja baadhi ya kasoro hizo ni pamoja na uwapo wa mazingira machafu, pamoja na kuwapo kwa harufu mbaya, wafanyakazi kutokuwa na vifaa ya kufanyia kazi kama vile vifaa vya kuzuia vumbi pamoja na stoo ya kuhifadhia nafaka kutokuwa na madirisha ya kupitishia hewa.

Kasoro zingine ni kiwanda hicho kuwa na watumishi wasiopima afya zao, watumishi kukosa mikataba ya kazi, maeneo ya kiwanda kuwa na sakafu iliyoharibika na uhifadhi wa nafaka usio na mpangilio katika stoo pamoja na kutokuwa na vifaa vya kuzimia moto.

Naye ofisa mazingira wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, Kelvin Mnali, alisema kwa namna mazingira ya kiwanda hicho yalivyo, mmliki wake anapaswa kutozwa faini kubwa na hata kufungiwa kiwanda.

Alimwambia mmiliki wa kiwanda hicho kuwa kwa kadiri ya mazingira yalivyo katika kiwanda hicho anastahili kutozwa faini.

Hata hivyo, mmliki wa kiwanda hicho alipewa maelekezo ya kurekebisha kasoro hizo kwa muda wa siku saba kwa sababu ni mara yao ya kwanza.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wafanyakazi katika kiwanda hicho walisema mikataba ya kazi pamoja na mazingira mabovu yaliyoandaliwa na uongozi wa kiwanda siyo ya kuridhisha na ni hatarishi kwa afya zao.

Musa Hyera mkazi wa Mji Mdogo wa Namtumbo anayekaa jirani na kiwanda hicho alisema kuwa harufu kali inayotoka katika kiwanda hicho inawakosesha hewa safi.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, akibadilishana mawazo na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo, alipotembelea Makao Makuu wa Jeshi hilo, jijini Dodoma juzi. Wengine ni Meneja Mwandamizi wa Uhusiano, Qeen Kunyamagoha, Meneja wa Kanda ya Dodoma, Chabu Mishwaro, Mkurugenzi wa Biashara za Serikali, Dk. Beneth Bankobeza na Meneja Wateja Kitengo Maalum, Crispin Sichwale. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wachache wajitokeza kujiandikisha Pemba

**Na Mwandishi Wetu,**
PEMBA

WAKATI Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), ikiendelea na uandikishaji wa wananchi katika daftari la kudumu la wapigakura, msukumo wa wananchi kujitokeza kujiandikisha bado ni mdogo.

Kazi ya uandikishaji katika daftari hilo iliyoanza Januari 18, mwaka huu inawahusu wananchi ambao hawajawahi kuandikishwa na wale wanaohakiki taarifa zao.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wananchi wa Micheweni walisema kuwa wanaishukuru ZEC kwa kusimamia kazi hiyo kwa amani na utulivu.

Khalid Hamad Ali mkazi wa mjini Wingwi alisema kuwa tokea kazi ya uandikishwaji ianze hadi jana inaendelea vizuri bila ya wasiwasi wowote ule. Alisema kwa wananchi wengi wa wilaya hiyo ni wavuvi na wakulima hivyo kutokana na shughuli zao ni vigumu wote kufika vituoni kwa mara moja.

Hata hivyo, alieleza kuwa anaamini kabla ya kufika tamati kwa kazi hiyo wananchi wote watakuwa wameshahakikiwa katika daftari hilo.

"Naamini kuwa wananchi wote watakuja kujiandisha na sisi tutakuwa mabalozi kwao kwa kuwashawishi ili waje wajiandikishe," alisema Hamad.

Naye Mpanvu Makame Khatib mkazi wa Chamboni Micheweni aliwataka wananchi wenzake wafike vituoni mwao ili waweze kujiandisha kwani hakuna vurugu.

Khatibu aliipongeza ZEC Kwa kusimamia vizuri zoezi hilo kwa salama na amani na kuongeza kuwa tume hiyo inafanya kazi zake vizuri.

"Nashukuru sana kuona hadi sasa amani na utulivu upo na ninaomba wananchi wote ambao aana wasiwasi na usalama wao watoe na wafike vituoni mwao kwa ajili ya kujiandisha," alisema Khatibu.

Ofisa uandishaji wa Wilaya ya Micheweni, Khamis Abdalla Hassan, alisema kuwa kazi ya uandikishaji na uhakiki kwa wapiga kura katika daftari la kudumu la wapiga kura linaendelea vizuri na hakuna dalili ya uvunjifu wa amani katika vituo vyote.

Alisema kulikuwa na changamoto kwa baadhi ya wananchi kuhusu majina yao ila ZEC ilifanya juhudi ya kurekebisha tatizo hilo na wananchi hao kupatiwa haki yao ya kujiandikisha.

# Uchafu machinjioni sasa tishio kwa afya

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

WANANCHI wanaoishi pembezoni mwa eneo la machinjio wilayani Tunduru mkoani Ruvuma wapo katika hatari ya kuungua magonjwa ya kuambukizwa endapo kutatokea homa za mlipuko. Malalamiko hayo yamebainishwa na baadhi ya wananchi hao katika eneo hilo, na kwamba endapo serikali haitachukua hatua za makusudi kuwasaidia na janga hilo, viongozi wajiandae kujibu hoja zitakazoibuka baada ya kutokea vifo.

Mohamed Abdala, Hashim Issa, Issa Mohamedi na Yasini Abdalah, walibainisha hayo wakati wakizungumza na Nipashe na kuongeza kuwa kutokana na uchafu wa mazingira ya eneo hilo, kuna wakati wadudu wanaofanana na funza husambaa na kuingia katika nyumba zao.

Walisema pamoja na hali hiyo, pia eneo hilo hutoa harufu kali wakati wote, hali ambayo imekuwa ikiwanyima raha ya kuishi katika makazi yao na kuwa tishio hasa kwa watoto wadogo ambao huenda kucheza katika maeneo hayo bila kujali hali ya uchafu huo. Wameiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuyahamisha machinjio hayo katika eneo hilo ambalo linazidi kuwa hatarishi kwa wananchi.

Walisema wakati machinjio hiyo inajengwa miaka ya 1970 idadi ya ng'ombe waliokuwa wanachinjwa walikuwa kati ya 1 hadi 3, lakini kutokana na ongezeko la watu hivi sasa wafanyabiashara wanachinja hadi zaidi ya ng'ombe 20, hali ambayo imeongeza mabaki ya uchafu katika eneo hilo la kuleta adha kwa wakazi wake.

Akizungumzia hali hiyo kwa niaba ya vibarua walioajiriwa na halmashauri kufanya usafi katika eneo hilo, Bakary Hashim, pamoja na kukiri kukithiri kwa uchafu ndani na nje ya machinjio hiyo, alisema chanzo ni mwajiri wao kutowalipa stahiki zao kwa zaidi ya mwaka mmoja na nusu sasa. Alisema hata usafi ambao wamekuwa wakiufanya ndani ni hutokana na posho au nyama kidogo ambayo hutolewa na wachinjaji kama motisha kwa kazi hiyo. Alisema kutokana na hali hiyo, wamekuwa wakifanya usafi wa ndani ya machinjio pekee na kwenda kufanya vibarua vingine ili kumudu kuhudumia familia zao. "Kutolipwa kwa stahiki zetu kwa muda mrefu kumekuwa ni kikwazo cha sisi kuendelea na shughuli za kusafisha maeneo yote ya machinjo," alisistiza Hashimu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Gasper Balyomi, amekiri kuwapo kwa hali hiyo na kwamba ofisi yake ipo katika harakati za kufanya ukarabati ambao utahusisha usafi wa eneo lote la machinjio hayo.

"Tumekwisha tenga kiasi cha

# Wanaume wa mabadiliko wawataka wanawake wengi kugombea 2020

**Na Mwandishi Wetu**

WANAUME wa mabadiliko Zanzibar, wamewataka wanawake kutoka kila chama kugombea nafasi za uongozi katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu na siyo kudhani nafasi hizo ni kwa ajili ya wanawake kutoka chama tawala (CCM) pekee.

Hassan Jani Masoud, mmoja wa wajumbe 20 waliomo katika timu ya wanaume wa mabadiliko Unguja na Pemba, Hassan kutoka Wilaya ya Kaskazini 'A', Unguja anasema ana imani kubwa kuwa wanajamii waliokuwa wakihudhuria mikutano ya uhamasishaji katika shehia mbalimbali watawaunga mkono wanawake watakapojitokeza katika michakato ya kisiasa ili waingie katika ngazi za maamuzi.

Hassan alisema changamoto anayoiona ni ile hali ya wanawake wengi kuona kuwa uhamasishaji huo ni kwa ajili ya wanawake kutoka chama tawala tu.

Alisema CCM imeweza kupata wanawake wengi kwenye safu za uongozi tangu uchaguzi wa vyama vingi kuanzia kupata nafasi moja hadi tatu kwenye Baraza la Wawakilishi, hatua ambayo ina uhafadhari ukilinganisha na vyama vingine. "Nafikiri katika mazingira ya siasa za upinzani ambapo wanawake kutoka katika chama tawala wanafanikiwa kupata viti, ingawa tungependa wapate viti vingi zaidi majimboni... wanawake kutoka vyama vingine vya siasa nao wanapaswa kujitokeza kwa wingi kugombea na kushinda," alisema Hassan.

Alisema ni muhimu kwa wanawake wa vyama vyote kusimama imara kugombea na kwamba kutokana na uwezo wao wa kujitolea kwa jamii na jinsi watakavyoweza kueleza mipango yao wataweza kushinda bila ya kujali mipaka ya chama.

Ili kuhakikisha hilo linatokea, alivishauri vyama kuweka mikakati thabiti ikiwamo kuwahamasisha wanawake ndani ya vyama vyao kugombea na kuwaunga mkono katika kila hali.

Zimba Khatib Bonde, kutoka Wilaya ya Kusini Unguja ambaye yumo katika timu ya wanaume wa mabadiliko iliyoundwa na Tamwa Zanzibar ili kuifikia jamii kuihamasisha kuhusu kumuunga mkono mwanamke kushiriki katika siasa na uongozi, alisema kuwa bado wapo wasiokubaliana na mawazo hayo na ambao wanaona kuwa kazi ya mwanamke ni kupika na kulea watoto tu.

Alizitaja changamoto nyingine kuwa ni mtazamo hasi dhidi ya wanawake kushika nafasi ya uongozi, fikra potofu zilizoelekezwa katika dini na uwezo mdogo wa kiuchumi walionao wanawake. Kadhalika alisema kwamba wapo wanaume ambao ni kikwazo kwa wanawake kugombea kwa sababu bado wamebeba fikra kwamba wanawake hawapaswi kugombea nafasi za kisiasa.

Wanaume hao wa mabadiliko, kumi kutoka Unguja na kumi kutoka Pemba, mwaka jana walitoa elimu katika wadi 54, Unguja 29 na Pemba 25 na kuwafikia watu wapatao 3,250 wa kada mbalimbali na kusababisha kupata wanaume wengine 26 zaidi walioitaka kujiunga na timu hiyo akiwamo Mkuu wa Mkoa mmoja na Mkuu wa Wilaya.




Mkurugenzi wa bidhaa za kijamii wa T-MARC, Flavian Ngole (kulia), akikabidhi msaada wa diapers mpya za Smiley zilizozinduliwa katika soko nchini hivi karibuni, kwa mzazi, Rebecca Nelson, katika wodi ya wazazi ya Hospitali ya Mwananyamala wakati wa hafla ya taasisi hiyo kukabidhi msaada hospitalini hapo jana. Katikati ni Balozi wa bidhaa za kijamii wa taasisi hiyo, Dinah Marrios. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafugaji mikoa ya Pwani kuongeza uzalishaji maziwa

**Na Gwamaka Alipipi**

WAFUGAJI wa ng'ombe wa maziwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga na Morogoro, wataweza kuongeza uzalishaji wa maziwa baada ya kuanzishwa kwa shindano la tuzo kwa taasisi zinazojihusisha na uuzaji na usambazaji wa pembejeo.

Akizungumza na waandishi wa habari, kiongozi wa mradi wa AgResults unaosimamia tuzo hizo, Neema Mrema, alisema wafugaji wengi wa ng'ombe wa maziwa wanakabiliwa na uzalishaji duni wa maziwa kutokana na changamoto ya upatikanaji wa pembejeo bora na huduma za ugani. "Mradi huu utasaidia kupambana na changamoto hizo kwa njia ya shindano na kutoa tuzo kwa washiriki kwa kipindi cha miaka minne... motisha itatolewa kwa sekta binafsi watakaotoa vifurushi vya pembejeo na huduma za ushauri kwa wakulima," alisema Mrema.

Alisema hatua hiyo itaongeza uzalishaji wa maziwa na kukidhi mahitaji ya soko la Tanzania. Pembejeo hizo ni uzalishaji kwa chupa, kudhibiti vimelea, chanjo na lishe bora ya mifugo.

Alisema kushiriki shindano hilo ni bure, lakini taasisi au shirika lazima liwe limesajiliwa na ina vibali stahiki kwa biashara ya pembejeo za ng'ombe wa maziwa itolewayo na Tanzania.

"Biashara hiyo iwe inaendelea au kuna matarajio kwa siku za karibuni kufanyika katika mikoa tajwa, mahitaji muhimu ni kwamba washindani lazima kuuza pembejeo moja kwa moja kwa wakulima," alisema Mrema.

Aliongeza kuwa shindano hilo litaanza Juni mwaka huu na mwisho ni Aprili mwakani na kwamba waombaji wanapaswa pia kuwa na uwezo wa kujumuisha aina mbili au zaidi ya pembejeo kwa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa. Alisema tuzo zitatolewa kulingana na mauzo, baada ya mauzo ya pembejeo kuthibitishwa kuwa yamekidhi vigenzo vinavyotakiwa. Alisema zawadi zinatofautiana kulingana na aina ya pembejeo na vifurushi vilivyoundwa ili kuongeza tija kwa wafugaji wadogo wa ng'ombe.

Mrema alisema pembejeo aina ya uzalishaji kwa chupa uzalishaji wake lazima ufikie kiwango cha asilimia 75 ya mimba na mshindi atapewa Dola za Marekani 15. Alisema pembejeo aina ya vidhibiti vimelea lazima ziuzwe katikakipindi cha mwaka mmoja na mshindi atapewa Dola za Marekani 6. Alisema pembejeo aina ya chanjo lazima zitolewe kwa ng'ombe wawili, kutupa mimba, mapele ya ngozi, homa ya bonde la ufa, na mshindi atapewa Dola za Marekani 5.

Aliongeza kuwa pembejeo za lishe lazima ziuzwe asilimia 30 ya uhitaji wa lishe kwa ng'ombe anayenyonyesha mwenye uzito wa kilo 400 na mshindi atapewa Dola za Marekani 27.

# Lowassa kuongoza harambee ya ujenzi kituo watoto yatima

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZIRI Mkuu mstaafu, Edward Lowassa, anatarajiwa kuwaongoza Waislamu mkoani Arusha katika harambee ya ujenzi wa kituo cha kulelea watoto yatima itakayofanyika Februari 22, mwaka huu, katika Kijiji cha Karangai wilayani Arumeru.

Mjumbe wa Kamati Kuu wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (Bakwata), ambaye ni Imamu wa Msikiti wa Patandi, Ally Labia, alisema harambee hiyo itafanyika siku hiyo ambayo ni Sikukuu ya Maulidi, kumbukumbu ya kuzaliwa kwa Mtume Muhammad.

Labia alisema harambee hiyo inafanyika ikiwa kuenzi aliyoyafanya Mtume Muhammad ambaye alisema aliishi vizuri na yatima baada ya kupoteza wazazi wake na alikuwa akiwapenda na kuwajali yatima.

"Ni muhimu kwa Waislamu na wasiokuwa Waislamu kuwaangalia, kuwajali, kuwatambua na kuwapenda yatima," alisema.

Katibu Mkuu wa Taasisi ya Waislamu (Twariqatul), Abdi Omary Said, alisema taasisi hiyo ilisajiliwa mwaka 2010 kwa ajili ya kuwaunganisha Waislamu na tangu kuanzishwa kwake ina matawi 5,662 ndani na nje ya nchi.

Hata hivyo, alisema taasisi hiyo, imejenga vituo vya kulelea watoto yatima 851.

Msemaji wa taasisi hiyo, Sheikh Haruna Hussein, alithibitisha kwamba Lowassa atakuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo na ataweka jiwe la msingi wa ujenzi wa kituo hicho.

"Mapokezi ya Lowassa yataanzia eneo la Nambala akiambatana na Wakuu wa Wilaya za Arumeru, Arusha na viongozi wa dini na wafanyabiashara wakubwa," alisema Hussein.

Aidha, alisema eneo la ujenzi wa kituo hicho, lina ukubwa wa ekari moja na litagharimu Sh. milioni 150, na litakuwa na uwezo wa kuchukuwa watoto yatima 50 hadi 60.

Licha ya kuzungumza hayo, aliwataka Watanzania kudumisha uhuru, amani na mshikamano kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

"Amani tuliyopewa na Mwenyezi Mungu ni tunu kwetu, tusikubali Watanzania wanasiasa wakaivuruga amani yetu. Kama kuna mtu anaona hakutendewa haki basi afuate taratibu zinazotakiwa," alisema.



Wataalamu wa Shirika lisilo la kiserikali la Oikos East Africa, wakitoa mafunzo kwa jamii ya wafugaji wa Kimasai jinsi ya kuchakata na kusindika ngozi kwa njia za asili, katika Wilaya ya Longido, mkoani Arusha, jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Watahadharishwa mvua zinazoendelea kunyesha

**Na Allan Isack,** KITETO

WAKAZI wa Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara, wametakiwa kuchukua tahadhari wakati huu mvua zinapoendelea kunyesha baada ya mkazi wa kijiji cha Dosidosi, Hamisi Ramadhani, kufariki dunia kwa kusombwa na maji.

Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, Tumaini Magessa, akizungumza juzi kwenye mazishi ya mkazi huyo, alisema jamii inapaswa kuchukua tahadhari mapema.

Alisema jamii inapaswa kuwa makini wakati huu mvua zinapoendelea kunyesha na kwamba watu wawe makini na mafuriko yanayopita katika makazi.

Pia aliwataka wananchi kuondokana na dhana kuwa mvua kidogo zinazonyesha hazina madhara. Alisema mvua zingine zinanyesha maeneo ya milimani na kusababisha mafuriko katika maeneo yenye mabonde.

"Kulikuwa na mvua zinanyesha maeneo ya milimani na kuleta madhara kwa mfano eneo la Kibaya maji nusura yasombe daraja la barabara inayokwenda Arusha," alisema.

Mmoja wa ndugu wa marehemu, Rajab Hamis, alimshukuru mkuu huyo wa wilaya kwa kufika kwenye mazishi hayo na kutoa pole.

"Tunakushukuru Mkuu wa Wilaya kwa kufika hapa Dosidosi kutupa pole na rambirambi kwenye msiba huu ambao umemkumba ndugu yetu," alisema.

Alisema watazingatia maelekezo yaliyotolewa na mkuu wa wilaya na watayafanyia kazi ili kuepuka madhara yatokanayo na mvua zinazoendelea kunyesha.

Ramadhan alifariki dunia Januari 19, mwaka huu, kwa kusombwa na maji wakati akienda nyumbani kwake na alizikwa Jumatatu iliyopita.

# Waonya migogoro ya ndoa kikwazo malezi ya watoto

**Na Allan Isack,** BABATI

MSHAURI wa malezi na makuzi na maendeleo ya awali ya watoto kutoka Shirika la Children in Crossfire la Ireland ya Kaskazini, Davis Gisuka, amewatahadharisha wanandoa wenye migogoro kuacha vitendo hivyo kwa kuwa migogoro inasababisha madhara kwa watoto wadogo.

Tahadhari hiyo aliitoa wakati akizungumza na Nipashe, akielezea migogoro ya wanandoa inavyoathiri malezi na ukuaji wa watoto.

Kutokana na kukithiri kwa vitendo hivyo katika jamii, alitoa wito kwa jamii kuhakikisha migogoro ya familia inatatuliwa bila kuleta madhara kwa watu wengine.

Naye Wakili wa Kujitegemea, Nickson Maganya, alisema Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 Sura ya 29, imezungumzia namna ya kuwasaidia watoto endapo itatokea wazazi wao wameachana.

Mwanasheria huyo alisema pindi migogoro hiyo inapotokea kwa wanandoa, madhara yanawakuta watoto kwa kukosa malezi ya baba na mama kitu ambacho ni muhimu kuliko vyote kwa wakati huo.

"Mtoto anaweza kukosa elimu kutokana na mgogoro ambao umesababisha familia kusambaratika. Watoto mara nyingi wanajikuta wakiishi katika mazingira magumu na wakati mwingine wanapelekwa kulelewa na watu ambao hahitaji kuishi nao," alisema Muganya.

Aidha, alisema sheria inaeleza kuwa wanandoa wanapotengana, mahakama inapaswa kuzingatia maslahi ya watoto ikiwa wana umri chini ya miaka saba.

"Nashauri wanandoa wavumiliane na kuacha tabia zitakazosababisha migogoro kwenye familia zao kwa kuwa kuachana na kunatokana na mambo yao binafsi na hiyo si njia ya kutatua tatizo," aliongeza.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Babati, Mathias Focus, alisema kila robo ya mwaka wa fedha, ofisi yake imekuwa ikipokea migogoro ya ndoa kati ya 20 na 50.

Focus alisema migogoro mingi ya ndoa inatokea kipindi cha njaa kwa kuwa wanaume wengi wanatelekeza familia zao kutokana na ugumu wa maisha.

## Wakili ashangaa wenye dhamana ukatili kwa watoto

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

WAKILI maarufu katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini, Elizabeth Minde, amesema bado anashangaa kwa nini baadhi ya watu waliopewa dhamana ya kupambana na ukatili dhidi ya watoto, ndio wanakuwa chanzo cha kuharibu kesi hizo mahakamani na katika upelelezi.

Minde alisema wanaotajwa zaidi kuharibu kesi za ukatili kwa namna moja au nyingine ni baadhi ya maofisa wa serikali hasa katika madawati ya Polisi yanayosimamia kesi hizo na wanaopewa kazi ya kupeleleza mashauri ya aina hiyo. Alisema kutokana na udhaifu huo, wanaharakati wa haki za binadamu mkoani Kilimanjaro, wameanzisha mchakato wa kuzishawishi mamlaka zinazohusika na udhibiti wa masuala ya ukatili wa kijinsia, kuridhia kurudiwa kwa uchunguzi wa kitabibu dhidi ya tuhuma za kubakwa mara kadhaa mwanafunzi mmoja wa darasa la sita katika Wilaya ya Hai.

Minde ambaye ni Mkurugenzi wa Shirika la Kutetea Masuala ya Wanawake na Watoto (Kwieco), alisema tayari wameanza mazungumzo na baadhi ya mamlaka hizo ikiwamo Ustawi wa Jamii na Polisi.

"Tunataka uchunguzi dhidi ya mwanafunzi huyo wa darasa la sita anayeishi huko Masama Mbweera urudiwe ili haki ya mtoto ipatikane.

"Tunazo taarifa kwamba wako watu wanafanya ujanja ujanja kupindisha ushahidi na tunaomba pia mamlaka nyingine zifuatilie sakata hilo kujua mwenendo wake," alisema Minde.

Mwishoni mwa mwaka jana, kuliibuliwa tuhuma za ubakaji dhidi ya mwanafunzi huyo kuhusishwa kimapenzi na mzee wa miaka 80, mkazi wa Kijiji cha Masama Mbweera.

# Wajisalimisha Polisi kwa tuhuma za kuhujumu reli

**Na Godfrey Mushi,** HAI

HATIMAYE wafanyabiashara wakubwa wawili wanaotoa huduma ya usafirishaji wa abiria kati ya mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Dar es Salaam, wamejisalimisha Kituo Kikuu cha Polisi Bomang'ombe, Wilaya ya Hai kutokana na tuhuma za kufadhili genge la uhalifu linalodaiwa kuhujumu miundombinu ya reli ya Arusha-Moshi.

Wafanyabiashara hao waliripoti jana zikiwa zimepita saa 24 tangu Mkuu wa Wilaya hiyo, Lengai Ole Sabaya, kutoa amri wajisalimishe au kukamatwa iwapo watashindwa kutii amri hiyo.

Alipotafutwa kutoa ufafanuzi iwapo wafanyabiashara hao wameitikia wito wake, Ole Sabaya alisema: "Ni kweli wameripoti jana na tayari wameanza kuhojiwa." Zaidi alieleza:"Mpaka sasa hivi (jana) tunavyozungumza wanasikilizwa na polisi huku wanaendelea kufanya kazi yao ya mahojiano kujua ukweli wa jambo hili ili kulifikisha mwisho. Kwa hiyo ni hatua ya kwanza na hatua nyingine baada ya mahojiano zitafuata."

Ole Sabaya alisema hatua kali za kisheria zitaendelea kuchukuliwa dhidi ya watu watakaoendelea kuhujumu miundombinu ya reli. Januari 19 mwaka huu, Ole Sabaya aliagiza wamiliki wawili wa mabasi kukamatwa kwa tuhuma za kuunda genge la uhalifu kwa lengo la kuhujumu miundombinu ya reli ili kuathiri usafiri wa treni ya abiria kati ya Dar es Salaam, Moshi hadi Arusha.

Aliagiza Mkuu wa Polisi wa Wilaya hiyo (OCD), Lwelwe Mpina, kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama kuwakamata wafanyabiashara hao, iwapo watakaidi amri ya kujisalimisha kabla ya saa 12:00 jioni ya Januari 19. Alinukuliwa na Nipashe akisema: "OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya) kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama mliopo hapa, kama hawa wafanyabiashara (anawataja majina) hawatajisalimisha wenyewe hadi kufikia saa 10 jioni ya leo (jana), kawakamateni na kufikia saa 12:00 jioni mniletee taarifa za kwamba mmeshawakamata na wako mahabusu.

"Nimepokea taarifa kwamba hawa wafanyabiashara wa mabasi, wameunda genge la uhalifu na linahujumu miundombinu ya reli hii," alieleza Ole Sabaya.

Kwa mujibu wa Ole Sabaya, baadhi ya wahalifu wanaokwenda kuhujumu miundombinu hiyo wanaweka mawe makubwa katika njia ya reli na wengine wanachimbua chini ya reli hiyo.

Kabla ya kutoa amri hiyo, Ole Sabaya alipokea taarifa fupi kuhusu maendeleo ya ukarabati wa reli hiyo kutoka kwa msimamizi wa ubadilishaji wa njia ya reli, Sindu Singozi, alimweleza Mkuu huyo wa Wilaya kwamba kazi hiyo inaendelea vizuri licha ya kuwapo changamoto za hapa na pale.

Kwa upande wao baadhi ya wafanyakazi wanaokarabati reli hiyo, walimweleza Ole Sabaya kuwa miundombinu ya reli hiyo ilihujumiwa katika eneo la Rundugai na Kia, Wilaya ya Hai.




Ofisa Elimu wa Elimu Maalum wa Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, Rashid Rajab, akieleza jambo kwa walimu wakuu wa shule za msingi (hawapo pichani), katika mafunzo yaliyoandaliwa na Shirika la Connects Autism kuhusu kujenga uelewa wa pamoja dhidi ya elimu jumuishi. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Wafugaji Kanda ya Kaskazini sasa kunufaishwa ngozi ghafi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAFUGAJI wa mikoa ya Kanda ya Kaskazini ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanga, wataanza kunufaika na soko la uhakika la ngozi ghafi katika siku za usoni, baada ya ujenzi wa kiwanda cha kisasa cha bidhaa hiyo kuanza rasmi karibu na Gereza Kuu la Karanga, Moshi.

Jana, Meneja wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Neema Kuweite, alitangaza neema hiyo kwa wafugaji wakati alipotembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi huo.

Ujenzi wa kiwanda hicho utagharimu zaidi ya Sh. bilioni 75.3 na unatarajia kukamilika mwezi Februari miaka huu.

Kwa mujibu wa Kuweite, ujio wa kiwanda hicho utafungua fursa za ajira kwa watu zaidi ya 4,000.

"Kiwanda hiki cha kutengeneza bidhaa za ngozi kilichopo katika Manispaa ya Moshi, ndicho kiwanda pekee katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tunatarajia kitakapokamilika wafugaji hasa kutoka kanda ya kaskazini na mikoa mingine nchini, watapata soko la uhakika la ngozi ghafi," alisema meneja huyo.

Alisema tatizo kubwa linalojitokeza na kusababisha ujenzi wa kiwanda hicho kusuasua ni mabadiliko ya tabianchi, ongezeko la gharama ya mradi unaosababishwa na mfumuko wa bei ikilinganishwa na bajeti iliyokuwa imepangwa awali.

Kabla ya Kuweite kuzuru eneo hilo na kujionea mradi unavyoendelea, kamati ya ulinzi na usalama ya Wilaya ya Moshi ikiongozwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Kippi Warioba, nayo ilitembelea ujenzi huo na kuagiza wasimamizi wa mradi huo kuwa makini na vifaa vya ujenzi vinavyoagizwa ili kudhibiti hujuma ikiwamo wizi.

Awali akizungumza katika eneo la mradi huo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Magereza, Hamisi Nkubaf, alisema usalama wa vifaa hivyo ni wa uhakika na kwamba idadi ya mafundi waliopo ni wengi na kusababisha vifaa vinavyoingia kushambuliwa huku wengine wakikosa kazi na hivyo kulazimika kusubiriana.

Kulingana na takwimu za Wizara ya Mifugo, ngozi ghafi inayotokana na mazao ya mifugo, zaidi ya vipande milioni nane huwa vinapotea, kati ya vipande milioni 10 vinavyozalishwa nchini.


Lakini ngozi ambazo zinaingia katika mfumo rasmi wa biashara na serikali inapata kodi katika hivyo vipande hivyo milioni 10 vinavyozalishwa ni vipande milioni 1.5.

ama
ALHAMISI JANUARI 23, 2020
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 20

**Ukisikia 'kichanga' chako kinalia, sababu hizi hapa, unamkabili hivi**



Ukurasa 16

Una shida ya ukoromaji? Tatizo hilo liko hivi



Ukurasa 14

**Ruksa mbegu kiume toka kwa marehemu**



## DK. MWAISELAGE:

# Ocean Road haina mshindani mashine kansa Kusini Sahara

Ukurasa 14



Shughuli ikiendelea maabara kumuumba mtoto. **PICHA: MTANDAO.**

## Ruksa mbegu kiume toka kwa marehemu

**LONDON,** Uingereza

WATAFITI wamefanyia kazi haki ya kugaiwa mbegu ya kiume kutoka kwa mtu aliyekufa, ili zipandikizwe kwa mama mhitaji.

Uchambuzi wa kisayansi unaowasilishwa kupitia Jarida la Afya, unaonyesha uhalali wa kiafya, kutumika mbegu hizo za kiume kutoka kwa aliyekwishatangulia mbele ya haki

Nchini hapa, matumizi ya mbegu hizo yamekuwa za kawaida sana hata mwaka 2017 walizaliwa jumla ya watoto 2,345 wanaotokana na mfumo huo wa uzalishaji, mbegu zikipandikizwa kwa kinamama.

Kuna malalamiko mengi ya kuwapo upungufu wa mchango huo, kutokana na taratibu zake kuwa na masharti kadhaa.

Mbegu hiyo inaelezwa huchukuliwa katika mfumo maalum kupitia msukumo wa nguvu za umeme na kuna ushahidi unaodai, zinapochukuliwa ndani ya saa 48 tangu kifo, inawezekana kuchangia mke kupata ujauzito

Wataalamu Dk. Nathan Hodson, kutoka Chuo Kikuu cha Leicester na mwenzake, Dk. Joshua Parker, kutoka hospitali ya Wythenshawe ya Chuo Kikuu cha Manchester, Uingereza wanasema ni mfumo usio na shaka ua unafaa kiafya.

Kwa mujibu wa sheria za Kiingereza, watoto waliozaliwa kutokana na nguvu za kiume za kupandikizwa, wanaweza kuunganishwa kisheria na 'baba' zao watakapofikia umri miaka 18. **BBC**

AFYA

### DK. MWAISELAGE:

# Ocean Road haina mshindani mashine kansa Kusini Sahara

• Afrika Mashariki wamiminika • Maboresho makubwa mbioni



Majengo ya Taasisi ya Saratani Ocean Road, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Mary Geofrey**

UNAPOITAJA leo inaitwa Taasisi ya Kansa Ocean Road, ambayo imeanzishwa kisheria mwaka 1996, lengo ni kuhudumia tiba na kinga ya maradhi ya saratani.

Mengine inayohudumia ni kuendesha kliniki za wagonjwa wa nje na wodini, uchunguzi wa radiolojia na nyuklia, maabara, tiba za kemia na mionzi, tiba shufaa, kulaza wagonjwa.

Aidha, Ocean Road ambayo iko katikati ya jiji la Dar es Salaam na ukingoni mwa Bahari ya Hindi, pia ni mahali panakofanyika kwa wanazuoni wa vyuo vikuu vya tiba, ikiwamo Muhimbili, ambako ina uwezo wa kuwalaza jumla ya wagonjwa wasiopungua 256.

> **Wagonjwa wanaotoka hospitali za rufani wanawahi matibabu na kupona, tofauti na wale wanaokuja moja kwa moja.**

Ikirejelea mzizi wa Ocean Road, historia inaenda mbali mwaka 1895 wakati huo nchi ilikuwa koloni la Ujerumani na baada ya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, Wakoloni wa Kiingereza waliibadili maslahi kuwa hospitali yao maalum.

Ilipotimu kupatikana uhuru wa Tanganyika mwaka 1961, ilibadilishwa kuwa hospitali ya kawaida na kitengo cha wazazi cha Hospitali ya Muhimbili. Hiyo ndio chimbuko la watoto wengi waliozaliwa Dar es Salaam.

Baada ya kutumika muda mrefu, sambamba na tiba za kawaida, mwaka 1980 Ocean Road ilifanyiwa maboresho mapya kuwa kitengo cha tiba ya kansa.

Hadi sasa Taasisi ya Saratani Ocean Road, inafanya kazi chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

### HALI YA AFYA

Kwa mujibu wa Sera ya Afya kitaifa, tiba ya saratani inatolewa bure kwa watu wasio na uwezo.

Katika kipindi cha miaka minne iliyopita, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Kansa Ocean Road, Dk. Julius Mwaiselage, anasema kumekuwapo ongezeko la wagonjwa wa saratani wanaofika huko kufanyiwa uchunguzi.

Je sababu za kuongezeka ni zipi? Dk. Mwailesage anasema kwamba taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Afya katika ziara ya kampeni iitwayo 'Tumeboresha Sekta ya Afya' inalenga kutangaza mafanikio yaliyopatikana ndani ya miaka hiyo.

Dk. Mwaiselage anasema katika kipindi hicho, kumekuwapo ongezeko la wanaougua saratani na kufika katika taasisi hiyo, sababu kuu ni mwamko wa jamii kuhusu vyanzo na athari za saratani kwa jamii na uchumi kwa ujumla.

Anasema katika kipindi hicho, wagonjwa waliopata huduma za uchunguzi na tiba, waliongezeka kutoka 40,885 kwa mwaka 2015/16 hadi 64,747 mwaka 2018/19, ikiwa sawa na ongezeko la wagonjwa zaidi ya 20,000 kwa kipindi hicho.

Dk. Mwaiselage anataja sababu za ongezeko, ni kuwapo msukumo unaoungana na mwamko kupitia serikali kuboresha mfumo wa mawasiliano nchini kote, iliyoendana na kuboreshwa vituo vya afya na hospitali ngazi ya chini, kumesaidia wananchi kuamka kwenda kupata huduma za afya.

Anasema, wananchi wanapoenda kupima afya katika vituo vya afya, wana warufaa ya kwenda Ocean Road kwa uchunguzi zaidi, kabla ya tatizo kuwa kubwa.

"Kuwapo vituo vya afya katika maeneo mbalimbali nchini kumesaidia sana jamii kuwa na mwamko wa kupima afya na ndio sababu wagonjwa wa Saratani wameongeza kutoka katika hospitali za chini," anasema na anaongeza:

"Wagonjwa wanaotoka hospitali za rufani wanawahi matibabu na kupona, tofauti na wale wanaokuja moja kwa moja, wanakuwa wapo katika hali mbaya zaidi."

Anataja sababu ya kuongezeka wagonjwa wa kansa duniani, ni kasi kubwa ya kuongezeka visababishi vyake katika maeneo mengi duniani.

Kwa mujibu wa Dk. Mwaiselage, kumekuwapo ongezeko la wagonjwa wa marudio kutokana na kuimarishwa kwa tiba ya saratani na wagonjwa wanaotibiwa na wakapona, kisha wakaendelea na maisha ya kila siku.

"Kumekuwapo mafanikio mengi na makubwa katika miaka minne ya utendaji wa Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais John Magufuli katika taasisi hii muhimu ya saratani," anasema Dk. Mwaiselage.

AFYA

# Ocean Road haina mshindani mashine kansa Kusini Sahara



Waziri mwenye dhamana na afya, Ummy Mwalimu, akikagua mashine mpya ya matibabu hospitalini Ocean Road.

**MAFANIKIO YALIVYO**

Anataja mafanikio makubwa wanayojivunia kama taasisi ni ujenzi wa vyumba maalum wa mashine za mionzi, kununua na kusimika mashine mbili mpya za kisasa za tiba mionzi aina ya 'Linac' na 'CT Simulator.'

Anasema, serikali ilisimika mashine mpya na za kisasa kutibu saratani na kabla ya ununuzi huo, walijenga jengo lenye thamani ya Sh. bilioni 2.3.

Dk. Mwaiselage anasema, ununuzi na usimikaji wa mashine hizo uligharimu Sh. bilioni 9.5 na gharama za awali ya mradi huo, ilikuwa Sh. bilioni 14, lakini taasisi ilinunua kiwandani moja kwa moja, hivyo kupata unafuu wa kuokoa Sh. bilioni 4.5.

Anasema mashine hizo za kisasa, zinatumia teknolojia iitwayo '3D' inayopatikana katika hospitali kubwa za saratani duniani, katika nchi kama India, Ulaya na Marekani.

Mkurugenzi hiyo anaitaja kuwa mashine za kwanza kusimikwa katika ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara na anafafanua:.

"Mashine hizi zilianza kutoa huduma za uchunguzi wa tiba Septemba mwaka 2019 na jumla ya wagonjwa 1,430 walikuwa wamepata kipimo cha 'CT Scan' hivyo kupunguza usumbufu kwa wagonjwa ambao walitakiwa kwenda hospitali nyingine kupata huduma hii."

Anasema hadi sasa, serikali imeimarisha upatikanaji dawa za kutibu saratani katika taasisi, kutoka wastani wa asilimia nne waka 2014/15 hadi wastani wa upatikanaji dawa asilimia 95 mwaka wa fedha uliopita.

Katika mafanikio hayo ya ndani ya miaka minne iliyopita dawa zinapatikana kwa kiwango cha asilimia 100, huku wagonjwa wenye saratani zinazoongoza katika taasisi hizi ni za; mlango wa kizazi, matiti, kiposi sarcoma, tezi dume, njia ya chakula kooni, damu matezi, ngozi na kibofu cha mkojo.

**VIFAA TIBA**

Dk. Mwaiselage anasema, serikali iligharamia ununuzi wa vyanzo vipya vya mionzi kutoka Ujerumani, kupitia Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kwa gharama ya Sh. milioni 473.

Anasema huduma hiyo imeboresha utoaji wa tiba ya mionzi ya ndani kwa kutibu wagonjwa 70 kwa siku kutoka wagonjwa 30 kwa siku mwaka 2015.

"Mashine za mionzi ya ndani hutumika kutibu zaidi wagonjwa wa Saratani ya mlango wa kizazi na wamefanikiwa kufunga 'AC' na kununua vitanda maalum vya kutoa tiba kemia," anasema:

"Hivyo, kuongeza utoaji Tiba ya Kemia kutoka wagonjwa 40 kwa mara moja hadi wagonjwa 100," na Dk. Mwaiselage anasema, taasisi ilinunua mashine za kutoa tiba kemia 60 kupitia Shirika la Dawa (MSD) kwa wagonjwa, zinazosaidia kutoa tiba hiyo kwa ufanisi zaidi kwa mara moja.

> "Kwa wastani, gharama ya kumtibu mgonjwa mmoja wa saratani nje ya nchi ni kati ya Sh. milioni 50 hadi 75, ikihusisha vipimo, tiba na kulazwa wodini.


Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani Ocean Road, Dk. Julius Mwaiselage. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**RUFANI NJE**

Dk.Mwaiselage anasema kwa wastani, gharama ya kumtibu mgonjwa mmoja wa saratani nje ya nchi ni kati ya Sh. milioni 50 hadi 75, ikihusisha vipimo, tiba na kulazwa wodini.

Anasema, katika mwaka wa fedha 2015/16, kuna wagonjwa 164 wa saratani waliopatiwa rufani za kwenda nje ya nchi, lakini baada ya kuboreshwa huduma za saratani mwaka 2017/18, wagonjwa 25 tu ndio waliopatiwa rufani na mwaka 2018/19, walikuwa 14, wengi walienda India.

Mkurugenzi anasema kutokana na kuimarika huduma zinazotolewa, kuna wagonjwa wanaotoka nchi jirani za Kenya, Comoro, Malawi, Msumbiji, Zimbabwe, Congo, Jamhuri ya Kidemokrasia Congo (DRC) na Burundi ,wameongezeka nchini kupata huduma za matibabu ya saratani na hulipia gharama zote.

**MABORESHO**

Ili kuimarisha huduma za uchunguzi wa saratani, serikali imeshatoa Sh. bilioni 14.5 kwa ajili ya jengo maalum, kununua na kusimimisha mashine mpya za kisasa aina ya 'Cyclotron na PET/ CT Scan.'

Dk.Mwaiselage anasema mradi huo utahusisha ujenzi wa jengo, ununuzi na usimikaji wa kiwanda cha Cyclotron na Mashine za PET/ CT Scan.

Anasema mchakato wa kununua mashine unaendelea kutekelezwa, kwa matarajio mradi huo utakamilika Juni mwaka huu, kuwezesha kuanza kupatikana kipimo hicho nchini.

Kwa mujibu wa mkurugenzi, ni hatua itakayopunguza gharama za kupeleka wagonjwa nje ya nchi, ikitarajiwa serikali itaokoa Sh. bilioni tano kila mwaka.

**MALENGO YAKE**

Mkurugenzi huyo anasema, Taasisi ya Ocean Road iliyoko kwenye mchakato wa kukopa fedha Sh. bilioni 3.84 kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), ili kuendelea kuimarisha huduma za saratani na kuongeza juhudi za serikali kumarisha tiba ya saratani kitaifa.

Dk.Mwaiselage anasema, taasisi yake imejipanga kuendana na kasi ya ongezeko la wagonjwa kutoka ndani na nje ya nchi na kwamba mradi utakapokamilika, utakuwa wa manufaa makubwa kitaifa.

Anaorodhesha maboresho hayo ni kuongeza wodi za wagonjwa binafsi, ili kuimarisha utoaji huduma kwa wagonjwa wenye uwezo wa kulipa, kutoka vitanda 23 hadi kufika100.

Dk.Mwaiselage anasema, pia wanalenga kuwa na wodi binafsi zenye viwango vya kimataifa, ili kuvutia wagonjwa kutoka nje ya nchi na kuimarisha uchunguzi wa magonjwa ya saratani.

Anaeleza kuwa litafanyika kwa kutumia mashine anazoziita MRI, itakayounganishwa na mashine za 'PET CT Scan' kuondoa usumbufu kwa wagonjwa wanaofuata huduma hiyo nje ya taasisi.

Anahitimisha kwa ahadi ya uimarishaji tiba ya mionzi, ili kuendelea kupunguza muda wa kusubiri tiba, ikitatuliwa kwa kununua mashine nyingine ya tiba bila mionzi.

AFYA

UNA SHIDA YA UKOROMAJI?

# Tatizo hilo liko hivi na linatibiwa kwa njia hii

**Na Mwandishi Wetu**

• Wanaume, wanene, wazee...



Hii ndo hali ya kukoroma katika maisha ya kitandani. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

KUKOROMA ni tatizo linalowapata watu wengi wakati wanapolala. Linaweza kuwatokea watu wa kila umri, ingawa zaidi ni wanaume na watu wanene.

Ina kawaida ya kuzidi kadri umri unavyoongezeka na asilimia 54 ya watu wazima hukoroma na wastani wa nusu yao wanakoroma kila wakati.

Kuna wakati, tatizo linakuwa kubwa na kuleta tu karaha kwa mtu anayelala jirani na mkoromaji. Hata hivyo, haimaanishi inafikia hatua ya kuharibu usingizi wa anayekoroma, pia kuwasumbua na kuwakeresha waliolala karibu na mkoromaji.

**MAANA YAKE?**

Wanaokoroma kila wakati na mara nyingi huchoka wanapoamka na watu wa aina hiyo, hushauriwa kumuona daktari kuhusiana na tatizo hilo.

Kunatokaje? Mtu anakoroma kunapokuwapo sababu yoyote itakayoziba kuingia au kutoka kwa hewa mdomoni na katika pua, pia kuta za koo hutikisika wakati wa kupumua na matokeo yake ni sauti inayosikika ya kukoroma.

Pia, kuingia au kutoka hewa kunaweza kuzuiwa na sababu mbalimbali kama vile, kuziba tundu za pua kwa kiasi fulani, kunakosababisha nguvu zaidi zitumike kupitisha puani, mtu anapokuwa amelala.

Ni hali ambayo kitaalamu inatajwa inaifanya nyama laini za pua na koo kukusanyika na kusababisha mkoromo. Kuna baadhi ya watu wanakoroma tu kipindi cha 'aleji na baadhi ya matatizo kama vile kupinda pua.

Inaelezwa, vilevile tundu za pua zina kawaida kuifanya pua zizibe na kusababisha kukoroma. Ni kawaida wengi wanaofanya operesheni za pua, hupatwa na tatizo la kukoroma.

Lingine ni misuli dhaifu katika koo na ulimi, au nyama za koo na ulimi zinapokuwa dhaifu, hulegea na kuanguka upande wa nyuma wa sehemu inayopita hewa. Suala hilo linatokea pale mtu anapolala 'fofofo' kunakomsababishia kukoroma.

Kuwa na misuli minene kooni, kuna watu wanene ambao nyama zao za koo nazo zina kawaida ya kunenepa na kupanuka, hata kuwasababisha kukoroma.

Ugonjwa wa wenye 'tonsezi' kubwa na 'adenoids' baadhi yao nao wanakoroma, hata ulimi mkubwa nao ni sababu, inapotikisika wakati hewa inapita kwa msukumo, nako husababisha kukoroma.

Umri mkubwa, nako umeshuhudiwa kuwa misuli na nyama za koo, huanza kuzeeka na kulegea kadri umri unayosonga.

Wanaume wanakoroma zaidi kuliko wanawake. Sababu ni kwamba, kuna njia nyembamba zaidi ya hewa; na kuna watu kukoroma kwao ni kwa kurithi.

Pombe, kuvuta sigara na matumizi ya baadhi ya dawa, yanasababisha misuli ya koo ilegee na kumfanya mtu akorome na mwisho kuna suala la kulala vibaya, kama vile chali, kwani kunafanya nyama za koo zilegee na kuziba hewa.

> **Vivyo hivyo, mdomo ukiwa wazi, kaza misuli ya nyuma ya koo na rudia kitendo hicho kwa sekunde thelathini. Unaweza kutazama kwenye kioo na kuona jinsi ulimi unavyoenda juu na chini.**



**DAWA YAKE NINI?**

Kukoroma huenda mbali hata kuathiri usingizi wa mkoromaji, kwani anayekoroma inambidi aamke kila mara ama akijua au bila kujua, kutokana njia zake za hewa kufunga kwa sekunde kadhaa na kukatika

Vilevile tunapaswa kujua, kukoroma kuna athari za kiafya za muda mrefu kwa anayekoroma, hivyo si jambo la mzaha na linapaswa kutatuliwa.

Mosi, mlalaji anayekoroma anapaswa kufunga mdomo na tendo hilo llinatoa ishara ya kuwapo matatizo ya ulimi; misuli au nyama za koo. Pia, mtu akikoroma ilhali yuko chali inamaanisha kuwa pengine kwa kubadilisha namna unavyolala, kukoroma nako kunaweza kwisha na kwa anayeendelea kukoroma akilala katika kila mtindo, inatoa ujumbe tatizo huenda ni kubwa zaidi.

Iwapo mtu anabadilisha namna unavyolala na haikusaidia, anashauriwa kujaribu mambo kadhaa. Mosi, kusafisha pua iliyoziba kuiwezesha kupumua vizuri.

Mtu anaweza, pia akatumia dawa za kusaidia kupumua kwa urahisi (nasal decongestants) zinazopatikana katika duka ya dawa.

Tiba nyingine ni kuacha kuvuta sigara na kulala mapema, ili kupata usingizi wa kutosha kila mara, huku ukijiepusha kuchoka sana.

Hiyo inaendana na wakati wa kulala unanyanyua kichwa kipimo cha nchi nne, inayosaidia kupunguza kasi ya upumuaji unaosaidia ulimi na taya kwenda mbele na kupunguza ukoromaji. Mkoromaji anapaswa kufanya hilo, kwa kutumia mito maalum ya kupunguza kukoroma au mbadala wa kulala bila ya mto.

Wataalamu wanasema kwamba, mtu anaweza kupunguza kukoroma kwa kuwa na kiwango cha kula, kutokula baadhi ya vyakula au dawa kabla ya kulala, kuepuka ukoromaji.

Hiyo inajumuisha yafuatayo:

o Kutokula mlo mkubwa kabla ya kulala.

o Kutokula vyakula vinavyotokana na maziwa au maziwa ya soya.


o Kutokunywa pombe kabla ya kulala.

o Kutotumia dawa aina ya 'antihistamines.'

o Kutotumia vyakula au vinjwaji venye kafeini.

Vilevile wenye tabia ya kukoroma, wanashauriwa kufanya mazoezi ya koo ambayo ni pamoja na kuimba, kusoma kwa kurudia rudia voweli (a,e,i,o,u) kwa nguvu kwa dakika tatu mara kadhaa kwa siku.

Kuweka ncha ya ulimi chini ya meno ya mbele na kurudisha ulimi nyuma kwa dakika tatu kila siku, pia achia mdomo ukiwa wazi peleka taya yako upande wa kulia na wacha ibakie katika hali hiyo kwa sekunde 30.



> **Umri mkubwa, nako umeshuhudiwa kuwa misuli na nyama za koo, huanza kuzeeka na kulegea kadri umri unaysonga.**

Vivyo hivyo, mdomo ukiwa wazi, kaza misuli ya nyuma ya koo na rudia kitendo hicho kwa sekunde thelathini. Unaweza kutazama kwenye kioo na kuona jinsi ulimi unavyoenda juu na chini.

Iwapo kukoroma hakutoisha kwa kutumia njia hizo tofauti zilizoelezwa, muone daktari akupe ushauri wa kitabibu kuhusiana na tatizo hilo. Kuna madakatari wataalamu wa magonjwa ya pua, masikio na koo wanaoweza kukusaidia kutatua tatizo hilo.

Hivi sasa, pia kuna vifaa mbalimbali vinavyotumiwa hospitalini kuzuia ukoromaji kama vile kinachowekwa kwenye meno (CPAP), au mgonjwa mgonjwa anafanyiwa operesheni kuondoa tatizo hilo.

***• wa mujibu wa taarifa za afya mtandaoni.***

# Shida kuu ya maradhi kuacha mboga, tunda

• Nyanya, kabichi vs moyo, kisukari





Mchanganyiko wa mboga na matunda unaounda lishe bora. **PICHA: MAKTABA**

MATATIZO YA kiafya yanayohusiana na kuwa vitambi na unene, ugonjwa wa kisukari na magonjwa ya moyo, yanaekezwa kuchangiwa sana na lishe duni.

Moja ya tiba jirani kwao, inatajwa ni ulaji mboga na matunda, kusaidia kujihami na maradhi mbalimbali katika jamii. Mtaalamu Jacky Ganry, kutoka Kituo cha Utafiti wa Kilimo nchini Ufaransa, katika kongamano mojawapo mjini Dakar Senegal, anasema nchi nyingi za Afrika, nusu ya watu wake wanauzito wa juu, usiolingana na wastani unaotakiwa.

Hilo linaelezwa, huku akirejea Shirika la Afya Duniani, WHO, limeweka wastani wa kiwango cha gramu 400 za matunda kuliwa na mtu kwa siku.

Watu wengi wanaoishi mijini, inaelezwa maisha yanabadilika katika ugumu na mpangilio wa mlo wao pia unabadalika.

Hapo ikiongezewa kutofanyika mazoezi na upungufu wa kula matunda na mboga za majani, kunachangia kwa kiwango kikubwa kuongezeka magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile kansa, shinikizo la damu, kisukari na yanayohusiana na moyo.

Maeneo ya mijini Afrika, kunaelezwa watu wengi ni wanene zaidi, ikilinganishwa na vijijini, kukitolewa mfano wa nchini Ethiopia, mwaka 2005, kulikuwapo idadi ndogo ya watu wanene, lakini asilimia 31 ya vifo vyote nchini humo kwa mwaka huo, vilitokana na magonjwa yasiyo ya kuambikiza

Nchini Senegal huko nyuma mwaka 1980, kulikuwapo wagonjwa wapya 200 tu wa kisukari kwa mwaka wakati huo, lakini sasa wameongezeka kufikia wagonjwa 2000.

Mtafiti huyo anasema, ongezeko la kupatikana na matumizi ya matunda na mboga za majani Afrika, bado ni changamoto kubwa, kwa sababu ya kuongezeka miji mikubwa, mabadiliko ya milo, kuongezeka gharama ya vyakula na ubora wake kushuka.

Ni mjadala wa kongamano lililoandaliwa na Shirika la Chakula na Kilimo kwa jili ya kutafuta namna mbonga na matunda inaweza kuwafikia watu wengi na kwenye miji inayokuwa haraka

Mkulima wa mboga, Chris Ojiewo, kutoka Tanzania, alisema utapiamlo na unene barani Afrika, unakuwa mzigo maradufu na rai yake ilikuwa Waafrika watumie mboga za majani za asili zinazolimwa kwa kirahisi na zina kiwango kikubwa cha virutubisho, kuliko vyakula vingine ili kuweza kutatua tatizo la utapiamlo na unene.

Pia, alikuwa ana rai Waafrika wengi wa tabaka la kati ambao ni wanywaji pombe na 'nyama choma' washawishiwe kuachana na vyakula hivyo, badala yake wale vyakula vya asili kama nyanya chungu, nyanya mshumaaa.

Baadhi ya mboga za asili ni chungu, na hazimpi mtu hamu ya kula, lakini zinatajwa kuwa na virutubisho vingi.

Wataalamu wa virutubisho, wanaelezwa kufanya kazi kubwa ya kuwafundisha kinamama jinsi ya kupika mboga na kutayarisha matunda, lakini mara nyingi inamaanika ni kwa ajili ya kuwa na umbo jembamba kutokana na kiwango cha virutubisho kilichono.

Ojiewo anasema, mtu mmoja anatakiwa kula gramu 16,300 za kabichi kwa mahitaji ya siku nzima kwa ajili ya Vitamini A, lakini hilo linaweza kufanikiwa kwa gramu 300 tu za nyanya chungu.

Ushawishi wa mboga za majani umefanikiwa sana katika nchi za Afrika Mashariki, ambao maduka makubwa yanayouza vyakula taratibu, yanapunguza mtindo wa kuuza bidhaa za mboga zinazoagizwa kutoka nje na badala yake kuuza zile zinazolimwa nchini.

**• Kwa DW Desemba, 2010**

MAZINGIRA

# Nani anainyima jiji Dar es Sal haki kuishi Mazingira Safi, Sa



Na Gerald Kitabu

DAR ES SALAAM, ndilo jiji kubwa zaidi nchini, kwa misingi ya idadi kubwa ya wakazi na shughuli zao za kiuchumi.

Aidha, ndicho kitovu cha biashara nchini na eneo lenye kiwanja kikubwa cha ndege, bandari kubwa inayohudumia Tanzania na nchi za jirani. Ni makao makuu ya mashirika kitaifa na kimataifa.

Pia, inatajwa kuwa moja ya miji inayokuwa kwa kasi zaidi barani Afrika. Sifa ya ukuaji wa Dar es Salaam inadhihirishwa na kiasi cha uwekezaji kinachoendelea kwenye ujenzi wa miundombinu.

Idadi ya shughuli za ujenzi zinanazoendelea Dar es Salaam, iko katika uendelezaji barabara, majengo na daraja.

**UZALISHAJI TAKA**

Ofisa Miradi wa Timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira (LEAT), Franklin Masika, anasema pamoja na sifa nyingi za jiji la Dar es Salaam ndilo linaloongoza kwa uzalishaji wa taka ngumu za viminika na za hewa.

Masika anasema, nani anaichafua Dar es Salaam na nini kipimo cha uchafu wa mji huo? Kutokana na uchafu huo serikali inaingia gharama kiasi gani? Je, uchafu unaifanya Dar es Salaam isifikie kikamilifu haki ya kuishi katika mazingira safi na salama?

Wakati wa kujiuliza hayo, kuna haja ya kurejea jitihada za serikali inavyosimamia namna mpya ya kusafisha taifa kwa jumla yake, hata kupitia amri ya kutimika siku ya Jumamosi kusafisha miji nchini, zikiangaliwa jitihada za serikali katika ngazi mbalimbali.

Mojawapo ni Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 na namna inavyolinda Mazingira ya jiji la Dar es Salaam kwa ujumla. Katika hilo, inafahamika halmashauri mbalimbali zina sheria ndogo za kusimamia mazingira yake.

Pia, kitaifa kuna Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), maofisa mazingira na maofisa afya nchini wanaolinda nchi dhidi ya uchafuzi huo.

Katika mamlaka mbalimbali nchini, suala la mazingira linashughulikiwa katika sura mtambuka na kuna jitihada nyingi zilizoleta mafanikio mara kadhaa.

> Ni jambo la kufadhaisha kuona kuta zilizoandikwa 'usijisaidie' au 'usikojoe hapa.' Ni kama vile jamii ya wakazi wa Dar es Salaam bado haijastaarabika.



Hali ya vyoo ambavyo haviko katika mazingira sahihi.**PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Pamoja na jitihada zinazoendelea, katika uhalisia bado jiji la Dar es Salaam lina changamoto kubwa, hasa linapokuja suala la haki ya kuishi katika mazingira safi na salama. Na ili kuweke suluhu ya kweli dhidi ya changamoto hizo, ndipo kunahitajika haja ya kubainisha, ni nani hasa anayewahujumu wakazi wa Dar es Salaam na miji mingine yenye hadhi hizo, kupata haki ya kuishi katika mazingira safi na salama.

Lazima tufahamu nani anazalisha taka, nani anatupa taka hovyo, nani hana choo, nani anatiririsha maji machafu, nani anafumbia macho uchafu, nani anazalisha moshi wenye sumu, nani anatuzalishia kelele kwenye makazi na kadhalika.

Masika anasema si kwamba, hakuna kinachifayika. Zipo nyingi tena za wazi. Halmashauri zote za jiji la Dar es Salaam, zinalinda mazingira.

Hivi sasa kuna sheria ndogo na mabango ya kuelimisha na kuonya wachafuzi na kuna wafuatiliaji katika ngazi mbalimbali wapo, sambamba na kampuni zenye kandarasi ya kukusanya taka zipo. Bado

# laam alama?





Taka zilizozagaa mitaa ya Kariakoo, jijini Dar es Salaam. Kulia, taka katika maeneo mengine.



Zilivyo kampeni za uzoaji taka, Temeke jijini Dar es Salaam.

changamoto zipo.

Ni jambo la kufadhaisha kuona kuta zilizoandikwa 'usijisaidie' au 'usikojoe hapa.' Ni kama vile jamii ya wakazi wa Dar es Salaam bado haijastaarabika.

Ni kama Dar es Salaam inaishi katika nyakati za ujima. Inawezekanaje mwaka 2019, watu bado wakakumbushwa maeneo ya kujisaidia?

**NANI ANAHUJUMU?**

Ofisa Miradi wa LEAT, Franklin Masika, anasema Dar es Salaam inahujumiwa na wengi. Katika tafsiri sahihi, wahujumu kimazingira wanaweza kugawanywa katika makundi makuu matatu.

Kwanza, ni wazalishaji wakuu wa taka. Hao ndio wanatajwa kuwa wahujumu wakuu wa haki za mazingira na tafiti zinaonyesha viwanda ndivyo hatua ya awali ya uzalishaji huo wa taka. Taka hizo huwa ni za namna zote.

Kwa mfano hivi sasa, mtu akitembea mitaani, mara moja anaona chupa za bidhaa za viwanda fulani zikizagaa kwenye mitaro, vizimba na kwingineko.

Chupa hizi kwa kiasi kikubwa ambazo ni za plastiki, zinaweza kuwa mfano mmojawapo tu. Viwanda vingi ni wazalishaji taka na wakati kwa kiasi kikubwa ndio sababu ya awali ya taka kuzagaa mitaani.

Kuna viwanda vinavyotiririsha maji yenye sumu. Tafiti mathalani za maji katika Mto Msimbazi jijini Dar es Salaam, zinaijulisha umma juu ya kuwapo sumu inayomiminwa na viwanda hivyo.

**MAJI MSIMBAZI**

Maji ya Mto Msimbazi hutumika na wakulima wadogo wa bustani za mboga, ambazo ndizo lishe kuu ya wakazi jijini na kwa maana nyingine, viambata vya sumu huingia kwenye mfumo wa chakula na baadaye kuwaathiri kiafya walaji.

Hiyo ni hatari kwa afya, hususani za masikini ambao ni wengi na wateja wakuu wa mlo huo, huku baadhi wakitumia maji yake kama katika ufuaji.

> **Kuna viwanda vinavyotiririsha maji yenye sumu. Tafiti mathalani za maji katika Mto Msimbazi jijini Dar es Salaam, zinaijulisha umma juu ya kuwapo sumu inayomiminwa na viwanda hivyo.**

Kundi la pili ni wakazi wa Dar es Salaam. Kimsingi, ni kundi hili ni kubwa. Tunapoungumza juu ya wakazi zaidi ya milioni tano tunazungumza juu ya kundi kubwa linalozalisha taka na kutokana na idadi kuwa kubwa basi wakazi ndio wanaofanya uhujumu zaidi.

Hadi sasa bado kuna wakazi wa Dar es Salaam ambao mara baada ya kutumia bidhaa huzitupa nje kupitia vioo vya magari. Inasikitisha kuona mtu anajiskia ufahari kwa kutupa taka, hali iliyo kimyume na jamii iliyokosa ustaarabu.

Kuna jingine, kuwapo wakazi wasio na vyoo na jiji la Dar es Salaam, ina wakazi waliogoma kufuata taratibu za kudhibiti taka.

Haiwezekani mwaka 2019 mtu azalishe taka kisha aamishe jukumu la kuzisimamia kwa watu wengine kwa kuzitupa mtaani. Lazima kila mtu ajenge utamaduni wa kushughulika na taka anazozalisha. Ni utamaduni wa waliostaarabika.

Kuna wakazi wa Dar es Salaam, wanakiuka kwa makusudi taratibu za usimamizi wa Mazingira. Kuna wanaochimba michanga kwenye kingo za mito ili kujinufaisha kwa kipato, kinyume na Sheria inayosimamia Mazingira.

Tatu, wanaohujumu Dar es Salaam ni waliopewa kandarasi za kukusanya taka na kusafirisha kwenda kwenye maeneo yaliyochaguliwa kuhifadhi taka. Kundi hilo linauhujumu, njia mojawapo wengi hawana rasilimali za kutosha kuwezesha ukusanyaji taka kwa wakati.

Pili, kuna wakati kazi zinafanywa kwa kulipuliwa. Mara kadhaa kusikika wakazi wa maeneo mbalimbali jijini Dar es Salaam wakilalamikia watoa huduma za kuzoa taka kuwa hawafuati ratiba na hivyo kulazimu wakazi kukaa na taka kwa muda mrefu huku wakisubiri wakusanyaji.

AFYA

# Ukisikia 'kichanga' chako kinalia, sababu hizi hapa, unamkabili hivi

• Kanuni 6 kukufungua masikio



Mtoto akilia, akibembelezwa na mama yake. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Mwandishi Wetu**

WAZAZI huwa na furaha baada ya kupata mtoto, hujisikia watu wenye bahati kwa kuongeza idadi ya familia.

Mama anapokuwa ujauzito, matunzo na uangalizi unakuwa wa kipekee pale anapojifungua mtoto, kwani kipindi hicho umakini na uangalizi unakuwa wa hali ya juu.

Kimsingi, mara mtoto anapozaliwa hadi anapofikia umri wa mwaka mmoja, anakuwa hawezi kujieleza japokuwa ana uwezo mkubwa wa kusikia na kuelewa jambo lolote linalomzunguka.

Ni kawaida ya watoto wachanga wenye umri huo wanakuwa na matatizo mengi na ndio maana wataalamu wanashauri, kila unapoona dalili ambazo huzielewi, mzazi anatakiwa kumuwahisha haraka hopitalini, kwa ajili ya uchunguzi wake kiafya.

Hata hivyo, kuna baadhi ya dalili ambazo mzazi au mlezi anapobaini, anaweza kujua mtoto anakabiliwa kitu gani kwa wakati huo, hivyo anamsaidia mtoto na tatizo linaisha.

Moja ya ishara anazotoa ili, kufahamisha kuwapo tatizo, liwe la kimwili au kihisia, ni kulia nyakati za usiku au mchana.

> **Japokuwa viungo vya mtoto vinakuwa viteke na si rahisi sana kuvunjika, lakini anaweza kuhisi maumivu au uzito anaouona si jambo la kawaida kwake.**

Kulia ndio njia pekee ya inayoonyesha hisia zake, kwamba ana tatizo ili mzazi achukue hatua za haraka kumsaidia.

Baadhi ya wazazi au walezi ambao ni mara yao ya kwanza kulea watoto wachanga, inakuwa vigumu kwao kujua sababu za kilio cha namna mbalimbali.

### KWA NINI KULIA?

Zifuatazo ni sababu ambazo mtoto anaweza kulia usiku na hatua ya kuchukua.

Kulaliwa: Kwa bahati mbaya mzazi anaweza kumlalia mtoto kwenye sehemu yoyote a ya kiungo chake, hivyo mtoto analia kueleza kwa ishara hisia yake.

Japokuwa viungo vya mtoto vinakuwa viteke na si rahisi sana kuvunjika, lakini anaweza kuhisi maumivu au uzito anaouona si jambo la kawaida kwake.

Ni msingi, mzazi anapolea ahakikishe hapati usingizi mzito ambao unaoweza kukufanya asitambue unachokifanya na kama umemlalia sehemu ya kiungo, basi amuondoe haraka mtoto huyo awe mbali kidogo na mama yake.

Pia, anaweza kumsaidia kunyoosha baadhi viungo, pamoja na kumpaka mafuta ya kumlainisha

Tumbo na maumivu: Watoto wachanga wanasumbuliwa sana na maumivu ya tumbo na inawezekana kusababishwa na kutopata choo kwa uhakika kutokana na mmeng'enyo wake kutofanya kazi vizuri.

Hiyo inatokana na aina ya maziwa ya mama au 'bandia' anayopewa kuwa na matatizo, huku mfumo wake wa chakula bado ni mpya na unaendelea kukua, hata kuzua shida katika kumeng'enya chakula.

Mara nyingi, gesi inajaa na kusababisha maumivu kwa mtoto. Shida hiyo si rahisi kukabiliana nayo na imekuwa ikiwapa wakati mgumu wazazi kwa watoto chini ya miezi mitatu.

Kinachotakiwa kufanyika hapo, ni kumlaza mtoto kifudifudi, ili atoe upepo, Ni njia inayoshauriwa, lakini katika usimamizi wa karibu tena wa hali ya juu.

Hata hivyo, ni hatari kumlaza mtoto mchanga kifudifudi kwa kuwa anaweza akajiziba hewa na kumhatarishia kifo.

Kumshikashika tumbo kwa mikono au kitambaa chenye maji ya uvuguvugu, nako kunaweza kukamsaidia kumtuliza mtoto.

Njia nyigine inayofafanuliwa ni matumizi ya dawa za kusaidia kulainisha utumbo wa mtoto na kutoa gesi, lakini kupitia ushauri wa wataalamu wa afya.

Kuhisi njaa: Mtoto akiwa na njaa na anahitaji chakula, anaweza kulia ili kutaka shida yake itatuliwe. Lakini, kwa bahati mbaya hana namna ya kukujulisha kuwa ana njaa bali ni kilio.

Ni vyema kufahamu aina ya sauti ya kilio anachokitoa kama kinaashiria njaa. Mzazi au mlezi atajua hili, kwa mazoea yake ya kila siku na mtoto wako.

Ili kuhakikisha hana tatizo hilo, anatakiwa kumpa mtoto chakula kila mara. Katika hilo, mzazi au mlezi huyo, anatakiwa kufuata taratibu za lishe bora, kwa kumpa chakula katika umri unaotakiwa na kama bado ampe maziwa kila mara anapohitaji, ili kuhakikisha hana njaa.

Kama mtoto anaendelea kulia baada ya kula au anakataa chakula, basi kutakuwa na sababu nyingine ya kiafya, amuone mtaalamu wa afya mara moja.

Kuhisi joto au baridi: Joto kali au baridi, inamfanya mtoto ajisikie vibaya kutokana na ngozi yake kushindwa kuhimili hali hiyo ya hewa.

Jambo linalotakiwa ni kukabili mapungufu hayo, ni kuwa makini kwa kuangalia mabadiliko ya hali ya hewa na kuhakikisha kama kuna baridi, mtoto avalishwe nguo nzito na kama kuna joto, nguo nyepesi za pamba zinafaa zaidi. Endapo joto likizidi, mzazi ana wajibu kuwasha feni au kiyoyozi.

Uchovu na usingizi: Kuna wakati watoto wanalia wakiwa na usingizi na hiyo inatokea mara nyingi. Hadi sasa kuna watoto wengi wanaelezwa kuwa na tabia ya kulia kabla ya kulala.

Kinachoshauriwa katika hilo, mtoto anatakiwa kulala kwa saa 12 hadi 15 kwa siku, kulingana na umri wake.

Mtoto mchanga hadi umri wa miezi mitatu, anatakiwa kulala kwa saa nyingi zaidi kuliko wenye miezi minne hadi mwaka mmoja.

Kuna watoto wengine wanaolala vizuri wakiwa wameshikwa mikononi na kuchezeshwa, kuliko kitandani. Watoto hao wanahitaji kubebwa na kukumbatiwa. Hii ni njia ya asili ya kuonesha upendo kwa binadamu huyu mdogo.

Kubadilishwa nepi: Mtoto anaweza kulia kama katika nguo zake kuna unyevu unaomfanya kujisikia vibaya na muwasho.

Hapo inahitajika kubadilishwa nepi, kuoshwa na kuvishwa nguo nyingine. Walezi wengi wanajisahau kubadilisha nguo hasa nyakati za usiku, hivyo kumfanya mtoto kulia

Suala la kuzingatia, Mtoto anayelia, anahitaji msaada na anatoa ishara ya mawasiliano kuwa ana shida. Kwa kuwa hawezi kusema wala kuonesha ni nini kinamsibu, mzazi au mlezi unatakiwa kutambua kwa haraka tatizo ili kumuondolea tatizo.

Mbinu zilizotajwa zinaweza kusaidia kukabiliana na matatizo yanayosababisha mtoto mchanga kulia usiku au mchana.



# TRA kutokusanya kodi ya ardhi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amesema serikali haina mpango wa kutumia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kukusanya kodi ya pango la ardhi.

Badala yake, amesema jukumu hilo litafanywa na watumishi wote wa idara ya ardhi katika maeneo husika.

Lukuvi alitoa tamko hilo juzi wakati akifungua mafunzo ya siku mbili ya mfumo mpya wa ukusanyaji kodi ya ardhi ambayo yanafanyika jijini Mbeya yakishirikisha maofisa ardhi na mipango miji kutoka mikoa yote ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

“Wizara yangu haina mpango wa kuwatumia TRA kukusanya kodi ya pango la ardhi, badala yake jukumu hilo litafanywa na wadau wote wanaojihusisha na upangaji wa matumizi ya ardhi kwa sababu wao ndio wanaojua nani anamiliki ardhi ipi na kwa matumizi gani,” alisema.

Kutokana na uamuzi huo, Lukuvi alisema kuanzia sasa suala la ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi litashughulikiwa na wadau wote wanajihusisha na upangaji wa matumizi ya ardhi kuanzia maofisa mipango miji, wachora ramani, wathamini na maofisa ardhi.

Alisema pamoja na majukumu mengine ya matumizi ya ardhi kama vile kupanga miji, kupima ardhi na kutoa hati za umiliki wa ardhi, jukumu kubwa na maofisa ardhi litakuwa kukusanya maduhuli ya serikali ikiwamo kodi ya pango la ardhi.

Kwa mujibu wa Lukuvi, kila wilaya nchini itakusanya kikamilifu kodi ya ardhi ili kuiweka vizuri katika mchango wake kwenye pato la taifa.

“Tunahitaji mchango wa idara ya ardhi uonekane kwenye pato la taifa, hivyo kila wilaya nchini italazimika kukusanya kodi hii kwa jitihada kubwa ili tuuone mchango wake kwenye pato kubwa la taifa,” alisema Lukuvi.

Waziri aliwaonya maofisa ardhi watakaotumia vibaya nyadhifa zao kukadiria vibaya kodi ya pango la ardhi kwa kupunguza kiwango ambacho mmiliki anapaswa kulipa huku akisisitiza kuwa kufanya hivyo ni uhujumu uchumi.

“Natambua maofisa ardhi mmekuwa na tabia ya kukadiria kodi ya pango la ardhi chini ya kiwango au kupunguza ukubwa wa eneo ambalo mtu anapaswa kulilipia kodi kwa nia ya kumpunguzia kodi, huku ninyi mkipokea virushwa vya ajabu ajabu. Ole wenu mkibainika sitakuwa na huruma na mtu wa aina hiyo,” alionya.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pia imeamua kuvunja kanda zote nane za makamishna wa ardhi nchini na majukumu yao kuyahamishia katika kila mkoa ambako imeamua kupeleka Kamishna wa Ardhi kila mkoa ili kusogeza huduma kwa wananchi.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (wa pili kushoto), akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Msingi Iyunga, alipokutana nao njiani katika Mtaa wa Lumbila Kata ya Iwambi, jijini Mbeya, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Siri Jiji la Mbeya kushika mkia katika mapato bayana

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya haikuwa na mpango mkakati wa kuongeza mapato ya ndani tangu mwaka 2012, hali ambayo imesababisha kushika nafasi mwisho kwenye ukusanyaji wa mapato kati ya majiji sita nchini.

Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Saad Mtambule, alisema hayo jana alipokuwa anazungumza na halmashauri hiyo itakavyotumia vitabu vitatu vya miongozo ya maendeleo vilivyoandaliwa kwa ushirikiano na mradi wa kuwezesha ukuaji kupitia biashara na uwekezaji (Engene) chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Watu wa Marekani (USaid).

Vitabu hivyo vilivyozinduliwa ni vya Mpango wa Kuongeza Ukusanyaji wa Mapato, Mkakati wa Kukuza Uwekezaji na Mpango Mkakati wa Jiji.

Alisema halmashauri hiyo ilikuwa haina mpango ambao ulikuwa unawawezesha kuweka vipaumbele vya kukusanya mapato pamoja na kukisia kwa uhalisia kiasi cha mapato ambayo vyanzo vilivyopo vitaliingizia.

“Tulikuwa tunatumia uzoefu kwenye ukusanyaji wa mapato kitu ambacho kilikuwa kinatufanya kuwa na ufanisi mdogo na tulikuwa tunashika nafasi ya mwisho kwenye ukusanyaji wa mapato,” alisema Mtambule.

Alisema kwa tangu walipoanza kutumia kitabu hicho cha mwongozo wa kuongeza ukusanyaji wa mapato, kiwango cha mapato kimekuwa kikiongezeka kila mwaka.

Alisema mwaka juzi walikusanya Sh. bilioni 11, mwaka jana Sh. bilioni 12 na kwa sasa ikiwa mwaka wa fedha unaendelea wameshafikia zaidi ya asilimia 45 ya malengo waliyojiwekea.

Aliushukuru uongozi wa Usaid kupitia mradi wa Engine kwa kuwasaidia kuandaa vitabu hivyo na kwamba wao wanatamani miongozo hiyo ingefundishwa katika halmashauri zote za mkoa wa Mbeya. Wakati wa uzinduzi wa vitabu hivyo, Mkurugenzi Mkazi wa Usaid nchini, Andrew Karas, alisema mradi huo una mkakati wa miaka mitano unaolenga kutoa kipaumbele kwenye kuongeza mapato ya halmashauri.

Aliipongeza serikali kwa kuendelea kushirikiana na shirika hilo katika miradi mbalimbali ambayo linatekeleza na kwamba ushirikiano huo unawapa nguvu ya kuanzisha mingine.

Pia alisema serikali ya Tanzania inafanya kazi nzuri ya kuboresha uhusiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwenye shughuli za maendeleo na kwamba hali hiyo inasaidia kuboresha hata ukusanyaji wa mapato.

“Mradi huu ni wa miaka mitano na unapata nguvu kubwa kutoka serikalini, tutaendeleza ushirikiano huu mpaka tuhakikishe huu mpango unafanikiwa,” alisema Karas.

Naye Mkurugenzi wa Mradi wa Engine, Rod Carvajal, alisema utafiti wao unalenga kuboresha huduma na ukusanyaji wa mapato kwenye halmashauri mbalimbali nchini.

Alisema lengo lao ni kushirikiana na serikali kuhakikisha usimamizi wa vyanzo vya mapato unaimarishwa na kuongeza mapato ya halmashauri ambazo zinahusika kwenye utafiti wao.

# Mbarali wajigamba kupata mavuno mengi

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WAKULIMA wa mpunga wilayani Mbarali mkoani Mbeya, wamesema wana matumaini ya kupata mavuno makubwa ya zao hilo kutokana na uwepo wa mvua za kutosha mwaka huu.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wakulima hao walisema mwaka huu maji wanapata ya kutosha kutoka kwenye mito mbalimbali pamoja na ya mvua.

Mmoja wa wakulima hao, Samson Luvanda, mkazi wa Igawa, alisema mwaka huu mvua inanyesha ya kutosha kiasi kwamba mito imefurika maji ya kutosha kutumika mashambani na mengine kuendelea kwenda kwenye Mto Ruaha Mkuu.

Alisema mwaka huu hakuna hata migogoro ya kugombania maji na wasimamizi wa Bonde la Mto Rufiji ambao wanasimamia Hifadhi ya Mto Ruaha.

Alisema wana matumaini ya kuongeza mavuno hata mara dufu kutokana na uwepo wa maji ya kutosha kwa ajili ya umwagiliaji wa mpunga ambao wamepanda.

“Miaka yote huwa tunapata tabu kutokana na kuingia kwenye migogoro na serikali kutokana na matumizi ya maji, mwaka huu skimu zote tunazotumia zina maji ya kutosha na maji mengine yanatiririka hata kwenye vikorongo vya kawaida,” alisema Luvanda.

Alisema kwa sasa wanachoiomba serikali ni kuimarisha huduma ya nishati ya umeme kwa madai kuwa viwanda vya kusindika mpunga huwa vinakwama wakati mwingine vinakwama kutokana na tatizo la umeme. Naye Sosten Joseph, ambaye ni miongoni mwa wananchi wanaolima katika skimu ya mnazi alisema miaka miwili iliyopita walipata matatizo ya kutaka kufukuzwa na serikali kwenye mashamba yao kwa madai kuwa skimu yao sio halali.

Alisema skimu hiyo ndiyo inayotegemewa na viwanda 15 vilivyopo katika Mji wa Rujewa kwenye uzalishaji wa malighafi na kwamba kwa mwaka huu wana matumaini ya kuongeza zaidi mavuno kutokana na maji kuwa mengi.





# LAAC yampa kibarua Mkurugenzi Jiji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) imemwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, kumaliza mgogoro wa kugombea eneo la biashara baina ya mganga wa kienyeji na kikundi cha watu wenye ulemavu.

Eneo hilo lipo katika Soko la Sabasaba jijini humo, ambapo kikundi hicho na mganga huyo kila mmoja anadai ni eneo lake.

Akizungumza baada ya kutembelea eneo hilo, Mwenyekiti wa LAAC, Vedasto Ngombale, alisema angependa kusikia kikundi hicho kinaendesha shughuli zake bila bughuza yoyote.

"Naomba umalize mgogoro huu haraka iwezekanavyo, hili eneo linajulikana ni la watu wenye ulemavu," alisema Ngombale.

Alisema hivyo kamati hiyo itaendelea kufuatilia ili kuona kama suala hilo limetekelezwa.

Aidha, aliwapongeza kikundi hicho kwa kuonyesha uwezo mkubwa wa kutumia fedha za mikopo kutoka halmashauri kuendesha biashara ambazo zinawasaidia kujikimu kiuchumi.

"Watu hawa wanastahili pongezi kubwa sana kwa sababu hawahitaji kuomba bali wameunda kikundi na kubuni mradi wa kufanya ambao unawapa faida ya kutosha," alisema Ngombale.

Naye Mjumbe wa Kamati hiyo, Mhandisi Christopha Chiza, alikitaka kikundi hicho kufanya hesabu zake vizuri ili wanapokaguliwa zisiwaletee tatizo lolote.

Alisema hawana sababu ya kufanya ujanja ujanja katika ujasiriamali wanaofanya hivyo ni vema wawe tayari wakati wowote kuja kukaguliwa hesabu zao ili biashara wanayofanya iende vizuri.

Akizungumza baada ya maagizo ya kamati, Mkurugenzi Kunambi alisema eneo hilo ni la halmashauri ya jiji na kwamba kikundi kitaendelea kutumia hadi hapo watakapotengewa eneo la biashara Nala. "Maagizo ya kamati nimeyapokea nitayafanyia kazi na kikundi hiki kiendelee kutumia eneo hili kwa ajili ya kuendelea na ujasiriamali ambao wanafanya, haya maeneo watu wamekuwa wakipeana kiholela tu, lakini hivi sasa suala hilo halipo tena hili eneo ni la serikali," alisema Kunambi.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, aliihakikishia kamati hiyo kuwa maagizo yaliyotolewa atasimamia utekelezaji wake.

Awali, akisoma taarifa ya kikundi, Katibu wa kikundi hicho, Alex Mbando, aliishukuru serikali kwa kujali kundi hilo kwa kuwapatia mikopo.

Kuhusu mgogoro huo, alisema mganga huyo tayari amefunga fremu mmoja ambayo walikuwa wanaitumia.



Mwendesha pikipiki wa kijiji cha Vingw'awe, Wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma, Sunder Chihonje, akipita kwa tahadhari kwenye barabara ya Mpwapwa-Berege jana, ambayo imeharibika vibaya kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha wilayani humo.
**PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wachinjaji kuku sokoni wapewa tahadhari

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAFANYABIASHARA wa soko la kuuza na kuchinja kuku Mwembe Tayari jijini Dodoma wametahadharishwa kujiepusha na magonjwa ya mlipuko kwa kuzingatia kanuni na sheria za usafi kutokana na eneo hilo kuwa chafu.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana na Ofisa Masoko wa Jiji hilo, James Yuna, alipofanya ziara ya kushtukiza kuangalia hali ya usafi katika soko hilo ambalo ni maarufu kwa uuzaji na kuchinja kuku.

Yuna alisema kuwa katika kipindi hiki cha mvua zinazoendelea kunyesha ni muhimu wafanyabiashara hao kuzingatia zaidi suala la usafi katika maeneo hayo wanayofanyia shughuli za biashara ya kuuza na kuchinja.

"Kwa kweli hali siyo mzuri, nimeikuta na kuiona maana nimekuta kuku waliochinjwa wamewekwa chini na hata hivyo bado hapo chini damu imetapakaa kila mahali hii ni hatari ugonjwa wa kipindupindu unaweza kujitokeza hapa," alisema.

Ofisa huyo alieleza kuwa kama wafanyabiashara hao hawatazingatia usafi unaotakiwa kwa maelekezo ya jiji, viongozi hawatasita kuwafungia biashara zao.

"Kwa sasa Dodoma ni jiji na ni makao makuu ya nchi wageni wanaingia kila saa kwa maana hiyo, ni lazima kuhakikisha usafi wa mazingira husussani katika masoko unazingatiwa.

"Hili soko la Mwembe Tayari lina sifa kubwa ya kuwapo kwa kuku wa kienyeji na wageni wengi wanataka kula kuku wa kienyeji kwa maana hiyo biashara ya kuku pamoja na machinjio yanatakiwa kuwa katika hali nzuri," alisema.

Aliongeza kuwa: "Mteja anapokuja katika soko la kuku na kumleta kuku wake hapa machinjioni hakute ni pasafi ili aondoke akiwa na furaha na hamu ya kula kuku ambaye anaandaliwa katika mazingira mazuri."

Katika hatua nyingine, Yuna aliagiza viongozi wa soko hilo kutafuta muda wa kufanya vikao na wafanyabiashara ili kuhakikisha usafi wa uhakika unafanyika ndani ya soko.

Alisema wafanyabiashara wasipozingatia usafi ndani ya masoko wanaweza kusababisha mlipuko wa magonjwa kwani walaji.

Wakizungumza na gazeti hili, wachinjaji hao walisema tatizo lililopo ni vitendea kazi ikiwamo na vifaa vya kuwahifadhia kuku hao wanaochinjwa na miundombinu ya soko hilo hairidhishi.

# Chamwino walia visima vya maji

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

WANANCHI wa Kata ya Loje Wilaya ya Chamwino, wameiomba serikali kuwachimbia visima vitakavyowaondolea kero ya kunywa maji ya Bwawa la Ingunguri Mtera.

Wakizungumza na Nipashe, walisema kutokuwapo visima vya kutosha vyenye majisafi na salama kunasababisha watumie maji ya bwawa hilo.

"Tunaomba serikali na kwa kushirikiana na Mbunge wa Mtera, Livingston Lusinde, kutujengea visima ambavyo vitakuwa vya kisasa vitawaondolea kero hii," alisema Pendo Msuliche.

Kwa upande wake, Diwani wa Viti Maalum aliwatahadharisha wananchi wanaojishughulisha na uvuvi wa samaki katika bwawa hilo la kuchemsha maji ili kujiepusha na magonjwa ya mlipuko.

Alisema hivi sasa wavuvi wanatumia maji ambayo si salama hivyo wanapaswa kuyachemsha ili yawe salama.

Diwani huyo, Hilda Kadunda, alisema kuwa wananchi wa Kata ya loje walio wengi wanatumia maji ya bwawa hilo na baadhi ya visima, lakini kutokana na hivi sasa na mvua zinazoendelea kunyesha zimesababisha kuchafuka.

"Wananchi wa Kata ya Loje wanaofanya shughuli zao za uvuvi bwawa la Ingunguri wanategemea maji hayo na kwenye visima kwa miaka mingi toka kuanzishwa kwake kwa kijiji hicho kwa shughuli za kibinadamu.

"Lakini kutokana na mvua inayoendelea kunyesha, bwawa la Mtera kwa sasa limejaa maji na limetapika na maji yamesambaa na kuingia katika visima vya maji ya kawaida ambayo yanayotumika," alisema.

Aliongeza: "Maji yanapotoka bwawani yanasomba takataka mbalimbali na uchafu kwa maana hiyo kama watu hawatachemsha maji hususani ya kunywa kuna uwezekano mkubwa watu kupata magonjwa ya mlipuko au magonjwa ya matumbo."



# Raia wa Ujerumani adaiwa kujiua kwa kisu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIA wa Ujerumani, Petern Lisches (43), anadaiwa kujiua kwa kujichoma kisu kwa sababu ambazo hazijaelezwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Awadh Juma Haji, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema kuwa tukio hilo lilitokea Kibweni Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema raia huyo alifika Zanzibar mwanzoni mwa Januari mwaka huu, na alikodi nyumba hiyo kwa ajili ya kuishi kwa siku ambazo atakuwa kwenye mapumziko.

Alisema mtalii huyo alikodi katika nyumba ya kupumzika wageni inayomilikiwa na Jafar Hussein huko Kibweni Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja.

Kwa mujibu wa Kamanda huyo, mwili wa Mjerumani huyo uligunduliwa na mmiliki wa nyumba hiyo, baada ya kutomwona mteja wake kwa siku moja na ndipo alipojaribu kufuatilia katika chumba chake na kukuta mwili wake sakafuni.

Kamanda Haji alisema uchunguzi wa awali ulibaini kuwa mtalii huyo ulikutwa ukiwa na kisu kidogo na majeraha sehemu ya mkono wa kushoto na shingoni.

"Uchunguzi wetu wa awali unaonyesha kwamba mtalii huyo amejiua mwenyewe kwa kujijeruhi kwani hakuna harakati zozote zinazoonyesha kwamba kulikuwa na juhudi za kumuua," alisema.

Aidha, alisema polisi wanaendelea na uchunguzi pamoja na kuwasiliana na Ubalozi wa Ujerumani nchini.




Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud (kushoto), akikabidhi pikipiki kwa bwanashamba wa wadi ya Cheju, Vuai Mwadini Vuai, kwa ajili ya utendaji kazi vijijini, katika hafla iliyofanyika Dunga Halmashauri ya Wilaya ya Kati Unguja, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri atangaza marufuku makonyo karafuu kuuzwa nje

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, amepiga marufuku wakulima wa zao la karafuu Pemba kuuza makonyo ya karafuu nje ya nchi.

Balozi Amina alisema hayo jana alipotembelea ujenzi wa kiwanda cha Majani makavu ya karafuu huko Mgelema Kisiwani Pemba.

Alieleza kwamba ni makosa kwa mujibu wa sheria za nchi wakulima kuuza makonyo nje ya nchi pamoja na bidhaa zinazotokana na karafuu.

Alisema kiwanda cha kusindika majani makavu ya karafuu mali ghafi yake kubwa inategemea majani makavu ya karafuu.

"Wizara ya Biashara na Viwanda inapiga marufuku wakulima wa karafuu kuuza makonyo nje ya nchi pamoja na bidhaa nyingine zinazotokana na karafuu kwa mujibu wa sheria," alisema.

Aidha, alisema juhudi za ujenzi wa kiwanda hicho ni sehemu ya kuwawezesha wakulima wa karafuu kuwaongezea soko la bidhaa zao ikiwamo makonyo.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Hemed Suleiman, alisema ujenzi wa kiwanda hicho ni moja ya fursa nyingine ya wakulima kufaidika na kilimo cha karafuu.

Aliwataka wakulima kuongeza bidii ya uzalishaji wa karafuu pamoja na kuuza bidhaa hiyo kupitia Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC).

"Hii ni fursa nyingine ambayo wakulima wa karafuu mnapaswa kuitumia kwa ajili ya kuongeza kipato kitakachosaidia kupiga hatua kubwa ya maendeleo na kiuchumi," alisema.

Karafuu ni zao tegemeo kwa uchumi wa Zanzibar, huku zikiwapo juhudi za ujenzi wa viwanda vidogo vidogo ambavyo vitasaidia kuongeza thamani ya uzalishaji wa zao hilo.

Tayari Kiwanda cha Makonyo kilichopo Pemba kimeanza kuzalisha bidhaa zaidi zinazotokana na malighafi ya zao hilo ili kuongeza thamani na kuwawezesha wakulima kupiga hatua kubwa ya maendeleo.

ZSTC ndiyo yenye jukumu la kununua na kuuza karafuu pamoja na bidhaa zake ikiwamo makonyo nje ya nchi.

# Matokeo kidato cha 4 yamkera ofisa elimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WALIMU wa Mkoa wa Kusini Unguja wametakiwa kuongeza bidii kuhakikisha kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa kidato cha nne unaongezeka.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mkoa wa Kusini Unguja, Kassim Abou Mtoro, alisema hajaridhishwa na matokeo ya mwaka huu ya mitihani ya kidato cha nne kwa wanafunzi wa Mkoa wa Kusini.

Alisema hayo juzi wakati wa kikao cha pamoja na walimu wa shule za Mkoa huo kilichofanyika katika halmashauri hiyo iliyopo Kitogani.

Alisema juhudi kubwa zimechukuliwa na uongozi wa mkoa katika kuimarisha sekta ya elimu ikiwamo upatikanaji wa vifaa vya sayansi.

"Serikali ya Mkoa wa Kusini Unguja haijafurahishwa na matokeo ya wanafunzi katika mitihani ya kidato cha nne...ufaulu umepungua sana," alisema.

Baadhi ya maofisa wa elimu Mkoa wa Kusini Unguja walisema kukosekana kwa ushirikiano baina ya walimu na wazazi kwa kiasi kikubwa kumechangia wanafunzi kufanya vibaya.

Ofisa wa Elimu Mkoa wa Kusini Unguja, Hamid Abdulrahim, alisema wanakosa ushirikiano kati ya wazazi ambao hawana ufuatiliaji mzuri wa watoto wao ikiwamo kujua maendeleo ya wanafunzi ya kila siku.

"Tunawaomba wazazi waongeze ushirikiano ambao utasaidia kuwapo kwa ufaulu mzuri wa mitihani ya kidato cha nne," alisema.

Naye Mwalimu Mkuu wa Sekondari Mkoa wa Kusini Unguja, Ali Suleiman, alisema wanafanya utafiti zaidi kujua chanzo cha wanafunzi kufanya vibaya katika mitihani ya kidato cha nne.

Alisema shule zote za mkoa huo za sekondari zinafaidika na vifaa vya maabara vya sayansi, hivyo hakuna sababu za wanafunzi kufanya vibaya.

"Tumepiga hatua kubwa katika shule zetu zilizopo Mkoa wa Kusini Unguja ambazo huduma za maabara ya sayansi zinapatikana bila ya matatizo," alisema.

Jumla ya shule sita za Mkoa wa Kusini Unguja wanafunzi wake wamefanya vibaya katika mitihani ya kidato cha nne, hatua ambayo imeufanya uongozi wa mkoa kuweka mikakati ya kukabiliana na tatizo hilo.

# Watumishi TRA kizimbani tuhuma za kupokea rushwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAFANYAKAZI wawili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), wamefikishwa mahakamani na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kwa tuhuma za kushawishi na kupokea rushwa ya Sh. milioni moja.

Mkuu wa Takukuru mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema wafanyakazi hao wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Dodoma kwa kushawishi rushwa hiyo kutoka kwa mfanyabiashara.

Aliwataja washtakiwa hao ni Emmanuel Erenest (31), Vincet Hassan (29) ambao walikamatwa juzi wakiwa katika eneo la majengo jijini hapa.

"Hawa wafanyakazi walimkamata mwendesha mkokoteni akiwa na mzigo wa Aluminium kwa kosa la kuwa na risiti ya EFD ya tarehe ya nyuma na isiyo na thamani halisi ya mzigo walioukamata," alisema.

Kibwengo alisema baada ya kuushikilia mzigo huo, walirudi na mwendesha mkokoteni hadi kwenye duka la Maliki Tarimo na kuacha ujumbe uliosema anapaswa kufika ofisi za TRA na pia wakuacha namba yao ya simu.

Alisema uchunguzi wa Takukuru unaonyesha kwamba baada ya muda kwa kupitia namba ya waliyoiacha dukani mwenye duka aliwapigia simu watuhumiwa ambao walimtaka Sh. milioni moja ili wasichukue hatua stahiki za kisheria dhidi yake na mnunuzi wa mzigo.

"Uchunguzi wetu umeonyesha kwamba watuhumiwa waliacha mzigo walioukamata baada ya kupewa rushwa hiyo na wala suala hilo hawakulitolea ufafanuzi ofisini kwao," alisema Kibwengo.

Alisema washtakiwa hao wametenda kosa hilo kinyume cha kifungu cha Sheria Namba 15(1) (a) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 Marejeo ya Mwaka 2018.

Katika tukio jingine, Mahakama ya Wilaya ya Kongwa jana imemhukumu Ofisa Mifugo Mwandamizi wa Halmashauri ya Kongwa, Dickson Urio (52), kwenda jela miezi sita au kulipa faini ya Sh. 300,000 kwa makosa matatu ikiwamo matumizi ya nyaraka za kumdanganya mwajiri kinyume na kifungu cha sheria 22 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa sura ya 329.

Mkuu huyo alisema hukumu hiyo ilitolewa jana mahakamani hapo na Hakimu Kisasila Saguda ambapo alimtaka mshtakiwa kuilipa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa Sh.1,638,000 ikiwa ni faini ya makosa matatu.

Kibwengo alisema kesi hiyo ya jinai namba 37/2018, katika uchunguzi wa Takukuru ilionyesha mshtakiwa alitumia risiti za kughushi na kumtaarifu mwajiri wake kwamba amenunua vifaa kwa ajili ya semina ya wafugaji jambo ambalo halikuwa la kweli.

## Taasisi zatakiwa kuwapa kipaumbele wanaosoma shahada uzamili

**Na Romana Mallya**

IDARA na taasisi zimetakiwa kutoa kipaumbele kwa watu wao kusoma Shahada ya Uzamili katika Taaluma ya Habari na Shahada ya Uzamili ya Uongozi wa Biashara, ili kuondokana na changamoto ya uongozi mahali pa kazi.

Naibu Mkuu wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Tumaini Dar es Salaam (TUDARCO), Prof. Andrew Mollel, alitoa wito huo jana jijini Dar es Salaam wakati chuo hicho kikizungumzia kuhusu kozi hizo mpya zinazotarajia kuanza mwezi Machi.

Prof. Mollel alisema wameshafanikisha utaratibu wote wa kuanza kwa kozi hizo na kwa sasa wanaendelea kupokea maombi.

"Wito wetu kwa watu wenye taaluma tofauti waombe kujiunga na mafunzo haya kwa sababu siyo tu yatawasaidia kwenye maeneo yao walikoajiriwa hata kuweza kujiajiri," alisema.

Mkurugenzi wa Masomo ya Juu chuoni hapo, Dk. Peter Mtesigwa, alisema kwa sasa wanaendelea kupokea maombi.

Alisema zifa za kujiunga kwa wale wenye shahada ya kwanza tathmini yake ya ufaulu inatakiwa isiwe chini ya GPA 2.7.

"Wenye Diploma ya Uzamili wanahitaji kuwa na GPA 4.0 na mwenye shahada isiyo bainifu angalau iwe daraja la B katika somo alilomakinikia," alisema.

Alisema lengo la kozi hizo ni kuwafanya wafanyakazi na wale wanaojiajiri kuwa mameneja wazuri.

Mkuu wa Idara, Taaluma ya Habari na Ukutubi, Dk. Getrude Ntulo, alisema Shahada ya Uzamili katika Taaluma ya Habari imelenga kuwaandaa watu katika nyanja mbalimbali ikiwamo kuwasaidia kuchambua mifumo ya mitandao ya kijamii.



Mkurugenzi wa Chama cha Kutetea Abiria (Chakua), Kanda ya Ziwa Victoria, Dickson Simon (katikati), akitoa elimu kwa madereva kuhusu kuheshimu haki za abiria, kwenye stendi ya mabasi mjini Bunda, mkoani Mara juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bodi ya kiwanda cha kahawa yachunguzwa

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

BODI ya Kiwanda cha Kusindika na Kukoboa Kahawa (TANICA) kilichopo Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, imetakiwa kupisha uchunguzi ili Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani humo iangalie utendaji kazi wao.

Agizo lilitolewa na Mkuu wa Mkoa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, alipokitembelea kiwanda ambacho kinamilikiwa na vyama vikuu vya ushirika Kagera Cooperative Union ( KCU )na Karagwe District Coperative Union (KDCU). Gaguti alisema kiwanda hicho kimekuwa kikifanya vibaya na kumekuwa na hujuma zinazokwamisha kuendesha miradi kutokana na kutopata malighafi kwa wakati.

Alisema bodi hiyo imepisha uchunguzi kutokana na utendaji wake kutokidhi malengo ya uzalishaji.

Aidha, alisema ili kutokwamisha na kufikia malengo kusudiwa, lazima bodi hiyo kupisha uchunguzi ili kupata ufumbuzi wa upatikanaji malighafi. "Kwa kutokuendelea kukwamisha na kutofikia lengo kusudiwa hii bodi iliyopo wapishe uchunguzi ili kupata suluhu ya malighafi," alisema Gaguti.

Alisema yamekuwapo matukio ya uingizaji wa malighafi nyakati za usiku, Takukuru ongeza uchunguzi wa kuangalia kwanini hakuna uongezekaji wa malighafi katika kiwanda hiki," alisema Gaguti.

Awali akisoma taarifa ya uzalishaji wa kipindi cha miezi sita kwa kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa huo, Mhasibu Mkuu wa kiwanda hicho, Didas Burchard, alisema, kiwanda hicho kinadaiwa Sh. milioni 160 likiwa deni la kahawa aina ya Arabika ambalo limebakia kutoka Sh. milioni 330 kwa kipindi cha mwaka 2019/20.

Burchard alisema kuwa kwa kipindi hicho cha miezi sita zilizalishwa tani 160 pekee wakati lengo la uzalishaji lilikuwa ni tani 200 kwa kahawa ya unga.

Alisema kahawa ya kukaanga imezalishwa tani 83 wakati lengo lilikuwa tani 116 kwa masoko ya ndani.

Mkuu wa Takukuru mkoani humo, John Joseph, alisema Januari 16, mwaka taasisi ilikamata watuhumiwa wanne wa kiwanda hicho kwa makosa ya kijihusisha na vitendo vya rushwa, ubadhirifu na uhujumu uchumi.

HABARI KIMATAIFA

# Ugonjwa wa ajabu kusambaa duniani

**WASHINGTON,** Marekani

MAOFISA wa afya wa China wamesema virusi vipya huenda vikazaana na kusambaa katika maeneo mbalimbali duniani.

Maofisa hao wameonya juu ya kusambaa kwa virusi huku wakitoa tahadhari, wakiongeza juhudi za kudhibiti maambukizi ya virusi hivyo.

Ugonjwa huo uligundulika nchini China hivi karibuni na wataalamu wa afya bado wanaendelea na kupata tiba yake, hadi sasa umeshaua watu huku wengi wakiendelea kuugua.

**Japo mfumo wa maambukizi haujaeleweka, kuna uwezekano virusi hivi vinaweza kuzaana na kusambaa.**

Idadi ya waliofariki kutokana na ugonjwa unaosababishwa na virusi hivyo imeongezeka na kufikia tisa huku watu wengine 440 wakithibitishwa kuugua.

Ofisa wa Tume ya Kitaifa ya Afya alikiri kuwa nchi hiyo kwa sasa iko katika awamu muhimu ya kuzuia na kudhibiti kusambaa kwake.

Juzi, mamlaka ilithibitisha usambazaji wa virusi hivyo kupitia binadamu.

Katika taarifa ya kwanza kwa umma tangu mwanzo wa mlipuko wa ugonjwa huo, Naibu Waziri wa Tume ya Afya ya China, Li Bin alisema kuna ushahidi kuwa ugonjwa huo unasambazwa kupitia mirija ya kutoa pumzi. Lakini China haijafanikiwa kubaini chanzo halisi cha virusi hivyo.

"Japo mfumo wa maambukizi haujaeleweka, kuna uwezekano virusi hivi vinaweza kuzaana na hatari ya kusambaa," alisema Li.

Onyo hilo linakuja wakati mamilioni ya watu kote nchini China wakisafiri kutoka eneo moja hadi lingine kuadhimisha mwaka mpya wa Lunar huku maelfu wakisafiri kutoka China kwenda nchi mbalimbali. **BBC**

## Bunge labariki Rais Trump kung'olewa

**WASHINGTON,** Marekani

BARAZA la Seneti nchini Marekani limepiga kura na kuidhinisha sheria zitakazotumika katika kesi ya kumwondoa madarakani Rais Donald Trump.

Baraza hilo lililo na idadi kubwa ya maseneta wa chama cha Republican limezikataa juhudi za Wademocrat za kupata ushahidi na kuhakikisha kwamba mashahidi wanasikilizwa.

Wakili Mkuu wa RaisTrump katika kesi hiyo alisema kesi ya Wademocrat ni juhudi zisizo na msingi kutaka kupindua ushindi wa Rais Trump katika uchaguzi wa mwaka 2016 ingawa mbunge mmoja wa chama cha Democratic amesema kuna ushahidi wa kutosha kuonyesha makosa ya Trump.

Baraza la Wawakilishi la Bunge la Marekani lilipiga kura ya kumwondoa madarakani Rais Trump mwezi uliopita kutokana na madai ya matumizi mabaya ya madaraka na kuzuwia mamlaka ya bunge la Congress kwa kuishinikiza Ukraine kumchunguza hasimu wake wa kisiasa ambaye ni Makamu wa Rais wa zamani, Joe Biden wa chama cha Democratic.

Hata hivyo, Rais Trump anashikilia msimamo wake kuwa hakufanya makosa yoyote. **DW**

## Watu 95 hufariki kila siku Mexico

**TOLUCA,** Mexico

WANAHARAKATI nchini Mexico wanatarajia kutembea umbali wa kilomita 130 wakifanya matembezi ya amani kupinga ghasia katika nchi hiyo.

Dhumuni la matembezi hayo ni kutokana na mauaji nchini humo kufikia viwango vya hali ya juu, huku watu 95 wakiuawa kila siku nchini humo, hii ikimaanisha kuwa mtu mmoja huuawa kila baada ya dakika 15.

Kwa mujibu wa taarifa rasmi, kulikuwa na mauaji ya watu 34,582 mwaka 2019, ikiwa ni idadi ya juu zaidi ikilinganishwa na wakati rekodi za mauaji hayo zilipoanza kuchukuliwa mwaka 1997.

Kwa mujibu wa taasisi ya uangalizi ya haki za binadamu nchini Syria, idadi hiyo ni kubwa ikilinganishwa na mauaji ya mataifa mengine ambapo wapiganaji wapatao 11,000 na raia waliuawa katika vita vilivyotokea nchini Syria mwaka 2019. **BBC**



Raia wa China wakiwa katika kituo cha treni cha Hankou huko Wuhan, mkoa wa kati wa China wa Hubei, wamejiziba pua kuhofia kuambukizwa ugonjwa wa ajabu uliozuka nchini humo. **PICHA: AFP**

# Serikali mpya yatangazwa, maandamano yaendelea

**BEIRUT,** Lebanon

LEBANON imetangaza serikali mpya katika juhudi za kumaliza maandamano ambayo yamedumu kwa miezi kadhaa.

Lakini maandamano na vurugu zimeendelea kushuhudiwa hata baada ya serikali mpya kutangazwa.

Waziri Mkuu wa nchi hiyo, Hassan Diab (60) alitangaza baraza lake la mawaziri 20, wengi wakiwa wataalamu wanaoungwa mkono na kundi la Hezbollah na vyama washirika kisiasa.

Hata hivyo, serikali hiyo ambayo imeundwa miezi mitatu baada ya aliyekuwa Waziri Mkuu, Saad Hariri kujiuzulu, imepingwa na waandamanaji wanaotaka mageuzi kamili na serikali iundwe na wataalamu huru wasioegemea upande wowote kisiasa wanaoweza kusuluhisha mgogoro wa kiuchumi na kifedha ambao umelikumba taifa hilo.

Diab aliwapongeza Walebanon kwa juhudi zao kutaka mageuzi na kuboresha huduma nchini humo, huku akisema kuwa sasa ni muda wa kufanya kazi, amewahakikishia wananchi kuwa serikali yake itashughulikia matakwa yao.

"Hii ndiyo mara ya kwanza, Lebanon imekuwa na serikali kama hii katika historia yake. Ni timu ya uokoaji, ambayo wajibu wake pekee ni kufanya kazi kwa bidii na kujitolea kikamilifu." Alisema Diab.

Lakini maelfu ya waandamanaji waliojitokeza mitaani na kuziba barabara katika mji mkuu Beirut na maeneo mengine nchini humo wakilalamika kuwa makundi ya kisiasa bado yamehusika katika kuwatangaza mawaziri wapya, hata kama ni wataalamu na wasomi.

Baadhi ya waandamanaji walionekana wakirusha mawe karibu na bunge hivyo kuwalazimisha polisi kuwatawanya kwa kuwafyatulia mabomu ya kutoa machozi pamoja na maji ya kuwasha. **DW**

## 15 wafariki boti ikizama ziwani

**KINSHASA,** DRC

WATU 15 wamepoteza maisha na wengine hawajulikana walipo, baada ya kuzama kwa boti katika Ziwa Mai-Ndombe, Magharibi mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Meya wa Mji wa Inongo alisema huenda idadi ya watu waliopoteza maisha ikaongezeka, baada ya ajali hiyo kutokea Jumatatu, wakati huu, juhudi zikiendelea kutafuta miili zaidi.

Ripoti zinasema kuwa boti hiyo ilikuwa inawasafisha watu 30 waliokuwa wametokea msibani, Kilomita 35 kutoka eneo la ajali hiyo. Katika miaka ya hivi karibuni, ajali za kuzama kwa boti zimeendelea kushuhudiwa nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, nchi ambayo bado inakabiliwa na changamoto ya miundombinu, watu wengi hutumia usafiri wa majini, kutokana na ukosefu wa barabara za kuunganisha maeneo mbalimbali.**RFI**

# Kilio cha X-ray hospitali ya serikali chapata ufumbuzi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

KILIO cha muda mrefu cha wakazi wa Mkoa wa Morogoro kuhusu kukosekana kwa mashine ya X-ray ya kisasa katika Hospitali ya Rufani ya mkoa huo imepata ufumbuzi.

Hali hiyo ilikuwa ikiwalazimu kupewa rufani kwenda Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kwa ajili ya matibabu.

Ufumbuzi huo umepatikana baada ya Serikali kusikia kilio chao na kupeleka mashine hiyo ya kisasa kama ilivyoahidi.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Dk. Ritha Lyamuya, alisema mashine hiyo imekuwa msaada mkubwa kwao kutokana na kuwa na uwezo kupiga na kutoa picha za teknolojia ya kisasa ambazo zinaweza kusomwa na watalaam waliopo nje ya mkoa huo na kutumwa majibu yake kwa njia ya mawasiliano ya intaneti.

Alisema kuwa mashine hiyo imesaidia kupunguza malalamiko ya wagonjwa ambao walikuwa wakikosa huduma ya X-ray kutokana na mashine iliyokuwapo awali kutokuwa na uwezo wa kufanya kazi na kusababisha baadhi ya wagonjwa kulazimika kwenda kupata huduma hiyo katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Dk. Lyamuya alisema kuwa mashine hiyo ina uwezo mkubwa wa kufanya kazi, hivyo kusaidia hata kupunguza idadi ya wagonjwa ina uwezo wa kutuma taarifa za mgonjwa kwa njia ya mtandao na kurejesha majibu ndani ya muda mfupi.

Mbunge wa Jimbo la Morogoro, Abdulaziz Abood ambaye alifika hospitali hapo na kujionea mashine hiyo ikifanya kazi ameishukuru Serikali kwa kusikia kilio cha wananchi wa Mkoa wa Morogoro ambaye aliwasilisha bungeni mwaka jana.

Abood alisema hatua ya Serikali kutekeleza ahadi yake hiyo inaonyesha kuwajali wananchi wa Mkoa wa Morogoro kwa kuleta mashine ya kisasa kwa ajili ya huduma za X-ray kwani kilikuwa ni kilio cha muda mrefu ambacho amekuwa akiiomba Serikali kuwasaidia kifaa hicho.

Alisema kuwa mara kadhaa amekuwa akiomba kupatiwa mashine hiyo hata akiwa bungeni. Alimshukuru Rais John Magufuli kwa kusikiliza ombi hilo maalum na kuwapatia mashine hiyo ya kisasa, na kuwaomba watumishi wa Hospitali hiyo kuitunza ili iweze kutoa huduma kwa muda mrefu.




Mkuu wa Idara, Taaluma za Habari ya Chuo Kikuu cha Tumaini Dar es Salaam, Dk. Getrude Ntulo (kushoto), akizungumza jana, wakati viongozi wa chuo hicho, walipokuwa wakitambulisha uanzaji wa kozi mbili za Shahada ya Taaluma ya Habari na Shahada ya Uzamili ya Uongozi wa Biashara. Katikati ni Naibu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Andrew Mollel na Mkurugenzi wa Masomo ya Elimu ya Juu, Dk. Peter Mutesigwa. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wakulima, wachakataji mafuta mawese kuwezeshwa mikopo

**Na Mwandishi Wetu**

WAKULIMA na wachakataji wa mafuta ya mawese mkoani Kigoma wamehakikishiwa kupewa mikopo na vifaa kwa ajili ya kuendeleza zao hilo.

Wamehakikishiwa uwezeshaji huo na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), ikiwaeleza kuwa kwa kufanya hivyo, watanufaika kiuchumi kwa kuongeza uzalishaji wa mafuta hayo.

Akizungumza na viongozi wa vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS) wa Wilaya ya Kigoma, Mkurugenzi wa Mikopo na Biashara wa benki hiyo, Agostino Chacha, alisema uwezeshaji huo utasaidia kuiondolea mzigo serikali wa kuagiza bidhaa za mafuta ya kula nje ya nchi na kuinua pia kipato cha wakulima na wadau waliopo kwenye myororo wa thamani wa zao hilo.

Chacha alisema kuwa benki hiyo imeishatoa jumla ya Sh. milioni 444 kwa ajili ya uanzishwaji wa kiwanda cha uchakataji wa mafuta ya kula mkoani humo, hali itakayowafanya wakulima wa zao hilo kuwa na soko la uhakika wa bidhaa zao.

Alisema pia kuwa hatua hiyo pia itawawezesha wakulima kuwa na uwezo wa kulipa mikopo watakayopewa na benki hiyo na zile za biashara.

Alifafanua kuwa: "Kwa wakulima watakaokuwa wamekidhi vigezo watapata mikopo kupitia utaratibu tuliongia na benki za biashara ambapo watapata kutoka kwenye benki hizo au kupata kutoka benki hiyo moja kwa moja."

"Kwenye vikundi hivi vinane vya michikichi vya wilaya hii ambavyo vimekidhi mahitaji na ndani ya kipindi kifupi kijacho watapata hizo fedha kwa ajili ya kuendeshea shughuli za zao kilimo," alisema Chacha.

# HakiElimu yataja sababu za shule kufaulu, kufeli

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA lisilo la serikali linaloshughulika na kufuatilia maendeleo ya elimu nchini (HakiElimu), limezindua ripoti ya utafiti inayoonyesha sababu zinazochangia baadhi ya shule kufanya vizuri na nyingine kufanya vibaya mfululizo katika mitihani ya darasa la saba nchini.

Akitoa ripoti jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa HakiElimu, John Kalaghe, alisema utafiti huo umefanyika kwa miaka miwili kati ya 2018 na 2019 katika mikoa 10 na ulilenga kuangalia na kujifunza mambo makuu matatu.

Alisema mambo hayo yalilenga kuangalia sababu mahsusi ambazo hazifahamiki zinazochangia baadhi ya mikoa kutofanya vizuri na mingine kufanya vizuri katika mitihani ya darasa la saba.

Jambo jingine ambalo waliliangalia ni iwapo ukanda wa kijiografia au utofauti wa mikoa ni miongoni mwa sababu zinazochangia ufaulu katika mitihani hiyo.

Pia ulilenga kufananisha na kutofautisha sababu za ufaulu kati ya mikoa isiyofanya vizuri na inayofanya vizuri katika miaka mitano mpaka 10 iliyopita.

"HakiElimu tuliona kuwa kufahamu sababu hizi kutaleta tija kwa baadhi ya mikoa ambayo ilikuwa inafanya vibaya kujifunza kutoka mikoa inayofanya vizuri na kutaisaidia mikoa iliyokuwa ikifanya vizuri kujiimarisha na kuendelea kufanya vizuri zaidi," alisema Kalaghe.

Katika matokeo ya utafiti huo, Kalaghe alitaja sababu ambazo zilibainika kuchangia matokeo mabaya kwa baadhi ya mikoa kuwa ni pamoja na nafasi finyu ya wazazi na walezi katika kuhamasisha watoto wao kufanya vizuri katika masomo na mitihani ya mwisho.

Sababu nyingine alisema ni umbali mrefu kutoka nyumbani kwenda shuleni na kutoka shuleni kwenda makao makuu ya wilaya, utofauti wa kimiundombinu kutoka mkoa mmoja na mwingine, changamoto za kimenejimenti na kukosekana kwa hamasa na mbinu za ziada katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji.

"Katika utafiti huu, ilionekana kwamba hata kukosekana kwa udhibiti mzuri kutoka kwa mamlaka za udhibiti wa elimu linachangia kwa kiwango kikubwa baadhi ya shule kufanya vibaya, kuna baadhi ya shule hazifikiwi kabisa na wakaguzi kutokana na miundombinu mibovu," alisema Kalaghe.

Miongoni mwa walioshiriki kufanya utafiti huo, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Richard Shukia, alisema walitumia mbinu mbalimbali ikiwamo kufanya mahojiano na wadau wa elimu, kuzungumza na wazazi, mikutano ya majadiliano katika ngazi mbalimbali na kupitia taarifa za machapisho.

"Kuna sababu nyingi ambazo ziliitajwa na watu waliohojiwa, lakini nyingi zilizojitokeza ni kwamba eti baadhi ya shule zinazofanya vizuri mfululizo katika matokeo yao wanafanya udanganyifu kwa kuiba mitihani, lakini wazazi kutokuwafuatilia watoto wao," alisema Dk. Shukia na kuongeza:

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MKOPO WA HARAKA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITD (EFL).** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumalizia tenda etc. Kwa maelezo zaidi **piga 0758 112 332. Karibu EFL**.

**TANZANIA RESEARCH AND CAREER DEVELOPMENT INSITUTE:** Inatangaza mhula mpya wa masomo Certificate na Diploma za kilimo na maendeleo ya jamii.maelezo zaidi tembelea tovuti yetu www.tracdi.ac.tz Simu:**0714404491/0746995144**

**WAHUDUMU WA HOTELI WANAHITAJIKA,** Hoteli ndogo Bagamoyo inatafuta wahudumu, wapishi, usafi, bartender wenye vyeti. **Piga 0757 129 546.**


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo
CHAMWINO MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;03/2020
Ombi la (1)ROPHINA.E.NGAILO(2)EVALISTO ELIAKIMU SANGA.Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HAPPY EDNARD NGAILO

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 21/01/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 14/01/2020.

Sahihi ya Hakimu

215596102

## KUPOTEA KWA KADI MSAMIRU KASSIM

**KAABUKA** anatangaza kupotea kwa kadi ya Bajaji aina ya Boxer yenye namba ya usajili MC674BZQ iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Yeyote atakaeion atoe taarifa kituo chcochcote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
KW/RB//17/2020

115595802

## TANGAZO LA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

JAFARI SITTA NYANDA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA KLUGER YENYE NAMBA ZA USAJILI T 139 DKZ YENYE CHASSIS N0 ACU 200111165 NA ENGINE NO 2AZ/603122

KWA YOYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI

**TAARIFA YA POLISI**
**KHM/RB/ TR/24/020**

215595902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**KINGOLWIRA MOROGORO**

Usimamizi wa mirathi **No;013/2020**

Ombi la **SHABANI SALEHE MARITE** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **ZAINABU SALEHE MARITE.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 23/01/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 09/01/2020.

215595502

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **AML FINANCE LTD, RAISSA COMPANY LTD** tutauza kwa mnada wa hadhara gari aina ya Toyota Hiace -T963 CMS mali ya mdaiwa sugu, Ndugu NEEMA KIPEJA na RAV4, T777 CBH mali ya Dina Bihondwa, mnada huo utafanyika tarehe 25/1/2020 Lengo ni kufidia/ kupunguza deni la mkopo anaodaiwa. Mnada utafanyika Tarehe 25/01/2020, mahali dhamana ilipo Makumbusho yard. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi.

Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Kwa mawasiliano fika kwenye ofisi zetu Victoria 5th floor au piga. 0652113262**

215595402


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# DE BRUYNE AWEKA REKODI YA ASISTI EPL

**MANCHESTER,** England

KEVIN De Bruyne ameweka historia kwenye Ligi Kuu ya England Jumanne kwa kuwa mchezaji wa kwanza kutoa pasi za mwisho 'asisti' 15 au zaidi kwenye misimu mitatu tofauti.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji ndiye aliyetengeneza bao pekee la ushindi la Manchester City dhidi ya Sheffield United juzi Jumanne.

Man City walipata ushindi huo wa bao 1-0 dhidi ya Sheffield kwa bao lililofungwa na Sergio Aguero kwenye dimba la Bramall Lane.

Lakini kazi kubwa ilifanywa na De Bruyne ambaye ndiye aliyetoa pasi ya mwisho kwa Aguero aliyekwamisha mpira huo wavuni na kufikisha mabao 16 kwenye Ligi Kuu ya England msimu huu.

Kwa kufanya hivyo, De Bruyne alifikisha 'asisti' ya 15 msimu huu, wakati msimu wa 2016-17 alitengeneza asisti 18 na msimu wa 2017-18 asisti 16.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, pia amefunga mabao saba kwenye Ligi Kuu ya England msimu huu.

## Lampard amtaja Kepa sare Arsenal

**LONDON,** England

FRANK Lampard amemtia moyo golikipa Kepa Arrizabalaga kwa kumtaka kusimama na kujiamini baada ya Chelsea kutoka sare ya 2-2 kwenye mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Arsenal juzi, Jumanne.

Golikipa huyo raia wa Hispania, Kepa, ambaye kiwango chake kwa sasa kinaibua maswali, alionekana kutochukua maamuzi ya haraka wakati Hector Bellerin alipoachia shuti na kusawazisha dakika ya 87 kwenye mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Stamford Bridge.

Jorginho na Cesar Azpilicueta waliifungia Chelsea huku Gabriel Martinelli akiifungia Arsenal baada ya mapema dakika 26 kipindi cha kwanza kumpoteza David Luiz aliyetolewa kwa kadi nyekundu.

"Najua kwamba wengi wanamwangalia yeye kwa sasa," alisema Lampard alipoulizwa kuhusu Kepa.

"Huu ndio mchezo wa soka ulivyo. Makosa yanaweza kuigharimu timu, lakini yeye kwa sasa anatakiwa kukaa na kutulia.

"Kwa mchezaji yeyote, hasa golikipa, watu watakuangalia wewe. Tupo nafasi ya nne, kitu ambacho siyo kibaya. Najua na tunajua kwamba tunatakiwa kupata angalau pointi nyingine 10. Hivyo ni jukumu letu kutulia na kuangalia mbele."



## Napoli sasa yajuta kumtimua Ancelotti



**NAPLES,** Italia

KLABU ya Napoli imeripotiwa kujutia uamuzi wao wa kumfuta kazi kocha Carlo Ancelotti na sasa wanamtaka aachane na Everton arudi.

Kocha huyo mwenye uzoefu mkubwa, Ancelotti alipoondolewa Napoli, nafasi yake ilichukuliwa na Gennaro Gattuso, lakini mambo ndio yamezidi kuwa magumu zaidi tangu kiungo huyo wa zamani wa AC Milan alipokabidhiwa timu.

Napoli imepoteza mechi nne kati ya tano walizocheza chini ya Gattuso kwenye Serie A tangu alipochukua mikoba hiyo Desemba 10, mwaka jana na kipigo cha karibuni ni kile cha 2-0 nyumbani mbele ya Fiorentina.

Mmiliki wa klabu hiyo, Aurelio De Laurentiis ameripotiwa kuchukizwa na matokeo hayo na sasa anajuta kwa kitendo cha kumfungulia mlango wa kutokea Ancelotti.

Huko Everton, Ancelotti mambo yake si mabaya, tangu alipopewa kazi Desemba 22, ameshinda mechi tatu, amepoteza mbili na sare moja, huku matokeo yake ya mwisho ni yale ya sare 2-2 dhidi ya Newcastle United juzi, Jumanne.

Huko Napoli kinachoelezwa ni kwamba huenda De Laurentiis akaingia tena sokoni kusaka kocha mpya baada ya Gattuso kuharibu mambo zaidi.

# Inter Milan yamgeukia Modric

**MILAN,** Italia

INTER Milan sasa inataka kumsajili Luka Modric kutoka Real Madrid kwa ajili ya kuimarisha kikosi chake.

Wakati ikiendelea na harakati zake za kumsajili kiungo wa Barcelona, Arturo Vidal mwenye umri wa miaka 32, na Christian Eriksen wa Tottenham Hotspur, Inter imeongeza jina la Modric katika orodha ya wachezaji inaowasaka.

Baada ya kushindwa kumsajili Modric wakati wa dirisha la usajili lililopita, Inter Milan imerudi kwa mara nyingine kuisaka saini ya staa huyo wa kimataifa wa Croatia ambaye mkataba wake Real Madrid unaisha mwaka 2021.

Kocha wa Inter Milan, Antonio Conte anaamini safari hii hawatakutana tena na upinzani mkali katika harakati zao za kumnasa staa huyo wa kimataifa wa Croatia kutoka kwa Madrid kwa sababu umri wake umeenda na mkataba wake wa kuitumikia timu hiyo unaelekea ukingoni.





# JORGINHO: SARE NA ARSENAL KAMA CHELSEA IMEFUNGWA

**LONDON** England

JORGINHO aliachwa akihisi ni kama Chelsea walipoteza mchezo dhidi ya Arsenal iliyokuwa na wachezaji 10 uwanjani baada ya "makosa" ya kipindi cha pili kuwagharimu na kujikuta wakigawana pointi kwa sare ya 2-2 juzi, Jumanne.

'Blues' hao walilazimishwa sare hiyo kwenye Uwanja wa Stamford Bridge licha ya Arsenal kucheza wakiwa na wachezaji 10 uwanjani baada ya David Luiz kuonyeshwa kadi nyekundu kwa kumfanyia faulo Tammy Abraham ndani ya eneo la boksi katika dakika ya 26 ya kipindi cha kwanza.

Jorginho alifunga bao la kwanza kwa Chelsea kabla ya Gabriel Martinelli kusawazisha dakika ya 63.

Makosa ya beki Cesar Azpilicueta ya dakika za mwisho yalifanya Arsenal kusawazisha na kugawana pointi, wakati Hector Bellerin alipomchambua na kupata bao la pili la kusawazisha na kukilazimu kikosi hicho cha Frank Lampard kukosa nafasi ya kuondoka na pointi zote tatu.

"Tunahisi kama tumepoteza mchezo," alisema Jorginho akiiambia BT Sport.

"Mchezo ulikuwa mkononi mwetu, halafu katika sekunde za mwisho tukaruhusu bao ambalo lilitugharimu. Tunahitaji kusonga mbele.

"Sidhani kama ni kujiamini kwa sababu tulicheza vizuri na tulitawala mchezo. Pengine jambo lililojitokeza ni kuhusu kutokuwa makini mchezoni."

# Guardiola: Laporte beki bora duniani

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amemsifia Aymeric Laporte kama "beki bora wa kushoto na kati duniani" baada ya kuthibitisha kwamba amerudi kwa Manchester City.

City imepitwa pointi 13 kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu, huku Laporte akiwa majeruhi tangu Agosti, lakini Mfaransa huyo alirudi kwenye kikosi cha Jumanne ambacho kilishinda 1-0 dhidi ya Sheffield United.

Kikosi cha Guardiola kilicheza mchezo wake wa pili bila kuruhusu bao kati ya michezo 12 iliyopita.

Baada ya mchezo huo bosi huyo wa Man City alibainisha kwamba kikosi chake kilimkosa kwa muda mrefu beki wao bora.

Alisema: "Ni beki bora wa kushoto na kati duniani. Fikiria timu bora duniani inampoteza beki wao bora wa kati, tulimkosa sana. "Ni mtaalamu wa mguu wa kushoto, yuko imara. Tulijua kwamba hatacheza kwa dakika zote 90, lakini alikuwa tayari kwa mchezo, Eric ni mchezaji bora kabisa."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MARTINELLI AMZIMISHA ARTETA SARE CHELSEA

Kucheza katika uwanja huu kwa namna alivyofanya na wachezaji 10 na dhidi ya Azpilicueta...

**LONDON** England

MIKEL Arteta ameukubali ushujaa na shauku ya Gabriel Martinelli kufuatia bao la kuvutia la kinda huyo kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu wakati ikipata sare ya mabao 2-2 katika Uwanja Stamford Bridge dhidi ya Chelsea juzi.

**Martinelli alitoka kasi nyuma ya katikati ya uwanja na kufunga bao hilo dakika ya 63, hivyo kusawazisha lile la Jorginho la kipindi cha kwanza lililopatikana kwa mkwaju wa penalti.**

Beki wa kati wa Arsenal, David Luiz alitolewa nje kwa kadi nyekundu dakika ya 26 kwa kumchezea faulo Tammy Abraham iliyosababisha penalti hiyo, lakini 'Gunners' waliodoka na pointi moja licha ya kwamba kipindi cha pili pia walitokea nyuma kusawazisha bao la pili.

Hector Bellerin alimpeleka siko kipa Kepa Arrizabalaga kwa shuti la mguu wa kushoto baada ya Cesar Azpilicueta kuiangusha Chelsea kwa kushindwa kuihakikishia ushindi dakika ya 83.

Kocha wa Arsenal, Arteta alisifu kujitoa kwa wachezaji wake na zaidi akitaja ukomavu wa Martinelli mwenye umri wa miaka 18, ambaye ameendelea kuvutia tangu alipotua Emirates akitokea kwao Brazil majira ya joto.

"Kucheza katika uwanja huu kwa namna alivyofanya na wachezaji 10 na dhidi ya Azpilicueta, ambaye kwa maoni yangu ni mmoja wa mabeki bora katika ligi, na alikwenda dhidi yake kila dakika, unahitaji ujasiri kwa hilo," Arteta alisema.

"Kisha nguvu yake. Nilihitaji kumtoa kwa dakika chache kwa sababu alionekana kukamiwa na alikanyagwa. "Si yeye pekee. Nadhani Laca [Alexandre Lacazette] alicheza kwa kiwango kizuri, ingawa hakufunga, na Nico [Nicolas Pepe] pia, na kila mmoja aliyeingia. Wanapigana sana katika mazoezi kujaribu kutushawishi kuchezeshwa zaidi.

"Wakati wanapohoji vitu fulani ninawaambia [kwenda] kuzungumza uwanja na hii ni kuzungumza uwanjani."

Arteta alilazimika kumchezesha Granit Xhaka kama beki wa kati baada ya kumpoteza David Luiz na alimsifu nahodha huyo wa zamani kwa uwezo aliouonyesha akitokea katika misukosuko iliyomsababishia kutaka kuondoka klabuni hapo.

"Nilijaribu kumshawishi kuwa hii ni sehemu sahihi kwake kubaki, kwamba nilitaka kumpa fursa ya kujaribu kufurahia kwa mara nyingine kucheza soka na kila kitu nilichomtaka kufanya kila kipindi cha mazoezi, yupo tayari kufanya," Kocha huyo wa Gunners, alisema.

"Leo [juzi] nilijua, wakati niliomweka pale, sikujua ni kwa namna gani alivyo mzuri atakavyokwenda kufanya, lakini alikwenda kuweka kila kitu nje ya pale, na ni mzuri."

## ZISIKUPITE

### AUBAMEYANG AWINDWA BARCA

BARCELONA imekuwa ikihusishwa na Pierre-Emerick Aubameyang, lakini kuondoka kwa mshambuliaji huyo Arsenal kabla ya mkataba wake kumalizika mwaka 2021 kunaweza kumgharimu nyota huyo wa Gabon kiasi cha pauni milioni 15.15 kama bonasi ya uaminifu. ***(Star)***

### BECKHAM KWA AGUERO, SILVA

KLABU ya David Beckham, Inter Miami imefanya mawasiliano na wawakilishi wa mshambuliaji wa Manchester City, Muargentina Sergio Aguero, 31, na kiungo Mhispania David Silva, 34, ambao wataondoka City majira ya joto. ***(Sun)***

### FERNANDES KIMEELEWEKA UTD

MANCHESTER United inaweza kumsajili kiungo Mreno Bruno Fernandes, 25, kwa dili la pauni milioni 55 mwishoni mwa wiki baada ya kufanikiwa katika mazungumzo yao na Sporting Lisbon. ***(Mirror)***

### SUAREZ ATAFUTIWA MBADALA

KOCHA wa Barcelona, Quique Setien amesema klabu hiyo inatazama uwezekano wa kuziba pengo la kiungo majeruhi, Luis Suarez, 32, mwezi huu. ***(Sport)***

### SPURS, CHELSEA VITANI

TOTTENHAM imetoa ofa kwa kiungo wa Lille, Boubakary Soumare, 20, hivyo kujiunga na Chelsea na Manchester United katika kujaribu kumsajili Mfaransa huyo. ***(L'Equipe, via Sun)***

### AITULIZA ASTON VILLA

KIUNGO wa Aston Villa na England, Jack Grealish, 24, ameiambia klabu hiyo hataondoka katika dirisha hili la Januari na kwamba mtazamo wake ni katika Ligi Kuu. ***(Mirror)***

### UNITED YAMFUATA JUDE

MANCHESTER United imetoa ofa zaidi ya pauni milioni 30 kwa kiungo wa Birmingham City, Muingereza Jude Bellingham. ***(Sun)***

### MORENO ATAJWA BARCELONA

BARCELONA inamwona mshambuliaji Mhispania Rodrigo Moreno, 28, kama usajili unaowezekana, lakini Valencia inaweza kuhitaji euro milioni 60 kwa mchezaji huyo aliyewahi kuichezea Bolton kwa mkopo. ***(Marca)***

### SPURS KUKWAMA KWA SLIMANI

MSHAMBULIAJI wa Leicester City na Algeria, Islam Slimani hana kipengele kinachomruhusu kurejeshwa kutoka Monaco anapocheza kwa mkopo, jambo linalofanya kuwa vigumu kwa Tottenham kumsajili katika dirisha hili la Januari. ***(Leicester Mercury)***

### KUJITOSA KWA ROSE

NEWCASTLE United inataka kwenda kumsajili kwa mkopo beki wa kushoto wa Tottenham na England, Danny Rose. ***(Telegraph)***

### ODRIOZOLA ATUA BAYERN

BEKI wa kulia wa Real Madrid, Mhispania Alvaro Odriozola, 24, ametua Ujerumani kukamilisha uhamisho wake wa mkopo wa kujiunga na Bayern Munich kwa kipindi chote cha msimu kilichobaki. ***(AS - in Spanish)***

HABARI MICHEZO

## Stars yaangukia pagumu kufuzu Kombe la Dunia

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA imepangwa Kundi J katika kuwania tiketi ya fainali za Kombe la Dunia mwaka 2022 nchini Qatar pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Benin na Madagascar.

Katika droo iliyopangwa juzi jijini Cairo, Misri ikihusisha nchi 40 wanachama wa Shirikisho la Soka Afrika (Caf) jumla ya makundi 10 yalipangwa katika hatua hii ya pili ya mbio za Qatar 2022 ambapo kila kundi litatoa timu moja zitakazocheza mechi ya mtoano kabla ya kupata timu tano zitakazofuzu fainali hizo.

Kundi A linaundwa na mabingwa wa Afrika, Algeria, Burkina Faso, Niger na Djibouti wakati Kundi B zipo Tunisia, Zambia, Mauritania na Equatorial Guinea huku Kundi C zikiwamo Nigeria, Cape Verde, Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR) na Liberia.

Kundi D linazikutanisha Cameroon, Ivory Coast, Msumbiji na Malawi, Kundi E likiwa na Mali, Uganda, Kenya na Rwanda huku Kundi F likiundwa na Misri, Gabon, Libya na Angola, Kundi G kuna Ghana, Afrika Kusini, Zimbabwe na Ethiopia, Kundi H Senegal, Kongo, Namibia na Togo na Kundi I Morocco, Guinea, Guinea-Bissau na Sudan.

## Meza kurindima Januari 24-26 Dar

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Mpira wa Meza Tanzania (TTTA), kinatarajia kufanya mashindano ya wazi ya mchezo huo yatakayofanyika Januari 24-26, mwaka huu kwenye viwanja vya Shule ya Msingi Aghakhan Jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa chama hicho, Issa Mtasalo alisema tayari Uganda, Zambia, Malawi, Kenya pamoja na wenyeji Tanzania Bara na Visiwani zimethibitisha kushiriki.

Alisema kutakuwa na aina saba ya mashindano siku hiyo, na kuwataka wadau mbalimbali wa mchezo huo kujitokeza kwa wingi kushuhudia.

Katibu huyo alisema hayo mashindano ya wazi ambayo kila mtu anaruhusiwa kushiriki ili kuboresha na kuinua zaidi vipaji vya mchezo huo.

# RT YATOA BARAKA GOBA HILLS MARATHON, ZAWADI ZATAJWA

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI waandaaji wa mbio za Goba Hills Marathon wakitangaza zawadi zitakazotolewa kwa washindi, Chama cha Riadha Tanzania (RT), kimetoa baraka zao na kutambua mbio hizo zinazotarajiwa kufanyika Februari 2, mwaka huu.

**Baraka na utambuzi huo umewekwa hadharani jijini Dar es Salaam jana na Kaimu Katibu Mkuu wa RT, Ombeni Savara wakati wa mkutano na waandishi wa habari.**

"Sisi RT kazi yetu ni kusimamia mbio mbalimbali hapa nchini kwa niaba ya serikali. Ni furaha kuona kuwa Klabu ya Michezo ya Goba Road Runners (GRR), leo wamezindua mbio zao za Goba Hills Marathon ambazo kwa kila mwaka zitakuwa zikifanyika Februari 2," Savara alisema.

"Naomba nitoe rai kwa waandaaji kuhakikisha kuwa taratibu zote za kuandaa mbio zozote zinafuatwa ili kuondoa malalamiko kutoka kwa washiriki. Pia ni muhimu kuweka zawadi hadharani kabla ya siku ya mbio hizo."

Kwa upande wake Ofisa Michezo wa Manispaa ya Ubungo, Fredrick Kadewele, alitoa wito kwa wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam kujitokeza kwenye mbio hizo za Goba Hills Marathon kwa kuwa manispaa yake imetoa kipaumbele kuhakikisha michezo inakua.

"Wote tunajua michezo ni ajira. Hata hivyo michezo pia inasaidia mwili kuwa na afya pamoja na kufahamiana. Mazingira yetu tumeweka kuwa rafiki na ni imani yangu kuwa mbio hizo zitakuwa ni chachu ya kuendeleza michezo kwenye manispaa yetu kwa ujumla," Kadewele aliongeza.

Naye Mwenyekiti wa Klabu ya Goba Road Runners (GRR), Benson Luoga, alisema klabu hiyo ya michezo imesajiliwa na Baraza la Michezo Tanzania (BMT) kwa cheti chenye usajili namba 12420, huku lengo kubwa likiwa ni jukwaa la kuhamasisha jamii kushiriki mazoezi na hasa ya ukiambiaji kwa ajili ya kupunguza magonjwa nyemelezi na yasiyoambukiza, kufahamiana na kufarahi kwa pamoja.

Luoga alisema lengo la mbio hizo kwa mwaka huu ni kuchangia fedha kwa ajili ya kuboresha vituo vya afya na kukuza vipaji vya vijana kutokana na mapato ambayo yatapatikana.

Alisema kutakuwa na mbio za kilometa 42.2, kilometa 21.1, kilometa 10 na kilometa tano huku waendesha baiskeli wakiwa na nafasi ya kuendesha kwa kilometa 42.2 na kwamba kila mshiriki atatakiwa kujisajili kwa kulipia ada ya ushiriki ya kiasi cha Sh. 25,000 kwa kilometa 42, kilometa tano na waendesha baiskeli.

Kwa washiriki wa mbio za kilometa 10 na 21.1, alisema watatakiwa kujiandikisha kwa ada ya Sh. 30,000, huku akifafanua kuwa kupitia ada hiyo kila mshiriki atakayemaliza atapata medali, fulana na bangili ya kuvaa mkononi.

"Kwenye mbio za kilometa 42 wanaume na wanawake zawadi itakuwa ni Sh. 500,000 kwa mshindi wa kwanza, Sh. 300,000 kwa mshindi wa pili, Sh. 200,000 kwa mshindi wa tatu huku mshindi wa nne na wa tano wakipata Sh. 100,000 na Sh. 75,000 kwa kila mmoja," Luoga alisema.

"Kwenye mbio za kilometa 21 kwa wanaume na wanawake zawadi zitakuwa ni Sh. 400,000 kwa mshindi wa kwanza, Sh. 250,000 kwa mshindi wa pili, Sh. 150,000 kwa mshindi wa tatu huku mshindi wa nne na tano wakipata Sh. 50,000 kwa kila mmoja.

"Kwa upande wa kilometa 10, mshindi wa kwanza wanaume na wanawake zawadi itakuwa ni Sh. 200,000 kwa mshindi wa kwanza, Sh. 150,000 kwa mshindi wa pili huku mshindi wa tatu akipata Sh. 100,000."

Luoga aliongeza kuwa kutakuwa na zawadi maalum kwa watu wenye ulemavu kwa mbio za kilometa 21 ambapo mshindi wa kwanza atapata Sh. 300, 000, mshindi wa pili Sh. 150,000 huku mshindi wa tatu akipata Sh. 50,000.

Aliwataja wadhamini wa mbio hizo kuwa ni Azam TV, Michuzi Blog, FastHub, SGA, Hill Water, Dasani Driking Water, ZENUFA Pharmaceuticals, Swahili Sweat Shop, Atlas Schools, Galaxy Energy, Red Bull, SDN, Flamingo Entertainment na Commercial Bank of Africa (CBA).



Beki wa kati wa Manchester City, Nicolas Otamendi akijaribu kufunga kwa 'kubinjuka' wakati wakiibuka na ushindi wa bao 1-0 ugenini juzi, kwenye mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Sheffield United. **PICHA: DAILY MAIL**

# *Mrisho Ngassa afungiwa, Mbelgiji Yanga aonywa*

**Na Shufaa Lyimo**

KAMATI ya Uendeshaji na usimamizi wa Ligi Kuu ya Tanzania (Kamati ya Saa 72) baada ya kukutana Jumatatu wiki hii, imewakuta na hatia wachezaji watatu wa Yanga, Mrisho Ngassa, Ramadhani Kabwili, na Cleofas Sospeter, hivyo kuwafungia kucheza michezo mitatu pamoja na faini ya Sh. 500,000 kila mmoja, imeelezwa.

Aidha, Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Mbelgiji Luc Eymael, amepewa onyo kwa kutoa matamshi yasiyofaa kuhusu ubaguzi wa rangi dhidi yake.

Eymael alitoa kauli hiyo wakati Yanga ikilala kwa bao 1-0 dhidi ya Azam FC iliochezwa Januari 18 katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam. Sambamba na onyo hilo, kamati hiyo imeutaka uongozi wa Yanga kukemea na kulitolea tamko kuhusiana na kauli hizo za ubaguzi wa rangi.

Wachezaji wengi waliokumbana na adhabu kama wa Yanga ni wa Klabu ya Mbeya City, Kelvin John na Majaliwa Shabani ambao wote kwa pamoja wameadhibiwa kutokana na kugoma kuingia vyumba vya kubadilishia.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi Steven Mguto, alisema wamechelewa kutoa maamuzi hayo baada ya mwezi uliopita kuwapo na sikukuu nyingi, lakini kwa sasa kamati hiyo itakuwa ikikutana kila Jumatatu kujadili matukio mbalimbali ambayo yatakuwa yanafanyika katika ligi.

"Tumeamua kutoa adhabu hiyo kwa wachezaji hao ambao walienda kinyume na Kanuni za Ligi ya 38 (9) ili iwe fundisho kwa wachezaji wengine na haya matatizo yamekuwa yanajirudia mara kwa mara lakini kwa sasa tutayadhibiti," alisema Mguto.

Mwenyekiti huyo alisema Klabu ya Yanga na Tanzania Prisons pia zimepigwa faini ya Sh. 500,000 katika mchezo namba 22 uliochezwa Desemba 29, mwaka jana baada ya kuchelewa kuwakilisha mapema majina ya vikosi vyao kabla ya mchezo kwenye kikao cha maandalizi ya mechi.

# Michezo

Alhamisi Januari 23, 2020


Nipashe




Inter yamgeukia Modric

HABARI UK.29

**UMETUOKOA...**



Beki wa Arsenal, Hector Bellerin (kulia), akishangilia na Granit Xhaka baada ya kuifungia timu hiyo bao la kusawazisha dhidi ya Chelsea zikiwa zimesalia dakika tatu kabla ya mechi hiyo ya Ligi Kuu England kumalizika, wakati wakitoka sare ya mabao 2-2 kwenye Uwanja wa Stamford Bridge juzi. **HABARI UK. 30**

# Eymael aweka rekodi Yanga ikiiua Singida

## ●●● Soka lakuvutia latawala, Molinga na usajili mpya walipa, Azam FC nayo yachanua huku...

**Na Somoe Ng'itu,** SINDIGA

WAPE Salam! Ikicheza kandanda safi na la kujiamini, Yanga ya jijini Dar es Salaam imeibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Singida United katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Liti (zamani Namfua) mkoani hapa.

**Ushindi huo ni wa tatu kwa Yanga dhidi ya Singida United baada ya timu hizo kukutana katika michezo sita, lakini ukiwa wa kwanza kwenye uwanja huo uliofunguliwa hivi karibuni baada ya kukamilika matengenezo.**

Kwa matokeo hayo, Kocha mpya wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael, amevunja mwiko wa timu hiyo kutokupata matokeo chanya katika uwanja huo, lakini huo ukiwa ushindi wake wa kwanza katika michezo mitatu tangu aanze kuinoa timu hiyo.

Hivyo, Yanga ambayo huo ni mchezo wake wa 15 katika Ligi Kuu msimu huu, imepanda hadi nafasi ya nne kutoka ya nane baada ya kujikusanyia jumla ya pointi 28, wakati Singida United walioshuka dimbani mara 17 wanaendelea kubaki katika nafasi yao ya 19 wakiwa na alama zao 10.

Mshambuliaji, David Molinga 'Falcao' ndiye aliyewanyanyua mashabiki wa Yanga baada ya kufunga bao la kwanza akiunganisha pasi fupi kutoka kwa Mapinduzi Balama na kupiga shuti lililopanguliwa na kipa Owen Chaima, lakini ukarejea kwake na kuumalizia kwa kupachika wavuni. Bao hilo lililofungwa dakika 12 na Mkongomani Molinga ni la tano kwake msimu huu, na liliwafanya Yanga waende mapumziko wakiwa mbele kwa goli 1-0.

Dakika ya 57, kiungo wa kimataifa wa Yanga kutoka Rwanda na mchezaji mzoefu katika Ligi Kuu Tanzania Bara, Haruna Niyonzima aliifungia timu yake bao la pili baada ya kumalizia kazi nzuri iliyofanywa na winga Mghana Bernard Morrison.

Ikionyesha wametimiza kauli yao kwamba walikuja Singida kwa kazi moja ya kuzoa pointi tatu, dakika ya 77 straika mpya Yikpe Ghislain aliyeingia kuchukua nafasi ya Molinga, alifunga bao la tatu na la kwanza tangu ajiunge na Yanga kwa kuuweka wavuni kwa kichwa mpira uliokuwa unazagaa jirani na lango la Singida baada ya kuokolewa na Chaima.

Yanga wakionekana kama wameshamaliza mechi, Sixtus Mwasekaga aliifungia Singida United bao pekee katika mchezo huo kwa kichwa akiunganisha krosi iliyopigwa na Athumani Iddi 'Chuji' dakika ya 83.

Hata hivyo, Yanga ilipoteza nafasi kadhaa katika kipindi cha kwanza kuliko wenyeji wao Singida United kwa Chaima kuwahi kuokoa mpira uliopigwa na beki Juma Abdul na kuwanyima wageni hao bao la mapema katika dakika ya 12 mchezo huo.

Dakika mbili baadaye, Singida United ilijibu shambulizi hilo kupitia kwa Aaron Lulambo, lakini kipa wa Yanga, Metacha Mnacha aliwahi kuokoa hatari hiyo langoni mwake huku Chaima akipangua tena mpira wa kichwa uliopigwa na Molinga dakika ya 24.

Metacha alidaka shuti la Haji Mwinyi ambaye aliunganisha mpira wa frikiki uliopigwa na Chuji dakika ya 85 na kuikosesha Singida United nafasi nyingine ya kufunga bao.

Katika mechi nyingine ya ligi hiyo, Azam FC ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Mwadui FC katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kambarage mkoani Shinyanga jana, likifungwa na Shabani Chilunda na kuifanya Azam FC ifikishe pointi 35 baada ya kucheza mechi 16 sawa na Simba iliyopo kileleni na alama zake 41.

# Samatta ahamisha mashabiki England

**Na Mwandishi Wetu**

KUTUA kwa mshambuliaji wa kimataifa wa Tanzania, Mbwana Samatta, katika klabu ya Aston Villa kumewavutia mashabiki wengi wa soka kuanza kuishabikia timu hiyo inayoshika nafasi ya 16 kwenye msimamo wa Ligi Kuu England ikiwa na alama 25 baada ya mechi 24.

Jumatatu usiku, Samatta alikamilisha usajili wake wa kujiunga na Aston Villa akitokea KRC Genk ya Ubelgiji kwa dau la pauni milioni 10, jambo ambalo limewafanya mashabiki wengi wa soka wa ndani na nje ya nchi ikiwamo England kutangaza kuisapoti timu hiyo.

Mbali ya Watanzania waishio England kueleza kumuunga mkono, shabiki wa Klabu ya Norwich City, Bongo Zozo, ambaye ni raia wa Uingereza ni miongoni mwa waliotangaza nia yao ya kuanza kuishabikia Aston Villa kutokana na Samatta kujiunga na timu hiyo.

Bongo Zozo ambaye anajulikana kwa mapenzi yake makubwa na Tanzania huku akiwa shabiki kindakindaki wa Taifa Stars, juzi alimwambia mwandishi wetu kwa njia ya simu kuwa amefurahishwa sana na kitendo cha Samatta kusajiliwa na Aston Villa.

"Kuanzia sasa na mimi ninaanza kuishabikia Aston Villa ingawa mimi ni shabiki mkubwa wa Norwich City, Samatta amefungua mlango kwa Watanzania kuja hapa lazima tumsapoti na kuwakaribisha kuja kumtembelea," alisema.

Mbali na Bongo Zozo, Nipashe lilitembelea kumbi na 'mabanda umiza' mbalimbali yanayoonyesha soka la England na kushuhudia wakiifuatilia Aston Villa wakati ikitokea nyuma na kushinda 2-1 dhidi Watford kwenye mchezo wa Ligi Kuu licha ya Samatta kutokucheza mechi hiyo.

"Manchester United na Arsenal sasa zinazingua kwa kutofanya vizuri, hivyo sehemu ya kujifariji itakuwa ni Aston Villa klabu anayocheza Samatta," alisema shabiki mmoja aliyejitambulisha kwa jina la Amani Shelukindo.

Samweli Mabuga, shabiki mwingine wa soka, alisema: "Hivi Samatta kapewa jezi namba ngapi? Kesho naenda Kariakoo kutafuta jezi ya Aston Villa nikiipata naandika namba yake aliyopewa."

Samatta ambaye amepewa jezi namba 20, anatarajiwa kuanza kuichezea timu watakapoikaribisha Leicester City Jumanne ijayo kwenye mechi ya Kombe la FA.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >